

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 22 Aprili, 2021**

*(Bunge Lilianza saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Mkutano wetu wa Tatu unaendelea, leo ni Kikao cha Kumi na Tano.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Malembeka, tunakushukuru sana.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 124

**Kupandisha Hadhi Kituo cha Afya Kinesi - Rorya**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, ni lini Kituo cha Afya Kinesi kitapandishwa hadhi na kuwa Hospitali kamili kutokana na kituo hicho kuhudumia wananchi zaidi ya vijiji 27 katika Jimbo la Rorya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, na kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya katika Wilaya ya Rorya katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali ilipatia Halmashauri ya Wilaya ya Rorya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ambapo tayari ujenzi wa majengo saba ya awali umekamilika na huduma za wagonjwa wa nje zinatolewa.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu ambapo tayari Halmashauri imeshazipokea fedha hizo na fedha shilingi milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba. Vilevile katika

mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali ya Halmashauri ya Rorya. Hivyo, Serikali haikusudii kupandisha hadhi Kituo cha Afya Kinesi kuwa Hospitali ya Halmashauri kwa kuwa Serikali inaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Rorya shilingi milioni 900 kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Afya Utegi kilichopewa shilingi milioni 500 na Kituo cha Afya Kinesi kilichopewa shilingi milioni 400 ambapo ujenzi na ukarabati wa vituo hivyo umekamilika na huduma za upasuaji zimeanza kutolewa. Aidha, Serikali imetenga shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma matatu ya zahanati katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo kimoja cha afya wilayani Rorya na shilingi milioni 150 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma matatu ya zahanati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Rorya, nilikuona.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nashukuru.

Niseme tu kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri nirudie kumuomba kama kuna uwezekano angalau wa kufika Rorya kuitambua na kuielewa jiografia ya Rorya ilivyokaa. Nimekuwa nikimuomba hii ni mara ya pili tena narudia kumuomba. Imani yangu akifika atagundua hiki Kituo cha Afya ambacho tumekuwa tukikizungumzia kinahudumia kata zaidi ya tano ikiwemo Kata ya Kyang'ombe, Baraki, Komuge, Kisumwa na Rabol. Inahudumia vijiji zaidi ya 27; *population wide* ambayo inakwenda kupata huduma pale sio chini ya watu 50,000 kulingana na jiografia ilivyokaa. Umbali wa kutoka kituo hiki cha afya mpaka Hospitali hii ya Wilaya inayojengwa ni zaidi ya kilometa 40 ndiyo maana mara ya

kwanza nilikuwa namuomba sana tupate daraja la Mto Moli ili kufupisha safari hii.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu la kwanza la nyongeza; Mheshimiwa Waziri haoni sasa kuna umuhimu wa kupandisha hadhi hizi zahanati ambazo ziko kwenye kata zinazozunguka kata hii ya Kinesi ikiwemo Kata ya Kyang'ombe, Banaki, Komuge na Kisumwa ili zile zahanati ziweze kutoa huduma kama vituo vya afya kukisaidia hiki kituo cha afya cha Kinesi *population wide* inayokwenda pale?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili la nyongeza Mheshimiwa Waziri huoni kuna umuhimu sasa kwa muktadha wa majibu haya hiki Kituo cha Kinesi angalau wpaate *ambulance* ili iweze kuwasaidia kwa umbali huo wa kilometa 40 wanaosafiri hasa tunapopata wagonjwa wa dharura kama akinamama wajawazito na wagonjwa wengine ambao wako *serious* kwenye matatizo kama haya? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa. Dkt. Festo Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Wambura Chege kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatetea wananchi wa Jimbo la Rorya na kuhakikisha wanapata huduma bora za afya ili tuhakikishe kwamba wananchi wale wanaona matunda mazuri ya Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kituo hiki cha afya kinahudumia wananchi wengi katika vijiji takribani 27 na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimeeleza namna ambavyo Serikali imeendelea kutoa fedha zaidi ya shilingi milioni 900 katika kituo hicho; kwanza, kuhakikisha majengo yanakamilika lakini pia kuendelea kukipanua kituo kile ili

kiendeleo kutoa huduma bora kwa hao wananchi wengi ambao kituo kinawahudumia. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba tutaendelea kukiboresha kituo kile cha afya, lakini pia zahanati zinazozunguka kituo cha afya, sera na mpango wa maendeleo ya afya msingi tunahitaji kituo cha afya katika kila kata na kila zahanati katika kila Kijiji. Kwa hiyo, kama kuna zahanati ambazo ziko nje ya kata ilipo Kituo cha Afya cha Kinesi tunaweza kupanddisha hadhi zahanati hizo zikawa Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la *ambulance*, ni kweli tunahitaji kuwa na magari ya wagonjwa kwa ajili ya dharura na tutakwenda kuweka mpango wa kuhakikisha kituo hiki cha Kinesi kinapata gari la wagonjwa ili kiweze kurahisisha huduma za rufaa.

**SPIKA:** Waheshimiwa leo hatutakuwa na maswali ya nyongeza. Tutakuwa na maswali ya msingi tu kwa sababu mnajua leo tunakimbizana na muda.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Mbunge wa Ulyankulu, Mheshimiwa Rehema Juma Migilla.

Na. 125

### **Ujenzi wa Barabara ya Mpanda – Ulyankulu - Kahama**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

(a) Je, kwa nini barabara ya Mpanda – Ulyanhulu – Kahama haikujengwa katika kipindi cha 2015 – 2020 kama ilivyoelekezwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015 - 2025?

(b) Je, ni lini sasa ujenzi wa barabara hiyo utaanza kama ilivyoelekezwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 – 2025?

**SPIKA:** Majibu ya Walyankulu Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Msongwe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu swali la Mheshimwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyanhulu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mpanda – Ugala – Kaliua – Ulyanhulu yenye urefu wa kilometa 457 inayounganisha Mikoa ya Katavi, Tabora na Shinyanga ni moja ya barabara zilizopo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020. Barabara hii ipo kwenye kundi la miradi inayotakiwa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, mkataba kwa ajili ya Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa barabara ya Mpanda – Ugala – Kaliua – Ulyankulu – Kahama ulisainiwa tarehe 18 Agosti, 2020 kati ya Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) na Kampuni ya *Crown Tech Consult Ltd* kwa gharama ya shilingi milioni 940.30. Kazi hii itafanyika ndani ya miezi 12 na inatarajiwa kukamilika Septemba, 2021. Mara baada ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina kukamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, wakati kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiendelea, Wizara yangu kupitia *TANROADS*, inaendelea kuihudumia barabara hiyo ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Aidha, ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa ili ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ufanyike, hatua mbalimbali hufuatwa ambazo ni pamoja na upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, utayarishaji wa nyaraka za zabuni na taratibu za ununuzi wa kumpata mkandarasi wa ujenzi. Hivyo, kuanza kwa hatua tajwa, maana yake ni kuanza kwa mradi husika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Majibu ya Serikali kupitia Waziri hayaoneshi matumaini kwa wananchi wetu wa Ulyankulu kwamba wanaenda kupata lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hii ilikuwemo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020 lakini pia kwenye Ilani ya Uchaguzi ya 2020/2025 barabara hii imo. Majibu ya Serikali yanaonesha barabara hii kwa kipindi chote hicho itakuwa tu kwenye upembuzi yakinifu.

Je, kwa miaka hii mitano mingine barabara hii ina uhakika wa kutengenezwa ili wananchi wangu waweze kupata barabara ya lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni kwamba Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alipotembea Jimboni kwetu Ulyankulu alitoa ahadi ya kututengenezea kilometa tatu kwenye Jimbo letu la Ulyankulu. Lakini tangu kipindi hicho mpaka leo hakuna hata kilometa moja iliyotengenezwa kwa kiwango cha lami.

Swali langu ni je, kupuuzwa kwa kutekeleza kwa kujengwa kwa hii barabara kwa hizo kilometa tatu ni kupuuzwa ahadi ya Mheshimiwa Rais au na kuwadharau wananchi wake waliompigia kura? Naomba majibu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Migilla, Mbunge wa Ulyankulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Migilla kama amenisikiliza kwenye jibu langu la msingi ni kwamba tayari usanifu wa kina unaendelea na utakamilika Septemba mwaka huu. Barabara haiwezi ikaanza kujengwa kabla ya kukamilika kwa usanifu. Atakuwa ni shahidi kwamba

wakandarasi wanaofanya usanifu wako *field* na Wizara inatambua kwamba barabara anayoitaja ni barabara muhimu sana kwani katika Jimbo lake tunatambua lina uzalishaji mkubwa sana wa mazao kama mahindi, mpunga na hata tumbaku.

Mheshimiwa Spika, hii barabara sasa ndiyo inayokwenda kwenye mbuga ambazo zimetambuliwa kama *National Park* ya Ugalla na nimhakikishie kwamba katika bajeti ya mwaka ujao pia tumetenga fedha kwa ajili ya kufungua na kuanza ujenzi wa Daraja la Ugalla ili kuunganisha Jimbo lake na Mkoa wa Mpanda. Ni barabara ambayo tayari wakandarasi wapo wakiwa wanaifungua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimalizie kwa kumhakikishia Mheshimiwa Migilla haitatokea na haiwezekani Serikali hii ikapuuza ahadi za viongozi wetu wa Kitaifa. Ahadi imeahidiwa mwaka uliopita isingekuwa rahisi tuwe tayari tumeshajenga hizo barabara na ndiyo maana tunasema tayari wakandarasi wako *site* wakifanya usanifu wa kina.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge barabara hiyo itajengwa na wananchi waiamini Serikali yao kwamba yaliyoahidiwa na yaliyoko kwenye Ilani yatatekelezwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunahamia Wizara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri.

Na. 126

**Kuwawezesha Wakulima Kulima Zao la Alizeti,  
Michikichi na Karanga**

**MHE. MARIAM D. MZUZURI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha wakulima nchini kuwekeza katika kilimo cha mazao ya alizeti, michikichi na karanga ili kuokoa kiasi cha fedha zinazotumika kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi?



**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, mkulima na mjasiriamali katika sekta ya kilimo kuwa Serikali inaona umuhimu wa kuwekeza kwenye mazao ya kuzalisha mafuta ambapo uwekezaji huo unatekelezwa chini ya mikakati ya kutatua changamoto katika sekta ya uzalishaji wa mafuta kwa kushirikisha Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu - Wizara ya Viwanda na Biashara. Mikakati hiyo inalenga kutatua changamoto ya uzalishaji wa mbegu za mafuta ili kujitosheleza kwa mahitaji ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 Serikali imewekeza jumla ya shilingi 5,820,361,798 kwa ajili ya kuendeleza zao la chikichi ambapo kufikia tarehe 31 Januari jumla ya miche bora ya michikichi 2,244,935 imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga jumla ya shilingi 3,158,200,000 kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza mbegu na miche ya zao la michikichi.

Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha uzalishaji wa mbegu za alizeti unaongezeka katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imeiwezesha taasisi ya ASA jumla ya bilioni tatu kwa ajili ya kuzalisha mbegu za alizeti. Vilevile, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imepanga kuiwezesha ASA shilingi bilioni 10.6 ili kuzalisha tani 5,000 za mbegu ya alizeti kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa mbegu za mafuta

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza gharama za kilimo kwa mkulima Wizara imeanzisha miradi ya *block farming* katika mikoa ya uzalishaji mbegu za mafuta ikiwemo alizeti michikichi na pamba ambapo katika mwaka ujao wa fedha Serikali tutatoa kipaumbele kwa kilimo cha uzalishaji mbegu kwa mfumo wa *block farming* kwenye baadhi ya

mikoa kwa ajili ya uzalishaji mbegu za alizeti, pamba na michikichi. Mahitaji ya mafuta ya kula nchini yanakadiriwa kufika tani 570,000 kwa mwaka. Aidha, uzalishaji wa mafuta ya kula nchini unakadiriwa kufikiwa wastani wa tani 205,000 na kufanya upungufu wa wastani wa tani 365,000 kwa mwaka, ambapo husababisha nchi kutumia shilingi bilioni 474 kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi kwa mwaka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwanza niipongeze Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwani wamekuwa wanafanya programu nyingi sana za kumwezesha mkulima hasa wa alizeti. Lakini pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mbegu bora ndio ambayo inazalisha zao bora, lakini changamoto kubwa ambayo inawapata wakulima wetu ni upatikanaji wa mbegu bora, lakini tuliona Serikali ikizindua mpango rasmi wa kugawa miche ya korosho kupitia Bodi ya Korosho katika Mikoa ya Kanda ya Kati, lakini sifa kubwa ya mikoa hii hususan Dodoma, Singida, Manyara na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro ni mikoa ambayo inazalisha alizeti bora sana. *(Makofi)*

Je, Serikali kwa nini haioni sababu yak ama walivyogawa mikorosho, wawe na programu maalum ya kugawa mbegu bora za alizeti kwa mikoa hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, niipongeze Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, hususan Naibu Waziri wetu Mheshimiwa Hussein Bashe, amekuwa ni msikivu na kutatua changamoto zetu kwa haraka. Wamefuta mfumo wa kuuza mazao kwa mfumo wa *TMX* ambao kwa kweli ulikuwa kero kubwa sana kwa wakulima wetu, lakini pia hawaoni haja ya kusitisha pia mfumo wa stakabadhi ghalani, hususan kwa mikoa ambayo bado hawana miundombinu na mfumo mzuri kwa ajili ya stakabadhi ghalani?

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri hapa Mkoa wetu wa Dodoma, Wilaya za Chemba, Bahi na Kondoa ambao tunazalisha sana ufuta na choroko, hatuna *AMCOS*, hatuna uongozi wowote. Kwa nini wasitoe muda ili tuweze kujiandaa tuunde mifumo mizuri halafu ndio tuweze kuanza kutumia mfumo huu wa stakabadhi ghalani? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nimevumilia kidogo kwa sababu maswali haya ndio yanayogusa wananchi. Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali. (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam Ditopile wa Mzuzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tusigawe mbegu za alizeti kama ambavyo tuligawa miche ya korosho?

Mheshimiwa Spika, sababu ya Serikali kugawa miche ya korosho kwa wakulima katika mikoa ambayo ni mipya ya uzalishaji wa korosho ama michikichi sababu ya kwanza ni zao la korosho na zao la michikichi *return on investment* kwa mkulima inachukua muda mrefu sana. Ukiangalia korosho mpaka mkulima aanze kupata mapato ni baada ya miaka mitatu, kwa hiyo, mfumo wa ku-*finance input* inakuwa kidogo ni gharama kwa mkulima na inakuwa inamuingia gharama nyingi, kwa hiyo, Serikali iliamua kuchukua hiyo hatua, ili kuweza kumpunguzia makali ya kununua miche na kuihudumia kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye alizeti hatua ambayo tunachukua kama Serikali nikiri kwamba upatikanaji wa mbegu bora imekuwa ni changamoto na gharama ya mbegu inayopatikana ni kubwa kwa hiyo, mkakati wa Wizara ya Kilimo na mtakuja kuona kwenye bajeti yetu mwaka huu, *Inshallah* Mungu akijalia, ni kwamba tunawekeza katika mashamba ya Serikali, mifumo ya umwagiliaji. Na kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba *ASA* tutawapatia fedha kiasi cha shilingi bilioni 10. Hatua ya kwanza tunayoichukua ni kufanya jitihada na mwaka huu

tumeanza kuishusha bei ya mbegu ya alizeti kutoka 35,000 ambayo wanayo sasahivi mpaka angalao shilingi 17,500 kwa kilo mbili kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, nah atua hii tunaifanya kwa kuiwezesha ASA na mwaka huu imefanya *pilot project*. Imeza mbegu zake za aina ya *OPV* ambazo uzalishaji wake wa mafuta hauna tofauti na mbegu ya *high breed* inayouzwa na kampuni binafsi kwa shilingi 35,000.

Kwa hiyo, tunaamini kwamba, kwa kuisaidia ASA itatusaidia kupatikana mbegu ya kutosha na tutasambaza kwa wakulima na katika bajeti yetu kuna mikoa ambayo ni ya uzalishaji wa alizeti ambayo tutaitaja katika bajeti ambayo tutaifanyia majaribio ya kupata mbegu, lakini vilevile tutaifanyia majaribio ya mifumo ya kusambaza mbegu hizo kwa wakulima, lakini vilevile kuwafanyia majaribio ya *end to end contract*, ili mkulima kama hana fedha tutengeneze utaratibu utakaomhusisha mnunuzi, mkulima apate mbegu bora na aweze kuzalisha shambani na kumuuzia mnunuzi moja kwa moja.

Kwa hiyo, hatuwezi ku-*committ* hapa kwamba, tutagawa mbegu za alizeti bure, lakini tunachoweza ku-*committ* ni upatikanaji wa mbegu za kutosha, lakini vilevile kuishusha bei kutoka 35,000 mpaka 17,500 ama elfu 15 kwa kilo mbili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mfumo wa stakabadhi ghalani; kwanza ni vizuri nitumie Bunge lako Tukufu ikaeleweka. Stakabadhi ghalani ni maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, hili ni jambo la kwanza, lakini la pili stakabadhi ghalani ni mfumo ambao unasaidia kupatikana kwa bei halisi ya zao (*price discovery*). Ndio lengo la uwepo wa mfumo wa stakabadhi ghalani kwa ajili ya ushindani.

Mheshimiwa Spika, lakini ili uweze kutekeleza mfumo wa stakabadhi ghalani kuna mambo ya msingi ambayo ni lazima yawepo; la kwanza lazima kuwepo kwa chama cha msingi cha ushirika, ili wakulima waweze ku-*aggregate*, la

pili lazima kuwepo na maghala, la tatu lazima kuwepo na wanunuzi ambao watashindana kwa uwazi.

Mheshimiwa Spika, ninakiri kwa niaba ya Serikali na Wizara kwamba yapo maeneo ambayo mfumo wa stakabadhi ghalani una changamoto. Na kama tulivyoamua kustopisha (*stop*) mfumo wa *TMX* tutasitisha katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu kwa mwaka mmoja wakati tunajenga ushirika imara katika maeneo hayo, lakini maeneo hayo mfano Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Singida, lakini Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Songwe katika maeneo haya hatuna ushirika imara, kwa hiyo, sasahivi timu yetu inafanya kazi ya kupita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na nitumie Bunge lako Tukufu kuwaomba Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi katika mikoa hii kwa mwaka huu, hatua ya kwanza wanayotakiwa kufanya wachukue, wasajili wanunuzi wote wa mazao ya ufuta, choroko na, dengue katika maeneo yao na wawapatie leseni bure. Hatua ya pili wazuwite uzaji wa mazao ya ufuta, choroko na dengue kwa kutumia madebe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi, leo katika Wilaya ya Songwe mkulima anauza debe la kilo 14 kwa shilingi 20,000 ufuta, ambayo ni sawasawa na shilingi 1,400 *average per kilogram*, huu ni wizi, wakati *FOB rate* ya ufuta ni shilingi 3,000 katika *port* ya Dar Es Salaam. Kwa hiyo, tutatoa waraka na maelekezo ya namna ya kufanya, lakini Halmashauri zivasajili wanunuzi bila kuwa-charge chochote, zianzishe *point of sale* katika kila kijiji na waweke mizani. Ni marufuku kuuza mazao ya kilimo kwa kutumia madebe na kufunga kwenye lumbesa. Nashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, maana hapa Dodoma mimi nafahamu wakulima wangu ambao wameacha kabisa kulima ufuta maana ukilima ufuta ni kama unataka kufungwa kwa zao lako mwenyewe kwa sababu ya hizo *AMCOS* ambazo kwanza hazipo. Tunashukuru sana

Serikali kwa hatua hiyo angalau kujenga misingi ile mwanzoni hapa, baadaye ita-*pick up*.

Wizara ya Nishati. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, uliza swali lako tafadhali.

Na. 127

### **Ufungaji wa Umeme Vijiji Visivyokuwa na Umeme**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, ni lini umeme utapelekwa katika Vijiji vya Buzi, Buguruka, Musina, Nsheshe na vingine ambavyo havijafikiwa na umeme katika Jimbo la Bukoba Vijijini?

**SPIKA:** Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ya swali hilo kutoka kwa wananchi wa Vijiji vya Bukoba.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inaendelea kupeleka umeme na kufikisha katika vijiji vyote vya Tanzania Bara ifikapo Desemba, 2022. Vijiji vinane kati ya vijiji 94 vya Bukoba Vijijini ambavyo ni Kijiji cha Buzi, Buguruka, Musira, Nsheshe, Ngarama, Omubweya, Kagarama na Rukoma vinatarajiwa kupatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulianza kutekelezwa Mwezi Machi, 2021 na unatarajia kukamilika Mwezi Desemba, 2022 na gharama ya mradi huu kwa Jimbo la Bukoba Vijijini ni shilingi bilioni 2.04.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jasson.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu yanayotia matumaini kutoka Serikalini, lakini ametaja vijiji ambavyo bado havijapata umeme, kuna kimoja hakukisema ambacho kinaitwa Ruhoko. Kijiji hiki kimefungwa waya zote, kimefungwa transfoma, kimewekwa nguzo, kila kitu kimekamilika mwaka wa pili leo umeme haujawashwa kwa nini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; amesema vijiji nane kati ya vijiji 94 ambavyo vimesalia kupata umeme, lakini na vitongoji 515, kati ya vitongoji hivyo vyenye umeme ni 86 tu zaidi ya vijiji 400 havina umeme. Utaratibu ukoje kuhusu vitongoji hivyo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Jasson Rweikiza. Zamani Jimbo hili la Bukoba Vijijini lilikuwa linaongozwa na Marehemu Sebastian Kinyondo na yeye alikuwa anakataa kuliita Jimbo la Bukoba Vijijini, alikuwa analiita Jimbo la Vijiji vya Bukoba kwa sababu vijiji vya Bukoba ni vikubwa kama miji.

Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Byabato.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Samson Jasson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, na-*declare interest* kwamba mimi natoka Jimbo la Bukoba Mjini na kabla ya utumishi wa Bunge nilikuwa mtumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba. Kijiji cha Luoko nakifahamu kiko katika Kata ya Katoro na katika ufuatiliaji wetu Kijiji cha Luoko tayari kilishapelekewa umeme, lakini tulipata changamoto ya kutopata wateja wa kuwaunganishia umeme katika kijiji hicho na hivyo miundombinu ile ilikuwa hajaanza kufanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, watakumbuka kuna kipindi Mheshimiwa Waziri wa Nishati alisema kwamba, wale ambao atawapelekea umeme na hawatataka kuunganisha basi

itabidi tutumie jitihada za ziada za kuwalazimisha kuunganisha ule umeme. Ningekuwa naweza kufanya hivyo na Kijiji cha Luoko kingekuwa kimojawapo ambapo tungewalazimisha wananchi kuunganisha umeme huo.

Mheshimiwa Spika, lakini tayari tumeshafanya *sensitization* na wananchi wa Luoko wako tayari kuunganishiwa umeme. Tumemuelekeza mkandarasi aliyekuwa anapeleka umeme katika kijiji hicho anaitwa Nakroi ambaye alipeleka umeme katika Awamu ya Pili ya Mzunguko wa *REA* na yuko tayari kupeleka umeme. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Kijiji cha Luoko kitapepekewa umeme ndani ya muda mfupi baada ya utaratibu wa kuunganishiwa wananchi kuwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili kuhusiana na vitongoji vya Jimbo la Bukoba Vijijini; upelekaji wa umeme kwenye vitongoji ni zoezi endelevu na kama ambavyo nimekuwa nikisema, tunapeleka umeme kwenye vitongoji katika njia tatu; kwanza *TANESCO* wamekuwa wakiendelea kupeleka umeme katika maeneo ya vitongoji vyetu, lakini njia ya pili ni kupitia hiyo miradi ya *REA* ambayo tumekuwa tukipeleka umeme kwenye vijiji na tunapeleka kwenye vitongoji, lakini njia ya tatu uko mradi maalum wa kupeleka umeme kwenye vitongoji unaoitwa *densification*. Na tulianza na *Densification* Awamu ya Kwanza tulipeleka katika mikoa nane, tukaja na *Densification Two (A)* tukapeleka katika mikoa tisa na sasa tuko *Densification Two (B)* inaendelea katika mikoa kumi na tutamalizia na *Densification Two (C)* ambayo tunatarajia ianze mwezi Julai kupeleka katika mikoa inayobakia.

Mheshimiwa Spika, tukiri kwamba hatuwezi kupeleka katika vitongoji vyote kwa wakati mmoja, lakini kama tunavyosema upatikanaji wa fedha na upelekaji wa umeme ni zoezi endelevu tunaamini ifikapo 2022 vijiji vyote Disemba vitakuwa vina umeme na kwenye vitongoji tutaendelea kupeleka kwa kadiri ya kuhakikisha kwamba, kila mwananchi anafikiwa na huduma ya umeme. Serikali Sikivu inapeleka umeme kw wananchi kwa maendeleo yao wenyewe.



**SPIKA:** Ahsante, tunahamia Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, uliza swali lako.

Na. 128

**Hitaji la Alama Kwenye Mpaka wa Tanzania na Kenya – Mkinga**

**MHE. MWANTUMU M. ZODO K.n.y. MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya zoezi la kuhakiki na kuweka alama kwenye mpaka wa Tanzania na Kenya kwa eneo la nchi kavu na baharini ili wananchi wa mpakani Wilayani Mkinga waondokane na kero ya muda mrefu ya kukamatwa na kutaifishiwa mali zao na askari wa Kenya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya una jumla ya urefu wa kilometa 817.71 ikiwa kilometa 758 ni nchi kavu na kilometa 59.71 ni ndani ya maji. Eneo la nchi kavu la mpaka huo linaanzia Ziwa Victoria, Wilaya ya Rorya Mkoani Mara hadi Jasini, Wilaya ya Mkinga Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa, sehemu ya mpaka wa Tanzania na Kenya yenye urefu wa kilometa 172 kutoka Ziwa Victoria hadi Ziwa Natron umeimarishwa na kuwekewa

alama 1,135. Kati ya alama hizo, alama 162 zimejengwa na kukarabatiwa na alama 973 zimejengwa kwa umbali wa mita 100 hadi 200 ili kuwezesha wananchi kuubaini mpaka kwa urahisi. Zoezi la kuimarisha mpaka kati ya Ziwa Natron hadi Namanga wenye urefu wa kilometa 128 kwa mwaka 2019/2020 liliahirishwa kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa *Covid-19*. Kutokana na uwepo wa ugonjwa huo, zoezi la kuimarisha mpaka uliobaki kati ya Tanzania na Kenya wenye urefu wa kilometa 586 kwa nchi kavu na kilometa 59.71 ndani ya maji limesimama hadi hapo nchi hizi mbili zitakapokubaliana. Urefu wa Mpaka katika Wilaya ya Mkinga katika mpaka huu ambao haujaimarishwa ni kilometa 52.96 ambayo ni nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya mpaka ndani ya Bahari ya Hindi kutoka Jasini hadi kwenye alama ya utatu kati ya nchi ya Tanzania, Kenya na Ushelisheli ina mkataba wa makubaliano kati ya nchi hizi tatu... katikati ya Kenya na Tanzania ambao ulitiwa saina tarehe 23 Juni, 2009 Jijini Dar es Salaam isipokuwa alama zake za maboya hazijawekwa. Kazi ya kuweka maboya katika mpaka huu itafanyika baada ya kukamilika uimarishaji wa mpaka katika eneo la nchi kavu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo kama una swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. naomba niulize maswali mawilinya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kijiji cha Jasini kwa Kata ya Moa na Mayomboni, Wilaya ya Mkinga wanapata usumbufu sana wa kukamatwa na askari wa Kenya na kwenda kushitakiwa Kenya na wakati mwingine mali zao kutaifishwa.

Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha hali hii inakoma?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili,...

**SPIKA:** Wanakamatwa kwa sababu gani?

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, wanaonekana wameingia Kenya, wakivua Kenya, ni eneo la bahari.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, askari wa Kenya mara kadhaa wanaingia Jasini, hali ambayo ni hatari sana kwa nchi zetu hizi mbili.

Je, ni lini sasa Serikali itachukua hatua za haraka za kuhakikisha inaweka mipaka ili kuhakikisha Serikali ya Kenya na Tanzania zisije zikaingia kwenye migogoro? Asante nashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikiri ni kweli katika eneo la Jasini kwenye Kata ya Moa na Mayombo mara nyingi kumekuwa kukitokea ukamataji wa wananchi wa eneo hilo na hili pia liliwahi kutokea wakati pia tuko ziara kule, nilishafika mpaka Jasini.

Mheshimiwa Spika, lakini kinachotokea hapa ni kutokana na kwamba katika uimarishaji wa mpaka tumesema tunaimarisha kwanza maeneo ya nchi kavu kwa sababu majini katika kuweka maboya tayari mpaka nchi zote mbili ziridhie wapi maboya yawekwe, pamoja na kwamba, tunajua kuna ule mbali wa *nautical miles* 200 ambazo ziko kwetu, lakini hii haijaweza kufanyika kutokana na hali halisi ambayo kila ukitaka kuweka alama lazima mkubaliane wote.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kushukuru sana Balozi zetu, Ubalozi wetu wa Kenya pamoja na ule mdogo wa Mombasa. Nimshukuru sana Mheshimiwa Pindi Chana wakati yuko pale wametatua matatizo mengi kutokana na kesi hizi na sasa hivi balozi aliyeko pale, *Consular* Athumani Haji aliyeko Mombasa, ni juzi toka miezi sita iliyopita wameweza kutatua pia changamoto hiyo ya kuweza kukamatwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo kutokuwekwa kwa maboya pale ni kutokana na makubaliano ya nchi mbili, lazima mkubaliane ndio muweke alama hizo. Bila kukubaliana hakuna nchi itakayoweza kuweka.

Mheshimiwa Spika, na kingine ambacho ni changamoto kule sasahivi wameanzisha sheria ya uvuvi ambayo chombo kinapoingia ziwani lazima ulipe dola 500 na ukikamatwa pale *fine* ni dola 300. Sasa mara nyingi wavuvi wetu wanakuwa hawana, lakini diplomasia imekuwa ikitumika wanajadiliana kati ya ubalozi n akule na watu wanatoka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba katika swali lake la pili analosema ni lini hii itakomeshwa? Niwaombe tu muwe na Subira kwa sababu mchakato unaendelea katika suala zima la kuimarisha mipaka kama ambavyo nimesema katika jibu langu la msingi. Tukiimarisha mipaka hiyo ya nchi kavu ikikamilika suala la kuweka maboya ndilo limebaki kwa sababu tayari mpaka ulishabainishwa isipokuwa ni kuweka alama tu. Tutaweka mara tutakapokuwa tumekubaliana na wenzetu wa Kenya.

**SPIKA:** Tunaishia hapo kwenye maswali ya leo, kwa sababu ya ratiba za kipeke yake za leo.

Wageni tulionao Bungeni kwenye Jukwaa la Spika, ambapo naomba nimtambulishie Katibu Mkuu - Ikulu Dkt. Moses Kusiluka, karibu sana, Katibu Mkuu - Utumishi Dkt. Laurean Ndumbaro karibu, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU - Brigedia Jenerali John Mbung'o, Kamishna wa Sekretarieti

ya Maadili ya Viongozi wa Umma - Mheshimiwa Jaji Mstaafu Sivangilwa Mwengesi, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni Ndugu zake kutoka Zanzibar, Ndugu Mohamed Likanga na Shemsa Ally, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni wa Mheshimiwa Jesca Kishoa kutoka Taasisi ya Nipe Fagio ya Dar es Salaam ambao Mkurugenzi Mtendaji wa Nipe Fagio Ndugu Anna Rocha na Mratibu Veronica Holela, ahsante. Hawa ndio wageni wetu leo. *(Makofi)*

Sasa Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Kuna mtu..., ongeza sauti.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Ahaa! wewe ndio unaongea hapo, *okey*.

Waheshimiwa Wabunge, subirini tunaelewa kinachoendelea *unless* kuna Mbunge anataka kuongea, kwa mezani hapa hakuna shida ninyi tulieni.

Waheshimiwa Wabunge kufuatana na yanayofuata leo mchana baadaye leo jioni ambapo nilishawatangazia siku ya Jumatatu tarehe 19 Aprili, 2021 kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan atalihutubia Bunge leo Alhamisi tarehe 22 Aprili, 2021 kuanzia saa 10.00 alasiri ya leo, kwa mujibu wa Ibara ya 91(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na

Kanuni ya 36(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020, kama mnavyofahamu Hotuba ya Mheshimiwa Rais Bungeni ni tukio kubwa la Kitaifa, hivyo ofisi yangu kuwaalika viongozi wakuu wa kitaifa kushuhudia tukio hilo.

Kwa taratibu zetu baadhi ya viongozi hao huingia humu ndani ya ukumbi wa Bunge, hivyo itabidi Kanuni zetu zinazohusiana na uingiaji Bungeni zitenguliwe ili kuwaruhusu viongozi hao kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge.

Kwa hatua hii ninamuita sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira vijana na Watu Wenye Ulemavu Mheshimiwa Jenista Mhagama awasilishe hoja ya kutengua Kanuni za Bunge. Mheshimiwa Waziri wa Nchi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ninatoa maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 174(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020.

KWA KUWA kama ulivyotutangazia kwamba leo tarehe 22 Aprili, 2021 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan atalihutubia Bunge la Kumi na Mbili kwa mujibu wa Ibara ya 91(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kanuni ya 36(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020.

NA KWA KUWA viongozi mbalimbali wa Kitaifa wamealikwa kuja kusikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Rais ambapo kwa mujibu wa taratibu na tamaduni za Bunge hili baadhi ya viongozi hao huingia ndani ya ukumbi wa Bunge.

NA KWA KUWA Kanuni ya 160(1) inaelekeza kwamba wageni wanaoruhusiwa kuingia Bungeni watakaa maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao, inabidi Bunge litengue kanuni hizi ili kuruhusu baadhi ya viongozi walioalikwa na

Mheshimiwa Spika, wasikae eneo maalum la wageni na badala yake waingie ndani ya Ukumbi wa Bunge.

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba Kanuni ya 160(1) itenguliwe ili viongozi wafuatao waingie ndani ya ukumbi wa Bunge leo tarehe 22 Aprili, 2021 na waketi sehemu itakayopangwa leo. Wageni hao ni kama wafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar - Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar - Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Zanzibar - Mheshimiwa Omary Othuman Makungu, Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar - Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na Spika wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki - Mheshimiwa Martin Ngoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, nawashukuruni sana. Sasa naomba niwahoji wale wanaoafiki kuhusiana na hoja ya Waziri wa Nchi.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Naona wote wameafiki, nawashukuru sana kwa kutoa ruhusa hiyo, na kwa hiyo baadaye kidogo hapa mbele patabadilika ili kuweza kuweka utaratibu ambao utahusisha viongozi hawa kuweza kupata mahali pa kukaa. *(Makofi)*

Ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge ni mambo ya ki-*protocol* ya kawaida, siku

anapokuja Kiongozi Mkuu wa nchi kama hivyo basi haishauriwi sana kwa wenzangu mimi kupiga tai nyekundu, nadhani tunakubaliana ile *red* inabakia na mwenye mamlaka, kwa hiyo, ni vizuri kuyajua haya mambo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, jioni tutakaporudi, sio wakati huu, wakati huu hakuna shida jioni tutakaporudi hapa basi tai nyekundu utarudia geti la nje. Ahsante sana tunakumbushana tu ni taratibu za kawaida. (*Kicheko/Makofi*)

Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**SPIKA:** Sasa naomba nimuite moja kwa moja Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mchengerwa karibu sana uweze kuendelea kutoa hoja yako. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwakuwa hotuba yetu ya Wizara hii ina kurasa 114 naomba uridhie sasa kurasa zote za hotuba hii ziingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako ili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, aomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu - Fungu 20 na 30, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma - Fungu 33, Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Fungu 32,



Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma - Fungu 67, Tume ya Utumishi wa Umma - Fungu 94, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma - Fungu Namba 9 na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa - Fungu Namba 4.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha mpango wa utekelezaji na makadirio ya fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia amani na utulivu ambavyo vimetuwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuwahudumia wananchi pamoja na kutuwezesha kukutana kwa ajili ya kupokea utekelezaji wa Ofisi yangu na kutafakari malengo yajayo katika Mkutano huu wa Tatu wa Bunge lako la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu kwa kuiteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, pia ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwa naibu wangu, Naibu Waziri Mheshimiwa Deogratius Ndejemi pamoja na watendaji wa Ofisi yangu ambao wameidhinisha na wanaendelea na nafasi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kipekee kuungana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan wewe mwenyewe pamoja na Bunge lako Tukufu kutoa pole kwa Watanzania wote na familia kwa kuondokewa na Rais wetu mpendwa Jemedari Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Awamu wa Tano. Naamini wote tulimpenda sana, lakini yote ni mapenzi ya Mungu, kilichobaki ni sisi kumuomba kwa

Mwenyezi Mungu na kuyaenzi yale yote mema aliyotuachia.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuapishwa kwake kuwa Rais wa Awamu ya Sita, vilevile ninampongeza kwa kuanza vizuri kuiongoza nchi yetu kwa kufanya uteuzi wa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, pamoja na Viongozi wa Taasisi. (*Makofi*)

Katika utekelezaji wa majukumu yake Rais ametoa maelekeo ambayo yameonesha dira na mwelekeo wa utekelezaji wenye maono mapana ya kuijenga nchi yetu ndani ya muda mfupi, ni matarajio yetu kuwa nchi yetu itaendelea kupata maendeleo makubwa tukizingatia kauli mbiu yake kazi iendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kauli hiyo maana yake ni kuwa maendeleo ya Tanzania yanaendelea kukua kwa kasi zaidi, tahadhari zake zinatuandaa tuepuke kuzinguana katika kutekeleza majukumu yake katika Serikali. Kwa niaba yangu binafsi, Ofisi yangu na kwa niaba ya wote wanaonisaidia kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ninaahdi kufanya kazi kwa bidii, uadilifu, weledi, uzalendo wa Kitaifa ili kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wote tumeshuhudia sana namna Mheshimiwa Rais alivyochukua hatua madhubuti ya kupambana na ubadhilifu uliojitokeza katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pia katika hotuba aliyoitoe wakati wa kuapishwa watendaji wa Serikali ambayo ilitoa mwelekeo wa kila Wizara, Taasisi namna ambavyo itatakiwa kufanya kazi ya kuwaletea Watanzania ustawi wa maendeleo endelevu kwa kasi kubwa. Aidha, Mheshimiwa Rais amesisitiza uwajibikaji, uchapakazi na uadilifu na utendaji wenye matokeo chanya kwa aliowateua ambao mwangwi wake umefika kwa watumishi wa umma.

Vilevile msisitizo wake kwenye utekelezaji wa miradi mikuu ya kimkakati kwa Taifa ni jambo ambalo tunatarajia yataokoa kama Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kwakwe, na kwa imani kubwa ya Bunge lako hili Tukufu, kwa kumthibitisha kwa asilimia 100. Pia Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeshuhudia akitoa maelekezo ya utendaji kazi ambayo yamedhihirisha kuwa tunakwenda kupata maendeleo endelevu ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi - Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake shupavu na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar na kuimarisha amani na utulivu. Vilevile ninampongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla - Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuteuliwa kuwahudumia wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa kuendelea na nafasi hiyo muhimu ambayo ni nguzo muhimu ya usimamizi na uratibu wa kazi za kila siku Serikalini na Bungeni. Umahiri, uzoefu ni chachu ya maendeleo kwa Taifa, utekelezaji wa shughuli katika Bunge hili la Kumi na Mbili ni matarajio ya kila mmoja wetu kwamba atatoa msaada mkubwa sana kwa Rais, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile ni matumaini ya kila mmoja wetu kwamba yeye atakuwa ni msaada mkubwa na kwako pia. *(Makofi)*

Naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuchaguliwa tena kwa nafasi zetu kuliongoza Bunge letu Tukufu, hiyo inaonesha kwamba Watanzania wana imani kubwa sana nanyi. Tunategemea kuwa mtaendelea kuwa

na umakini, busara na hekima kubwa kama mliyodhihirisha katika Bunge la Kumi na Moja, nawapongeza pia Wenyeviti wote wa Kamati kwa kuchaguliwa kwao na kuaminiwa katika kuongeza ustadi wa hali za juu za kazi waliyopewa ya kuliongoa Bunge lako hili Tukufu. Kwa hakika watakuwa ni msaada mkubwa sana katika uendeshaji wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwapongeza Mawaziri wenzangu wote na Naibu Mawaziri wa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuteuliwa kwao na kupata nafasi ya kuwatumikia Watanzania katika kutekeleza Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na Dira ya Taifa ya Maendeleo mwaka 2025. Kwa namna ya kipekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Humphrey Polepole - Mbunge na Makamu wake Mheshimiwa Abdallah Chaurembo - Mbunge wa Mbagala, kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri wa kupitia taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021na mapendekezo ya mpango huu utekelezaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na ushirikiano wa Kamati umetuwezesha kuboresha utendaji kazi wa ofisi yangu na maandalizi ya hotuba hii. *(Makofi)*

Ninamshukuru sana Naibu Waziri wangu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi ambaye amekuwa msaada mkubwa katika kuongoza ofisi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Balozi Hussein Katanga - Katibu Mkuu Kiongozi, Dkt. Moses Kusiluka - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Ikulu, Dkt. Laurean Ndumbo - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Francis Michael - Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi hii pamoja na Ofisi ya Ikulu -

Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha ofisi kufikia malengo yake ikiwa ni pamoja na kukamilisha hotuba hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru waajiri na watumishi wote hapa nchini (watumishi wa umma) kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo pamoja na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ambao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuzishukuru nchi wahisani na washirika wa maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Rufiji kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa wakati wote na kuendelea kuwawakilisha hapa Bungeni, vilevile naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipatia na kwa dua zao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu, viongozi na watumishi wa umma waliopotelewa na ndugu zao kutokana na sababu mbalimbali zinazojitokeza katika kila kipindi, tunamuomba Mwenyezi Mungu awape faraja wote ili waendelee kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba dunia kwa sasa imekumbwa na mlipuko wa pili wa ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Corona (UVICO 19) ugonjwa huu umesababisha vifo katika nchi mbalimbali. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa dhamira ya kuunda Tume ya Kitaalamu itakayosaidia kutoa mapendekezo namna bora ya kupambana na UVICO 19. Kwa sasa natoa rai kwa kila mtumishi wa umma kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 tuliwasilisha mbele ya Bunge lako maombi ya fedha kwaajili ya kutekeleza mipango kazi inayoweza Ofisi yangu kwa mazingatio ya kisera na kimkakati kwa mara nyingine tupo mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli tulizoomba fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Pamoja na kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango kwa mwaka wa fedha 2020/2021 utekelezaji na mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulizingatia mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano 2016/2017 na 2020/2021 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2015 pamoja Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Shughuli zilizotekelezwa na Taasisi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Ikulu na Taasisi zake; katika mwaka wa fedha 2020/2021 Fungu 20 Ofisi ya Rais - Ikulu iliidhinishiwa shilingi 24,493,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida hadi kufikia mwezi Machi mwezi 2021 shilingi 18,84,770,849.97 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri Fungu Namba 30 inajumuisha Taasisi zote zilizo chini ya Ikulu iliidhinishiwa shilingi 608,155,446,000 kati ya fedha hizo shilingi 439,935,875,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 168,219,571,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2021 shilingi 408,734,273,169 zilipokelewa na kutumika kati ya fedha hizo shilingi 278,861,618,923.99 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 129,872,654,245 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Yafuatayo ni maelekezo ya kila taasisi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - Ikulu imeendelea kuongoza kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi mwezi Machi, 2021 kazi zilizotekelezwa na ofisi hii ni Pamoja na hizi zifuatazo:-

Huduma zimetolewa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake, vilevile ushauri umetolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ratiba ya kila siku.

Pia ushauri ulitolewa katika masuala ya siasa, uchumi, jamii, sheria, diplomasia, mawasiliano ya habari, uhusiano wa kikanda kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi na pili mikutano minne ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka nane zilijadiliwa na kutolewa maamuzi. Pia mikutano miwili ya Kamati ya Katiba na Bunge la Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo Miswada 17 ilijadiliwa. Aidha, mikutano hiyo ilitanguliwa na mikutano ya wataalamu kwa ajili ya kuandaa ushauri vile vile ufuatiliaji na tathmini ya maamuzi ya Baraza la Mawaziri ulifanyika na taarifa ya utekelezaji wake iliandaliwa. Maelezo kamili utayakuta katika ukurasa wa 10 hadi 14 ya hotuba hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329. Juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukabiliana na vitendo vya rushwa nchini zimeleta mafanikio makubwa kwa kuongeza nidhamu, uadilifu na uwajibikaji na matumizi bora ya madaraka kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo za utumishi wa umma, biashara, uwekezaji, ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya *Transparency International* ya mwezi Februari, 2021 Tanzania imepata alama 38 na kushika nafasi 94 kati ya nchi 180 ikiwa ni kupanda katika nafasi mbili ikilinganishwa na alama 37 katika nafasi ya 96 mwaka 2019. Taasisi hii inaamini ilifuata falsafa ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Koffi Annan aliyewahi kusema *if corruption is a disease transparency is essential part of its treatment*, mafanikio yetu yanathibitisha kuimarika kwa ujenzi wa uwazi katika utendaji wa Serikali na hasa mifumo ya utoaji huduma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU imeanzisha ofisi inayotembea ambapo ofisi za Mikoa na Wilaya zinatenga siku moja kila mwezi kusikiliza na kutatua kero za wananchi. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa ilitekeleza shughuli zaidi ya 17 baadhi ya shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kesi 909 ziliendeshwa Mahakamani zikijumuisha kesi mpya 263 katika kipindi hiki kesi 294 ziliamuliwa mahakamani. Kati ya kesi hizo 195 watuhumiwa wake walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini.

Pili, kutokana na *operation* mbalimbali za uchunguzi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo unaofanyika kote nchini shilingi bilioni 27.58 zimeokolewa na shilingi bilioni 11.3 ni fedha taslimu zilizorejeshwa Serikalini na shilingi bilioni 16.55 zilidhibitiwa na kurejeshwa kwa wananchi, pia TAKUKURU ilitaifisha na kurejeshwa Serikalini au kwa wananchi waliodhulumiwa fedha na mali zenye thamani ya shilingi bilioni 44.6. Maelezo kamili yanapatikana katika ukurasa wa 14 – 26 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uongozi imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa kitivo au kituo cha utaalam wa hali ya juu cha kuendesha viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni viongozi waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali, Sekta binafsi, Asasi za Kiraia Pamoja na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi mwezi Machi 2021 Taasisi ya Uongozi imetekeleza kazi 11 tukizitaja kwa uchache, ya kwanza ni Wabunge 388 wa Bunge lako la Kumi na Mbili la Jamhuri la Muungano wa Tanzania wamepata mafunzo ya masuala ya uongozi ikiwemo uongozi binafsi na jinsi ya kutafuta rasilimali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viongozi wa Umma 376 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 12 kwa



lengo la kuimarisha utendaji na kupanua uelewa katika masuala ya kiuongozi. Maelezo kamili ya eneo hili yanapatikana katika ukurasa wa 21 mpaka ukurasa wa 26.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania - MKURABITA; Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania yaani MKURABITA umeendelea kutekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo ya Kitaifa wa umiliki rasilimali na uendeshaji wa biashara hapa nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi mwezi Machi, 2021 MKURABITA imetekeleza kazi kubwa saba ikiwemo huduma za urasimishaji wa biashara zilisogezwa karibu na wananchi kwa kuanzisha vituo vya huduma kwa Pamoja katika Halmashauri ya Jiji la Arusha na Manispaa ya Musoma ambapo huduma muhimu za kuwezesha uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo *SIDO* zinapatikana sehemu moja. Maelezo kamili ya eneo hili yanapatikana ukurasa wa 26 hadi 29.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – *TASAF* umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya *TASAF* ya kuwapa kipaumbele maeneo ya ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii na utawala bora na uwajibikaji. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – *TASAF* umetekeleza kazi 10. Kazi ya kwanza ilikuwa ni ruzuku ya Serikali ya shilingi bilioni 135 ili ilihawilishwa kwa kaya maskini 883,194 kwa walengwa katika Halmashauri 184 zote za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar baada ya uhakiki kufanyika na kukamilika. Maelezo kamili ya eneo hili yanapatikana katika ukurasa 29 hadi 32 ya hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ndege za Serikali Ofisi yangu ndiyo inayosimamia Wakala wa Ndege za Serikali ambayo ina jukumu la kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Wakala wa Ndege za Serikali

ilitekeleza kazi sita nikizitaja kazi mbili muhimu ilikuwa ni huduma za usafiri wa anga zilitolewa kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambapo jumla ya safari 104 za ndani na tatu za nje ya nchi zilifanyika. Wakala pia imeendelea kusimamia mikataba nane ya ukodishwaji wa ndege za Serikali kwa Kampuni ya Ndege ya ATCL. Maelezo kamili ya eneo hili yanapatikana katika ukurasa wa 32 hadi 33 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa jumla ya shilingi 9,471,110,000 kati ya fedha hizo shilingi 7,621,110,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1,850,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2021 shilingi 5,365,126,200 ni matumizi ya kawaida zilizopokelewa na kutumika kwa upande wa miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 Sekretarieti ya Maadili na Viongozi wa Umma ilitekeleza shughuli tisa ikiwemo moja muhimu ni jumla ya viongozi 14,981 ambao ni sawa na 99% kati ya viongozi 15,110 wamarejeshwa fomu zao za Tamko Rasilimali na Madeni katika kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba. Jumla ya viongozi 129 sawa na 1% ya viongozi wote bado hawajarejeshwa Tamko hilo. Maelezo kamili katika eneo hili yanapatikana katika ukurasa wa 33 hadi 37 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wakala zake; katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma Fungu 32 inayojumlisha Mamlaka ya Wakala iliyo chini yake iliidhinishwa jumla ya shilingi 43,878,828,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa mwaka kati ya fedha hizo shilingi 32,923,578,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 10,955,250,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufika mwezi Machi, 2021 jumla ya shilingi 30,350,465,668.19 zilikuwa zimepokelewa na

kutumika kati ya fedha hizo shilingi 21,949,423,716.38 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 8,401,041,951.81 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake ilitekeleza jumla ya shughuli 53 baadhi ya shughuli hizo ni pamoja na Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma (*Standing Orders*) zimewekwa katika mfumo wa sauti ili kuwawezesha watumishi wa umma wenye ulemavu wa kuona waweze kuzielewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vibali vya ajira mpya na mbadala nafasi 11,064 kwa kada mbalimbali vimetolewa, watumishi wa umma 23,971 wa kada mbalimbali waliopandishwa vyeo waliidhinishwa kwenye mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara, madai ya malimbikizo ya mishahara watumishi wa umma yalipokelewa na Wizara ya Fedha na Mipango baada ya kuhakikiwa na kuidhinishwa na Ofisi yangu jumla ya watumishi 37,388 yenye thamani ya shilingi 69,041,217,747.35 na madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 17,699 yenye thamani ya shilingi 37,474,809,031.55 yanaendelea kufanyiwa kazi kuhakikiwa. Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango tutahakikisha kwamba madai yote hayo yanalipwa katika mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawaagiza waajiri wote hasa Maafisa Utumishi wafanye kuwasilisha madai ya utumishi kwa wakati ili kupunguza mlundikano wa madeni. Ofisi imepokea na kushughulikia mapendekezo ya nafasi ya uteuzi, mikataba ya ajira na vibali vya kukaimu nafasi za uongozi ili kuwezesha waajiri kujaza nafasi za uongozi kwenye taasisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mfumo wa *HCMIS* umekamilika na kuanza kutumika kuingiza bajeti ya mishahara ya mwaka 2021/2022; malalamiko ya watumishi kuhusu haki zao na ya wananchi yaliyohusu ukiukwaji wa maadili katika utumishi wa umma yalipokelewa na

kushughulikiwa. Kwa maelezo kamili yanapatikana ukurasa wa 38 hadi 53.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma; maelezo kamili kuhusu Chuo chetu cha Utumishi wa Umma yanapatikana katika ukurasa wa 53 hadi 56 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), mamlaka hii ilianzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Namba 10 ya mwaka 2019. Mamlaka ilianzishwa ili kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa taasisi zake. Maelezo kamili yanapatikana katika ukurasa 56 hadi 61.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - Sekretarieti ya Ajira na Utumishi wa Umma nimeyaeleza na kuyafafanua katika ukurasa wa 61 hadi 65. Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma yamefafanuliwa katika ukurasa wa 66 hadi 67 kama ambavyo nimesema. Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma nimeyafafanua kwa kina kabisa katika ukurasa wa 68 hadi 69; Ofisi ya Rais Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa maelezo kamili nimeyafafanua katika ukurasa wa 70 hadi 74.

Mheshimiwa Spika, mpango wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022; mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2020 hotuba ya Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliyoitoa katika Bunge la Kumi na Mbili pamoja na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 unaoitaka Tanzania iwe na uchumi shindani katika maendeleo ya viwanda kwa maendeleo ya watu shughuli zinazotekelezwa katika taasisi hizi nimezifafanua kwa kina kabisa katika kurasa za 75 na 78.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namna itakavyotekeleza kazi zake nimezifafanua kwa kina katika kurasa 78 hadi 80.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uongozi; Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema nanukuu; "*Inasemekana kuwa viongozi wanazaliwa na hawatengenezwi*" lakini usemi huu ni kweli nusu yaani ni wenye mashaka hakuna mtu anayeishi ambaye sifa zake za uongozi haziwezi kuboreshwa na kuendelezwa kwa mafunzo kwa kuheshimu busara hiyo ya Mwalimu Nyerere nimeifafanua katika ukurasa 80 hadi 82.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara (MKURABITA) nimezifafanua pia katika ukurasa wa 82 hadi 85.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais ndiyo inayohusika na uwezeshaji wa maamuzi juu ya nchi sambamba na Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambao ni nguzo muhimu katika uendeshaji na uendelezaji wa nchi. Utumishi wa umma umeendelea kutoa mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi ambao sasa imefikia uchumi wa kipato cha kati. Tuna matarajio makubwa kuwa mchango wa watumishi wa umma utaendelea kuwezesha nchi kufikia uchumi wa kati wa kiwango cha juu. Aidha, maendeleo hayo yanatarajiwa kuongezeka kwa kuimarisha uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu kama inavyoshajirishwa katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais itaendelea kuimarisha uwezeshaji wa vyombo vinavyosaidia kwenye maamuzi ya nchi, usalama na kuimarisha vita dhidi ya rushwa. Maadili kwa viongozi wote na watumishi wa umma yanatarajiwa kusimamiwa ipasavyo ili yachangie kwenye kuongeza tija ya rasilimaliwatu na rasilimali fedha ili kupata thamani ya fedha ya rasilimali hizo, kwa maendeleo ya watu. Kati ya mambo ambayo Serikali itayapa kipaumbele ni usimamizi thabiti wa maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa ujumla inafanya maboresho ya kisekta na ya maeneo mbalimbali yaliyo mtambuka. Ofisi ya Rais ndio mratibu wa jumla wa maboresho yote katika Serikali. Hivyo, wajibu huo utatekelezwa kwa kuhakikisha kuwa maboresho yanayofanyika katika nchi yetu bila kuleta urudufu na yanaleta tija katika Utumishi wa Umma na kuchochea maendeleo. Aidha, Ofisi yangu itahakikisha kunakuwepo na utawala bora ulio imara kuanzia ngazi ya juu ya uongozi hadi chini. Katika kuimarisha uwazi Ofisi ya Rais itahakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu maamuzi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nchi yetu na kwa mujibu wa miundo na mgawanyo wa majukumu kwa Mawaziri, utekelezaji kwa ujumla unajumuisha, mafungu yote ya Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, mipango wa bajeti kwa mafungu niliyoyataja hapo awali bila kujumuisha Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa yamezingatia vipaumbele vya Serikali kwenye eneo la kuimarisha utendaji kazi wa utumishi wa umma na unaotoa bora haraka na stahiki kwa kuzingatia Katiba, sera, sheria kanuni pamoja na miongozo na taratibu ili kuondoa matumizi mabaya ya rasilimali fedha. Ukiukwaji wa madili ya uongozi na kujenga imani zaidi kwa wananchi na kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kuendana na wakati jitihada zaidi zitawekwa kwenye kujenga uwezo wa mifumo kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama na fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa kutumia TEHAMA ndani ya Serikali pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara Tanzania ili kuendana na kauli mbiu ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza awali tutaimarisha mfumo wa uwezo kwa matumizi ya mfumo wa kushughulikia malalamiko ya watumishi kuhusu mambo

mbalimbali ikiwemo haki zao na wananchi kuhusu huduma za watumishi wa umma kwenye ngazi zote ili kupunguza kwa kiwango kikubwa kero hizo. Aidha, natoa rai kwa Maafisa Utumishi wote kushughulikia changamoto zote za utumishi haraka. Narudia kusisitiza tukitembelea kwa mwajiri yoyote ikiwa ni mimi au wasaidizi wangu na tukakuta kwamba kuna malalamiko yanaweza kutatuliwa na mwajiri tutachukuwa hatua kali. Ikiwemo kuwavua madaraka wale wote waliozembea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninawaomba Wabunge kuleta kero na malalamiko yenu kuhusu watumishi wa umma katika majimbo yenu moja kwa moja kwangu, wakati wowote, nimedhamiria kupunguza kama siyo kumaliza kabisa malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi yanayohusu Ofisi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yetu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Mipango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2021/2022 sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi yetu kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote jumla kuu ya bajeti ninayoiomba kwa mafungu yate yaliyo chini ya Ofisi Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2021/2022, ni kama ifuatavyo:-

Jumla kuu matumizi ya kawaida ni shilingi 544,574,460,000; jumla kuu ya matumizi ya miradi ya maendeleo ni shilingi 183,358,401,000 na jumla kuu kwa mafungu yote ni 727,932,861,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili kwa kina na kuyaidhinisha. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja iliitolewa lamuliwe*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI  
YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA,  
MHESHIMIWAMOHAMED O. MCHENGERWA (MB) YA  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA  
MWAKA 2021/22 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**,naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30); Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09); na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04); Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

**2. Mheshimiwa Spika**, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujaalia amani na utulivu ambavyo vimetuwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuwahudumia wananchi pamoja na kutuwezesha kukutana kwa ajili ya kupokea utekelezaji wa Ofisi yangu na kutafakari malengo yajayo katika mkutano huu wa tatu wa Bunge la 12. Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mheshimiwa



Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu kwa kunitewa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Pia, namshukuru Rais kwa imani yake kwa Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Deogratius Ndejemi pamoja na Watendaji wa Ofisi yangu ambao amewaidhinisha na wameendelea na nafasi zao.

**3. Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii ya kipekee kuungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika pamoja na Bunge lako Tukufu kutoa pole kwa Watanzania wote na familia kwa kuondokewa na Rais wetu mpendwa na Jemedari Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano. Naamini sote tulimpenda sana lakini yote ni mapenzi ya Mungu, kilichobaki ni sisi kumuomba kwa Mungu na kuyaenzi yale yote mema aliyotuachia.

**4. Mheshimiwa Spika**, napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuapishwa kwake kuwa Rais wa Awamu ya Sita. Vile vile nampongeza kwa kuanza vizuri kuiongoza nchi yetu kwa kufanya uteuzi wa Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na viongozi wa Taasisi. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Rais ametoa maelekezo ambayo yameonesha dira na mwelekeo wa utekelezaji wenye maono mapana ya kuijenga nchi ndani ya muda mfupi. Ni matarajio yetu kuwa nchi yetu itaendelea kupata maendeleo makubwa tukizingatia kauli mbiu yake ya **“Kazi iendeleo”**. Kwa kauli hiyo, maana yake ni kuwa maendeleo ya Tanzania yaendeleo kukua kwa kasi zaidi. Tahadhari zake zinatuuandaa **tuepuke kuzingwana** katika kutekeleza majukumu ya Serikali. Kwa niaba yangu binafsi, Ofisi yangu na kwa niaba ya wote ninaosaidiana nao kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ninaahidi kufanya kazi kwa bidii, uadilifu, weledi na uzalendo wa kitaifa ili kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**5. Mheshimiwa Spika**, Sote tumeshuhudia namna Mheshimiwa Rais alivyochukua hatua madhubuti kupambana na ubadhirifu uliojitokeza katika taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pia katika hotuba aliyotoa wakati wa kuapisha watendaji wa Serikali ambayo ilitoa mwelekeo kwa kila Wizara na Taasisi namna ambavyo itatakiwa kufanya kazi ya kuwaletea watanzania ustawi na maendeleo endelevu kwa kasi kubwa. Aidha, Mheshimiwa Rais amesisitiza uwajibikaji, uchapakazi, uadilifu na utendaji wenye matokeo chanya kwa alioateua ambao mwangwi wake umefika kwa Watumishi wa Umma. Vile vile, msisitizo wake kwenye utekelezaji wa miradi mikuu ya kimkakati kwa Taifa ni jambo ambalo tunatarajia litatutoa kama Taifa.

**6. Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuteuliwa kwake, na kwa imani kubwa ambayo Bunge lako limethibitisha jina lake kwa asilimia 100. Pia, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumeshuhudia akitoa maelekezo ya utendaji kazi ambayo yamedhihirisha kuwa tunakwenda kupata maendeleo endelevu ya kiuchumi.

**7. Mheshimiwa Spika**, Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake shupavu na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar na kuimarisha amani na utulivu. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuteuliwa kuwahudumia wananchi wa Zanzibar.

**8. Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuaminiwa kuendelea na nafasi hiyo muhimu ambayo ni nguzo muhimu ya usimamizi na uratibu wa kazi za kila siku za Serikali na Bungeni. Umahiri nauzoefu wake ni chachu ya maendeleo kwa Taifa na utekelezaji wa shughuli za Bunge hili la 12. Ni

matarajio ya kila mmoja wetu kwamba atatoa msaada mkubwa sana kwa Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, ni matumaini ya kila mmoja wetu kwamba yeye ni msaada mkubwa na kwako pia wewe Mheshimiwa Spika.

**9. Mheshimiwa Spika**, naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika, kwa kuchaguliwa tena katika nafasi zenu za kuliongoza Bunge letu Tukufu, hiyo inaonesha kwamba Watanzania wana imani kubwa kwenu. Tunategemea kuwa mtaendelea na umakini, busara na hekima kubwa kama mlivyodhihirisha katika Bunge la 11. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kuchaguliwa kwao na kuamini kuwa watatenda kwa ustadi wa hali ya juu kazi waliyopewa ya kuliongoza Bunge letu, kwa hakika watakuwa msaada mkubwa sana katika uendeshaji wa Bunge kwa ujumla.

**10. Mheshimiwa Spika**, Naomba pia kuwapongeza Mawaziri wenzangu wote na Manaibu Waziri wa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuteuliwa kwao na kupata nafasi ya kuwatumikia Watanzania katika kutekeleza Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

**11. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Humphrey Polepole (Mbunge) na Makamu wake Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mbunge wa Mbagala kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri waliutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/21 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/22. Maoni, ushauri na ushirikiano wa Kamati umetuwezesha kuboresha utendaji kazi wa Ofisi yangu na maandalizi ya hotuba hii.

**12. Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Balozi Hussein A. Kattanga, Katibu Mkuu Kiongozi; Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Dkt. Laurean J. Ndumbaro, Katibu

Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Dkt Francis Michael, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Aidha, napenda kuwashukuru waajiri na watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo pamoja na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ambao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

**13. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni:- Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, India, Jamhuri ya Korea, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Italia, Malaysia, Misri, Singapore, Cuba, Thailand na Ireland. Vile vile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), OFID-OPEC Fund for International Development, DfID, KOICA, GIZ, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, DANIDA, JICA, UNICEF, ILO, WFP, UN Women, Global Fund, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation.

**14. Mheshimiwa Spika**, natumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Rufiji kwa kuendelea kunipa ushirikiano wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha. Vile vile, naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa na kwa dua zao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu.

**15. Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa natoa pole pole kwa Watanzania wenzetu, Viongozi na Watumishi wa Umma waliopotelewa na ndugu zao kutokana na sababu mbalimbali zilizojitokeza katika kipindi hiki. Tunamuomba

Mwenyezi Mungu awape faraja wote ili waendeleo kujenga Taifa letu.

**16. Mheshimiwa Spika**, tunatambua kwamba Dunia kwa sasa imekumbwa na mlipuko wa pili wa ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Korona - UVIKO 19. Ugonjwa huu umesababisha vifo katika nchi mbali mbali. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa dhamira ya kuunda Tume ya kitaalamu itakayosaidia kutoa mapendekezo ya namna bora ya kupambana na UVIKO 19. Kwa sasa natoa rai kwa watumishi wa umma kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu.

**17. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21 tuliwasilisha mbele ya Bunge maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango kazi inayowezesha Ofisi yangu kwa mazingatio ya kisera na kimkakati. Kwa mara nyingine tupo mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli tulizoombea fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 pamoja na kuwasilisha mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

## **MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

**18. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 ulizingatia, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2015 pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Shughuli zilizotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:-

### **OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE**

**19. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu: 20 Ofisi ya Rais, Ikulu ilidhinishiwa **Shilingi 24,049,003,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2021 **Shilingi 18,084,770,849.97** zilipokelewa na kutumika.

**20. Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya

Baraza la Mawaziri (Fungu 30) inayojumuisha taasisi zilizo chini ya Ikulu, iliidhinishiwa **Shilingi 608,155,446,000** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 439,935,875,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 168,219,571,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2021 **Shilingi 408,734,273,169.02** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 278,861,618,923.99** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 129,872,654,245.03** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Yafuatayo ni maelezo kwa kila taasisi:-

#### **A: OFISI YA RAIS - IKULU**

**21. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Machi, 2021, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Huduma zimeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

(ii) Ushauri umeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ratiba ya kila siku;

(iii) Ushauri umeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi.

(iv) Mikutano 13 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika, ambapo nyaraka 26 zilichambuliwa. Mikutano 8 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika na nyaraka 17 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Mikutano 8 ya kazi ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu ilifanyika ambapo mada 19 ziliwasilishwa na kujadiliwa. Mikutano 4 ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 8 zilijadiliwa na kutolewa maamuzi. Aidha, mikutano 2 ya Kamati ya Katiba na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo miswada 17 ilijadiliwa;

(v) Kumbukumbu za Mikutano ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri ziliandaliwa na kusambazwa kwa wakati kwa wahusika. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya Maamuzi ya Baraza la Mawaziri ulifanyika na taarifa ya utekelezaji wake iliandaliwa;

(vi) Ziara ya Maafisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kutembelea Kampuni ya Ranchi za Taifa katika Ranchi ya Kongwa ilifanyika ili kuona hali halisi ya utendaji na kushauri ipasavyo;

(vii) Mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara yalifanyika;

(viii) Mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri kwa Menejimenti za Wizara nne za Maji; Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi); Habari Utamaduni na Michezo; na Mifugo na uvuvi yalifanyika;

(ix) Kongamano la Wadau wa Sera Serikalini lililowashirikisha Wakurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara, Wakurugenzi Wasaidizi wa Sehemu ya Sera Wizarani, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Maofisa kutoka Taasisi ya Uongozi lilifanyika Morogoro mwezi Februari, 2021;

(x) Vitabu vya Taarifa za Utekelezaji wa Kazi na Shughuli za Baraza la Mawaziri na Kamati zake kwa kipindi cha mwaka 2005 – 2010 na 2010 – 2020 viliandaliwa;

(xi) Uratibu wa utekelezaji wa Programu ya Kujenga Uwezo wa Taasisi nufaika 9 simamizi za utawala bora za Serikali za Kupambana na Rushwa (BSAAT) nchini ulifanyika;

(xii) Mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (NACSAP III) kwa Kamati za Kudhibiti Uadilifu 90 za Taasisi za Umma na kwa AZAKI 700 katika wiki ya Asasi za Kiraia Jijini Dodoma yalifanyika;

(xiii) Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Programu ya Maboresho (Blue Print) kwa Taasisi ya BRELLA, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Kituo cha Uwekezaji (TIC) -Dar es salaam umefanyika;

(xiv) Rufaa 170 za Watumishi wa Umma, Mamlaka ya Nidhamu na Waajiri zilichambuliwa na kutolewa uamuzi na Rais na Katibu Mkuu Kiongozi ambapo wahusika walijulishwa. Aidha, malalamiko 462 ya Watumishi wa Umma na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo;

(xv) Majibu na ushahidi kwenye kesi za madai tisa zinazohusu watumishi wa Umma na wananchi wengine zilizoko Mahakama Kuu zinazopinga uamuzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Katibu Mkuu Kiongozi yalitolewa kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;

(xvi) Kikao cha Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu wanaosimamia Utekelezaji wa Programu za Maboresho katika Sekta ya Umma na mikutano miwili ya Waratibu wa Programu ya maboresho imefanyika hizo umefanyika ili kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki mchakato wa maboresho katika sekta ya umma nchini; na

(xvii) Ujenzi na ukarabati wa majengo katika Ikulu ya Chamwino unaendelea. Aidha, ukarabati wabaadhi ya majengo katika Ikulu ya Dar es salaam na Ikulu Ndogo ya Lushoto umefanyika.

## **B. TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)**

**22. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329. Majukumu hayo ni kuchukua hatua stahiki za kuzuia na kupambana na rushwa kwenye sekta ya umma, mashirika na sekta binafsi.

**23. Mheshimiwa Spika**, Juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukabiliana na



vitendo vya rushwa nchini zimeleta mafanikio makubwa kwa kuongeza nidhamu, uadilifu na uwajibikaji na matumizi bora ya madaraka kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo za utumishi wa umma, biashara, uwekezaji, ukusanyaji mapato na matumizi ya fedha za umma. Mafanikio haya yamejengea Serikali uwezo imara wa kukuza uchumi na kuongeza kasi ya utoaji huduma bora kwa umma.

**24. Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya tafiti zilizofanywa na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kupambana na rushwa zimedhihirisha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika kudhibiti vitendo vya rushwa na ufidiaji nchini. Miongoni wa Taasisi hizo ni REPOA, TWAWEZA, Mo Ibrahim, Afrobarometer na Transparency International. Katika taarifa ya Transparency International ya mwezi Februari, 2021 Tanzania imepata alama 38 na kushika nafasi ya 94 kati ya nchi 180; ikiwa ni kupanda kwa nafasi mbili ikilinganishwa na alama 37 katika nafasi ya 96 ya mwaka 2019.

**25. Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza Ibara ya 116 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 na maagizo ya Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyotoa wakati wa kufungua Bunge la 12 tarehe 13 Novemba, 2020 Dodoma; TAKUKURU imeanzisha Ofisi inayotembea ambapo ofisi za mikoa na wilaya zinatenga siku moja kila mwezi kusikiliza na kutatua kero za wananchi lakini pia imeandaa mpango kazi wa miaka 5 wa utekelezaji wa majukumu yake na kusambazwa katika idara na vitengo vyake na kwamba mpango kazi husika umewasilisha ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya kufuatilia matokeo ya utekelezaji wa mpango kazi husika.

**26. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Uchunguzi wa majalada 561 ulikamilika na majalada 119 kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kuombewa kibali

ambapo Majalada 107 yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Aidha, majalada mengine yanaendelea kufanyiwa kazi;

(ii) Kesi 993 ziliendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya 312. Katika kipindi hiki, kesi 338 ziliamuliwa mahakamani ambapo kesi 122 watuhumiwa wake waliachiwa huru na kesi 216 watuhumiwa wake walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini. Kesi 655 zinaendelea mahakamani;

(iii) Shilingi bilioni 28.65 zimeokolewa kutokana na operesheni mbalimbali za uchunguzi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo unaofanyika kote nchini ambapo Shilingi bilioni 11.28 ni fedha taslimu zilizorejeshwa Serikalini na Shilingi bilioni 17.37 zilidhibitiwa au kurejeshwa kwa wananchi. Pia, Taasisi ilitaifisha na kurejeshwa serikalini au kwa wananchi waliodhumiwa fedha na mali zenye thamani ya Shilingi bilioni 44.6 ikihusisha fedha taslimu, nyumba 12, mashamba mawili (2), viwanja 77, magari 13, Trekta mbili (2) na pikipiki nne (4) zilizotokana na operesheni maalum za kufuatilia madeni sugu ya Shirika la maendeleo la Taifa (NDC) kwa waliokopeshwa matrekta, madeni ya Mfuko wa Pembejeo (AGIFT), ubadhirifu wa shilingi bilioni 28 zilizotolewa kama mkopo na Serikali ya Libya kwa ajili ya kujenga kiwanda cha Saruji mkoani Lindi, Ubadhirifu wa mali na uchepushaji wa vifaa ghafi vya umeme uliofanyika TANESCO katika Mradi za REA II na ufuatiliaji wa madeni ya PSSSF yaliyokopeshwa kwa Vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOS);

(iv) Utafiti wenye lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mianya ya rushwa umefanyika katika maeneo ya programu za uelimishaji umma zinazotekelezwa na TAKUKURU na maadili ya Asasi za Kiraia (AZAKI). Matokeo na mapendekezo ya kuziba mianya ya rushwa katika maeneo haya yamewasilishwa kwa mamlaka husika ili hatua stahiki zichukuliwe;

(v) Kazi 469 za uchambuzi wa mifumo zilifanyika katika maeneo mbalimbali yakiwemo kodi ya huduma, uchaguzi mkuu na utoaji wa vibali vya ujenzi ambapo kutokana na

kazi hizo, hatua zimechukuliwa ikiwemo kutoa elimu kwa umma na kushauri mamlaka husika namna ya kudhibiti mianya ya rushwa katika maeneo husika;

(vi) Ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (PETS) katika Miradi ya maendeleo nchini umefanyika ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha inapatikana. Miradi 742 ya maendeleo yenye thamani ya Shilingi bilioni 1,065 katika sekta za kipaumbele za Afya, Maji, Fedha na Mamlaka za Serikali za Mitaa ilifuatiliwa. Kati ya miradi hiyo, miradi 267 yenye thamani ya Shilingi bilioni 280.3 ilionekana kuwa na kasoro mbalimbali na inaendelea kufanyiwa uchunguzi;

(vii) Utafiti wa Kitaifa wa hali ya Utawala na Rushwa (National Governance and Corruption Survey) umekamilika. Utafiti huu ulikusanya taarifa kuhusu kiwango cha rushwa, aina za rushwa na tabia/mbinu mpya za vitendo vya rushwa kwa lengo la kuisaidia Serikali kuweka msingi wa kisayansi kukabiliana na tatizo la rushwa nchini;

(viii) Warsha/vikao 202 vya Wadau matokeo ya kazi za utafiti, PETS na uchambuzi wa mifumo kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa vilifanyika;

(ix) Kazi 77 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio yatokanayo na mapendekezo ya utafiti, PETS na uchambuzi wa mifumo zilifanyika ili kuziba mianya ya rushwa katika maeneo mbalimbali yakiwemo vitalu nyumba, miradi ya maji na rushwa ya ngono katika taasisi za elimu ya juu na miradi ya usambazaji wa umeme vijijini;

(x) Elimu kuhusu athari za rushwa na juhudi za Serikali za kuidhibiti ili kupata uungwaji mkono ilitolewa kwa umma kupitia njia mbalimbali zikiwemo semina 2,856, mikutano ya hadhara/mijadala 3,275, vipindi vya redio na televisheni 314, maonesho 271 na taarifa kwa umma 143 zilitolewa kupitia vyombo vya habari. Aidha, habari/makala 557 ziliandaliwa kwa ajili ya wavuti na jarida la TAKUKURU na matangazo tisa yaliandaliwa kwa ajili ya kuelimisha umma;

(xi) Elimu kuhusu rushwa ilitolewa kwa vijana walio shuleni na vyuoni ambapo Klabu za wapinga rushwa 1,595 zimefunguliwa na 5,617 kuimarishwa ili kujenga kizazi cha vijana wenye maadili na wanaochukia rushwa;

(xii) TAKUKURU imepokea malalamiko na taarifa kutoka kwa wananchi saa 24 kwa siku ambapo wananchi 86,221 wameweza kuifikia TAKUKURU kwa simu namba 113 ambapo walipata fursa ya kutoa maoni, ushauri, kuuliza maswali na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa;

(xiii) Kampeni ya “Vunja Ukimya” inayolenga kudhibiti rushwa ya ngono iliendeshwa katika mikoa yote. Lengo kubwa likiwa ni kuwahamasisha wanaokumbana na vitendo hivyo na wananchi kwa ujumla kutoa taarifa TAKUKURU ili hatua dhidi ya wahusika zichukuliwe;

(xiv) Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Taasisi kwa mwaka 2019/20 iliwasilishwa kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 14 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura 329 kinachoitaka TAKUKURU kuwasilisha taarifa ya utendaji kazi ya mwaka uliopita kwa Rais kabla ya tarehe 31 Machi, ya kila mwaka;

(xv) Elimu kwa umma imetolewa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kubeba agenda ya mapambano dhidi ya rushwa ambapo jumla ya matangazo 47 yaliandaliwa na kusambazwa kwa njia ya “Whatsup”, taarifa mbalimbali zimeendelea kutolewa kwenye mitandao ya “Twitter”, “WhatsApp” na “Instagram”. Aidha, uzinduzi wa TAKUKURU Online TV umefanyika ili kuwashirikisha wananchi wengi kwa gharama nafuu;

(xvi) Mfumo wa TEHAMA ndani ya TAKUKURU umeimarishwa kwa kuunganisha Ofisi za Wilaya 66 kwenye mtandao wa Taasisi na kuboresha njia za mawasiliano katika Mikoa 28 kwa lengo la kurahisisha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za Wilaya, Mikoa na Makao Makuu; na

(xvii) Watumishi 366 walipatiwa mafunzo ya ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo wa kumudu majukumu kwa ufanisi.

### C. TAASISI YA UONGOZI

**27. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya UONGOZI imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa Kituo cha Utaalam wa Hali ya Juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Mahakama.

**28. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Taasisi ya UONGOZI imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Programu ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi iliendelea kutekelezwa. Stashahada hii inalenga kuwajengea viongozi uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine na kujenga sifa binafsi za kiongozi. Stashahada hii yenye moduli 10 inatekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto kilichopo Helsinki, nchini Finland. Katika kipindi hiki, awamu ya nne ya mafunzo inayojumuisha Maafisa Waandamizi 32 kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma iliendelea kutekelezwa;

(ii) Programu ya Uongozi ngazi ya Chetikwa njia ya mtandao ilizinduliwa rasmi tarehe 31 Agosti, 2020. Astashahada hii yenye moduli 3 inatekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto kilichopo Helsinki, nchini Finland kwa muda wa miezi sita. Katika kipindi hiki, awamu ya kwanza ya mafunzo inayojumuisha Maafisa Waandamizi 46 kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma, Taasisi za Kiraia na Taasisi Binafsi kutekelezwa. Awamu hii ya kwanza ilimalizika mwezi wa Februari ambapo Maafisa wote 46 walihitimu mafunzo;

(iii) Viongozi wa Umma 376 wamepata mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 12 kwa lengo la kuimarisha utendaji na

kupanua uelewa katika masuala ya kiuongozi. Kozi zilizotolewa zilihusu maeneo ya Uongozi; Uongozi Binafsi na Akili Hisia, Usimamizi wa Mashirika, Usimamizi wa Rasilimali za Umma, Usimamizi wa Viashiria Hatarishi na Udhhibiti wa Ndani na Mbinu za Uchambuzi wa Taarifa;

(iv) Wabunge 388 wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamepata mafunzo ya Masuala ya Uongozi ikiwemo Uongozi Binafsi na jinsi ya kutafuta rasilimali;

(v) Kwa kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi, makongamano manne (4) ya Kitaifa yalifanyika kwa lengo la kukutanisha viongozi ili kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu ambapo jumla ya viongozi 128 walishiriki. Makongamano yafuatayo yalifanyika:-

(a) Kongamano la Kitaifa la Wadau wa sheria kuhusu “Majadiliano ya Rasimu ya Mpango wa Pili wa Maboresho ya Sekta ya Sheria”, lilifanyika tarehe 20 Agosti, 2020. Kongamano liliandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria. Kongamano hili lilihudhuriwa na viongozi 60 kutoka Wizara na Idara za Serikali, Asasi za kiraia, na Sekta Binafsi;

(b) Kongamano la Kitaifa la Watunga Sera kuhusu “Namna Bora ya Kuandaa na Kuchambua Sera za Umma Nchini” lilifanyika kwa kushirikiana na Sekretariati ya Baraza la Mawaziri tarehe 30 Januari, 2021. Kongamano hili lilihudhuriwa na Viongozi 68 kutoka Wizara mbalimbali;

(c) Kongamano la Kitaifa la Wadau wa Masuala ya Mazingira kuhusu “ Majadiliano ya Rasimu ya Mkakati wa Kitaifa wa mabadiliko ya Tabia ya Nchi 2021 - 2026” lilifanyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira tarehe 3 Machi,2021. Kongamano hili lilitoa fursa kwa wadau kupitia na kupitisha Mkakati huu, ambapo wadau 73 walishiriki;

(d) Kongamano la Kitaifa la Wadau kujadili “Rasimu ya Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo 2021/22 - 2025/26” liliandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya fedha na

Mipango. Kongamano hili lilifanyika kuanzia Tarehe 22 mpaka 26 Machi, 2021 ambapo wadau zaidi ya 1,000 walishiriki.

(vi) Vipindi vitatu vya mahojiano na viongozi waandamizi na wataalam wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu viliandaliwa na kurushwa kwenye runinga na kuwekwa kwenye tovuti ya Taasisi ya UONGOZI na mitandao ya kijamii kwa lengo la kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu. Vipindi hivi vinaonekana Bara zima la Afrika;

(vii) Tafiti 20 kwenye maeneo ya uchumi wa Viwanda, Uchumi Mpana, Fedha, Usimamizi wa Mikopo endelevu, Mazingira Wezeshi ya Kibiashara na Rasilimali Asilia zimefanyika na kukamilika kwa kushirikiana na Taasisi ya Umoja wa Mataifa; UNU-WIDER, iliyoko Finland;

(viii) Tathmini 3 zilifanyika kutathmini “Athari za Kimazingira na Kijamii, zitokanazo na ujenzi wa Njia ya Umeme”, “Mpango wa Utekelezaji wa Wananchi Waliiothirika kwa kupoteza makazi, mali na kutwaliwa kwa ardhi kwenye Mradi wa Reli ya Kisasa” na “Athari kwa Wananchi Waliobomolewa kwa Kuvamia na Kujenga Kwenye Maeneo ya Shirika la Reli”, waliobomolewa ili kupisha ujenzi wa Reli ya kisasa. Tathimini hizi zilifanyika kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na wataalamu kutoka Wizara mbalimbali;

(ix) Kitabu kinachoelezea maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi kilichapishwa. Uzinduzi wa Kitabu hiki unatarajiwa kufanyika robo ya mwisho wa mwaka 2020/21. Aidha, Kitabu kinachoelezea maisha ya aliyekuwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa kimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na kinatarajiwa kuchapishwa katika robo ya mwisho wa mwaka 2020/21;

(x) Ushauri wa kitaalam kuhusu kuendesha mikutano, kuboresha na kuandaa programu na kufanya tathmini ya miradi umetolewa kwa Taasisi nne za Serikali ambazo ni Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha na Mipango,

Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) na Shirika la Reli Tanzania (TRL); na

(xi) Machapisho 18 yanayotokana na Tafiti kuhusu masuala ya Maendeleo Endelevu yalitolewa na yanapatikana kwenye tovuti ya Taasisi.

#### **D. MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)**

**29. Mheshimiwa Spika**,Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) umeendelea kutekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa Kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa Biashara nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, MKURABITA imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Huduma za Urasimishaji wa Biashara zimesogezwa kwa wananchi kwa kuanzisha Vituo vya Huduma kwa Pamoja katika Halmashauri ya Jiji la Arusha na Manispaa ya Musoma ambapo huduma muhimu za utoaji leseni za biashara, utoaji wa Namba ya Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN) kupitia TRA, usajili wa jina la biashara kupitia BRELA, huduma za benki na mifuko ya hifadhi ya jamii na huduma ya kuwezesha uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo kutoka SIDO zinapatikana sehemu moja. Aidha, katika Vituo vilivyoanzishwa kwenye Halmashauri ya Jiji la Arusha na Manispaa ya Musoma, jumla ya wafanyabiashara 1,540 wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara. Hadi kufikia Machi, vituo vimesajili majina ya biashara 284, Wafanyabiashara 529 wamepata Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi (TIN) na leseni za biashara 1,294 zimesajiliwa. Vituo vimewezesha ukusanyaji wa mapato ya Shilingi 168,150,260 yaliyotokana na ada za leseni. Ajira takriban 3,431 zimetolewa na biashara zilizorasimishwa;

(ii) Wafanyabiashara 200 waliorasimishiwa biashara zao katika Halmashauri ya Mji wa Njombe wamepata mafunzo ya namna bora ya kuendesha biashara katika mfumo rasmi.



Mafunzo haya yalitolewa na wadau kutoka TRA, Benki ya CRDB, SIDO na TCCIA;

(iii) Kituo Jumuishi kimoja cha urasimishaji na uendelezaji biashara kimeanzishwa katika Wilaya ya Mjini Unguja, Zanzibar. Taasisi zinazotoa huduma katika Kituo hicho ni Baraza la Manispaa Mjini, Wakala wa Dawa, Chakula na vipodozi, Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Bodi ya Mapato Zanzibar, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali pamoja na Benki ya Watu wa Zanzibar;

(iv) Ujenzi wa Masijala za Ardhi za Vijiji katika Halmashauri za Wilaya tatu za Mbarali (Kijiji cha Kapyo), Nachingwea (Kijiji cha Mbondo) na Mpwapwa (Kijiji cha Inzomvu) umekamilika;

(v) Urasimishaji ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino umefanyika ambapo jumla ya viwanja 3,191 vimetambuliwa na michoro ya Mipango Miji 10 yenye viwanja 1,152 imeandaliwa na kuidhinishwa. Hadi kufikia Machi 2021 jumla ya viwanja 375 vimepimwa na upimaji unaendelea uwandani. Aidha, jumla ya mashamba 107 yamepimwa na Hati Miliki za Kimila 107 zimeandaliwa. Vilevile, mafunzo ya kujenga uwezo wa kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila yametolewa kwa wananchi 70 wa Kijiji cha Manyemba-Chamwino na wananchi 342 wa Kijiji cha Lugodalutali katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi. Kwa upande wa Zanzibar, jumla ya Hati 43 za matumizi ya ardhi zimetolewa katika Shehia ya Welezo, Wilaya ya Magharibi B;

(vi) Elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa shughuli za urasimishaji imetolewa kupitia vipindi 33 vya redio, runinga na mitandao ya kijamii. Aidha, makala 21 yametolewa katika magazeti mbalimbali na mitandao ya kijamii; na

(vii) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za MKURABITA umefanyika Zanzibar katika Wilaya ya Mkoani, Chakechake, Kaskazini A, Mjini Unguja, Kaskazini B na Micheweni ambapo shughuli za urasimishaji ardhi na biashara zilifanyika.

## E. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

**30. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Maendeleo ya Jamii umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya TASAF kwa kuyapa kipaumbele maeneo ya Ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; Kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na Utawala bora na uwajibikaji. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Mfuko wa Maendeleo Jamii (TASAF) umetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini umekamilika katika Halmashauri nne za Nanyamba, Siha, Mtwara/ Mikindani na Kigamboni. Mitaa 28 na Vijiji 98 vimefikwa na jumla ya Kaya 6,791 zimetambuliwa. Utambuzi katika Halmashauri 180 na Unguja na Pemba unaendelea na unategemewa kukamilika ifikapo Juni 2021. Lengo ni kuzifikia Kaya zote ambazo hazikuwepo katika Kipindi cha Kwanza cha Mpango;

(ii) Utambuzi na Uhakiki wa awali wa kaya zilizoboreka umefanyika katika maeneo yote 186 ya utekelezaji. Jumla ya kaya 1,013,635 zilihakikiwa ambapo kaya 886,724 zimekidhi vigezo vya uhakiki wa awali wa kuendelea kuwepo katika Kipindi cha Pili cha Mpango.

Katika uhakiki huo Kaya 1,992 zimejitoa kwa hiari kwani Mpango umeboresha maisha yao. Matokea ya tafiti yamebaini Kaya 165,000 zimeboresha maisha yao na hivyo zitaondolewa kwenye mpango na hivyo kufanya jumla ya kaya 166,992 zenye wanakaya 834,960 kuhitimu na zitaondolewa kwenye Mpango;

(iii) Ruzuku ya Shilingi bilioni 135 ilihawilishwa kwa kaya maskini 883,194 za walengwa katika Halmashauri 184 zote za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar baada ya uhakiki kufanyika na kukamilika;

(iv) Miradi 12 ya kutoa ajira za muda kutoka katika Halmashauri 6 yenye thamani ya Shilingi milioni 900 imetekelezwa. Miradi hii imetoa ajira za muda kwa kaya za walengwa 39,337;

(v) Vikundi 120 vya kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya vyenye jumla ya walengwa 1,800 vimeundwa. Hivyo hadi sasa jumla ya vikundi 22,303 vyenye wanachama 311,114 vimeundwa kutoka mamlaka ya maeneo ya utekelezaji 51. Vikundi hivyo vimeweka akiba ya Shilingi bilioni 5.6 na kukopeshana Shilingi bilioni 3.6;

(vi) Mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa kumbukumbu za walengwa, uendeshaji na utoaji wa taarifa imeimarishwa kulingana na mahitaji ya utekelezaji wa Kipindi cha Pili cha TASAF Awamu ya Tatu. Halmashauri zote zimeunganishwa na mifumo ya TASAF Makao Makuu kupitia Miundombinu ya Mfumo wa TAMISEMI;

(vii) Jumla ya Halmashauri 39 zimeingizwa katika malipo ya njia ya Kielektroniki. Njia hii ya malipo inawezesha fedha kutumwa moja kwa moja kwa Walengwa kupitia mitandao ya simu, Benki na kwa namba ya NIDA na kumfikia kwa haraka na gharama nafuu;

(viii) Mapitio ya pamoja ya timu ya serikali na wadau wa maendeleo kuhusu utekelezaji wa shughuli za mpango yamefanyika katika vipindi vya mwezi Julai, 2020 na Januari, 2021. Taarifa zote za mapitio zimeonesha pande zote kuridhishwa na maendeleo ya utekelezaji wa Mpango;

(ix) Mafunzo ya kuwajengea uelewa kuhusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini wa kusimamia na kutekeleza shughuli za Mpango kwa ufanisi yametolewa kwa watumishi 261 wa TASAF makao makuu, watumishi 5,580 wa ngazi ya Halmashauri, Waratibu wa Mpango wa Mikoa 26 na Zanzibar; na

(x) Kupitia kujenga uwezo kwa watumishi katika ngazi mbalimbali za utekelezaji na kuongeza matumizi ya TEHAMA kumeboresha ufanisi na uwajibikaji katika usimamizi wa ufuatiliaji wa shughuli za Mpango na matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za utekelezaji.

## F. WAKALA YA NDEGE ZA SERIKALI

**31. Mheshimiwa Spika**,Wakala ya Ndege za Serikali ina jukumu la kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa. Wakala ilianzishwa ili kuboresha huduma na kuimarisha usalama wa usafiri wa ndege kwa viongozi wanaotumia huduma hizo. Aidha, Wakala imeongezewa jukumu lingine la kuratibu kwa niaba ya Serikali, ununuzi wa ndege, kuzikodisha kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege hizo.

**32. Mheshimiwa Spika**,Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Wakala wa Ndege za Serikali ilitekeleza kazi zifuatazo:

(i) Huduma za usafiri wa anga zimetolewa kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambapo jumla ya safari 104 za ndani na tatu za nje ya nchi zilifanyika;

(ii) Wanahewa tisa wamepatiwa mafunzo ya kisheria ya uhuishaji wa leseni zao;

(iii) Matengenezo madogo ya ndege mbili zinazowahudumia Viongozi Wakuu wa Kitaifa yalifanyika na vipuri vilinunuliwa kadri ya mahitaji.

Aidha, matengenezo makubwa ya Ndege aina ya Gulfstream kwa mujibu ya kalenda ya matengenezo yanaendelea kufanyika nchini Marekeni;

(iv) Gharama za bima za ndege pamoja na bima za Wanahewa zillipwa;

(v) Hatua za awali za ukarabati na upanuzi wa karakana ya Ndege za Serikali zimekamiliwa kwa kusaini mkataba na Mkandarasi; na

(vi) Wakala imeendelea kusimamia mikataba nane ya ukodishwaji wa Ndege za Serikali kwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL).

**OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

**33. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2020/21 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa **Shilingi 9,471,110,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 7,621,110,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,850,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2021 **Shilingi 5,365,126,200** Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 1,000,000,000** zilipokelewa na kutumika.

**34. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Malalamiko 112 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 58 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi na malalamiko 54 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, malalamiko 54 ambayo hayakuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma walalamikaji walipewa ushauri na mengine yalielekezwa kwenye mamlaka zinazohusika;

(ii) Jumla ya Viongozi wa Umma 14,981 ambao ni sawa na asilimia 99 kati ya Viongozi 15,110 wamarejesha Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa kipindi kilichoishia Machi, 2021. Jumla ya Viongozi 129 sawa na asilimia moja (1) ya Viongozi wote bado hawajarejesha Tamko. Kwa mujibu wa Sheria ya Maadili Fungu 15 (c) kuchelewa kutoa Tamko bila sababu za msingi ni kosa na ni ukiukwaji wa Maadili. Viongozi wasiorejesha wameandikiwa barua za kutoa maelezo na itakapobainika kuwa hawakuwa na sababu za msingi watachukuliwa hatua ikiwemo kufikishwa mbele ya Baraza la Maadili;

(iii) Uhakiki wa Tamko la Rasilimali na Madeni kwa Viongozi 609 waliopangwa kuhakikiwa umefanyika Mwezi Februari, 2021. Taarifa kuhusu zoezi husika inaonesha kuwa Viongozi wa Umma 534 walihakikiwa sawa na asilimia 87.8. Kati ya hao,

asilimia 20 ni wanawake na asilimia 80 ni wanaume. Matokeo ya uhakiki yanaonesha kuwa, asilimia 4.1 ya Viongozi waliohakikiwa mapungufu kwenye matamko walioyatoa. Mapungufu hayo yanajumuisha: baadhi ya vipengele vya tamko kutojazwa kwa ukamilifu, kutotaja thamani ya mali, kutotamka baadhi ya rasilimali wanazozimiliki na kutotamka maslahi binafsi. Aidha, asilimia 2.4 ya Viongozi wamebainika kuwa na viashiria vya Mgongano wa Maslahi. Viongozi wote waliobainika na mapungufu, watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(iv) Elimu kwa umma ilitolewa kwa jumla ya wadau 9,095 ambapo viongozi wa Umma 4,649, Watumishi wa Umma 4,294 na wananchi 152 kuhusu jinsi ya kujiepusha na mgongano wa maslahi na kuishi kwa kuzingatia kiapo cha Ahadi ya Uadilifu. Aidha, Klabu 82 za Maadili zenye wanachama 1,500 zilianzishwa katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo. Klabu 71 zilitembelewa kwa lengo la kukuza na kuendeleza maadili miongoni mwa wanafunzi na wanachama wa klabu. Lengo la klabu hizi ni kukuza na kuendeleza vijana katika kuzingatia Maadili na kujiandaa kuwa Viongozi wa kesho;

(v) Siku ya Maadili Kitaifa iliadhimishwa Kitaifa tarehe 10 Desemba, 2020 kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali zinazosimamia masuala ya utawala bora, uwajibikaji, haki za binadamu, mapambano dhidi ya rushwa na maadili. Maadhimisho ya Siku hii yalienda sambamba kwa kuzitembelea baadhi ya shule za msingi ambazo ni wanachama wa Klabu za maadili;

(vi) Jumla ya Viongozi wa Umma 5,093 walioteuliwa/ kuchaguliwa kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi katika utumishi wa umma walisaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu;

(vii) Utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma umeendelea na umesaidia kuboresha utendaji kazi katika kufuatilia tabia na mienendo ya viongozi wa umma. Katika kipindi husika, Kanuni za Ufuatiliaji wa Ahadi ya Uadilifu kwa viongozi wa umma ziliandaliwa na kuanza kutumika mwezi Novemba, 2020. Kanuni zinatoa mwongozo wa namna bora

ya kufuatilia tabia na mienendo ya viongozi waliosaini kiapo cha uadilifu na hatua za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa pale viongozi wanapokiuka kiapo husika;

(viii) Ujenzi wa Ofisi za Sekretarieti ya Maadili Makao Makuu Dodoma ambao unafanywa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) unaendelea na kwasasa hatua iliyofikiwa ni ujenzi wa ghorofa ya nne (structure); na

(ix) Mfumo wa Ujazaji Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya mtandao umejengwa na kuunganishwa na Mfumo wa Mamlaka za Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na ulikamilika mwezi Aprili, 2020 na mfumo kuanza kutumika kwa majaribio. Hadi kufikia Desemba, 2020, jumla ya matamko 4,357 yaliwasilishwa kupitia mfumo. Kati yao 3,817 ni ya mwisho wa kutumikia wadhifa, 215 matamko ya cheo kipya na 325 matamko ya mwaka. Hata hivyo Desemba, 2020 Mfumo husika ulisitishwa na viongozi kutakiwa kuwasilisha kwa kutumia njia ya zamani wa karatasi.

## OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA WAKALA ZAKE

### A. MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA

**35. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2020/21, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma: Fungu 32 inayojumuisha Mamlaka na Wakala iliyo chini yake, iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 43,878,828,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 32,923,578,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 10,955,250,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**36. Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Machi, 2021 **Shilingi 30,350,465,668.19** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo Shilingi **21,949,423,716.38** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **8,401,041,951.81** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**37. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Taasisi za Serikali zimejengewa uwezo wa kuandaa Sera za Kisekta zinazozingatia utafiti ili kuziwanisha na kuondoa migongano na urudufu wakati wa utekelezaji: Taasisi hizo ni Wizara ya Viwanda ambao walijengewa uwezo wa kuandaa Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Vile vile, Ofisi ya Rais Uwekezaji ilijengewa uwezo wa kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji;

(ii) Kanuni za Utumishi wa Umma zilikuishwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata ushauri wa kisheria;

(iii) Uhamasishaji wa ujumuishwaji wa masuala ya Anuai za Jamii (Jinsia, ulemavu, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa) umefanyika ili kuhakikisha anuai zote katika utumishi wa umma zinapata mazingira sawa ya kiutumishi;

(iv) Tathmini ya utekelezaji wa Miongozo inayosimamia ujumuishwaji wa makundi maalumu (Anuai za Jamii) imefanyika katika Taasisi 25 za Umma na kuandaa Taarifa inayoonesha maeneo ya kuboreshwa katika kuhakikisha jinsia zote zinajumuishwa katika utumishi wa umma na kupata mazingira sawa ya kazi;

(v) Makala ya Utekelezaji wa Miongozo wa Huduma kwa watumishi wa umma wenye ulemavu imeandaliwa. Pia, Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma (*Standing Orders*) zimewekwa katika mfumo wa sauti ili kuwawezesha watumishi wa umma wenye ulemavu wa kuona waweze kuzielewa;

(vi) Imetolewa Miongozo ya Kuimarisha Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Nyaraka za Kiutumishi ikiwemo ufafanuzi kuhusu Utaratibu wa Kupokea Maelekezo/Maagizo yanayotolewa na Viongozi kwa Njia ya Mdomo; Waraka



Kuhusu Baraza la Mawaziri Kuendelea Kutekeleza Majukumu yake Baada ya Bunge Kuvunjwa; Mwongozo kuhusu Viongozi na Watendaji Wakuu wa Umma Kuandaa Taarifa za Makabidhiano ya Ofisi; na Waraka wa Mavazi katika Utumishi Umma;

(vii) Uwianishaji na uoanishaji wa viwango vya mishahara katika utumishi wa Umma umefanyika kwa taasisi 40 kwa kupitia nyaraka za Maendeleo ya Utumishi za Taasisi hizo na kwa kuzingatia matokeo ya zoezi la Tathmini ya Kazi;

(viii) Nyumba 132 zimeendelea kujengwa katika eneo la Kisasa Njedengwa - jijini Dodoma ambapo nyumba 40 zilijengwa katika awamu ya kwanza na kuuzwa kwa watumishi wa umma na awamu ya pili ya ujenzi ina nyumba 92 ambazo zipo katika hatua za mwisho za ujenzi na mauzo yake yamefikia asilimia 75%;

(ix) Upimaji wa viwanja 331 katika eneo la Usa River - Arusha kwa kushirikiana na Halmashauri ya Arumeru umefanyika na viwanja hivyo vinatarajiwa kuuzwa kwa bei nafuu kwa watumishi wa umma, wafanyakazi wa sekta binafsi na wanachama wengine wa mifuko ya hifadhi ya jamii. Mawasiliano na Halmashauri nyingine 20 yanaendelea kwa ajili ya kupimiwa viwanja;

(x) Miundo ya Taasisi za Umma 41 imehuishwa ambapo Mitano (5) imeshapitishwa na Kamati ya Rais ya Utekelezaji (PIC). Aidha, Miundo ya jiji la Dar es salaam na Dodoma, Ofisi za Afisa Tawala za mikoa 26 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 183 imehuishwa ili kuendana na matakwa ya utoaji huduma na maelekezo ya Serikali;

(xi) Taasisi za umma 26 zimewezeshwa kwa kupewa utaalam wa uchambuzi ili kuandaa Orodha ya Kazi na Maelezo ya Kazi zitakazotoa viwango na kutengeneza uwiano mzuri wa watumishi katika kutekeleza majukumu ya Taasisi husika;

(xii) Michakato ya utoaji huduma imeendelea kuboreshwa na kuimarisha usimamizi wa Mifumo na Viwango vya utendaji

kazi kwa kufanya ufuatiliaji pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam katika Taasisi za Serikali ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi ambapo Taasisi 23 zimewezeshwa kuandaa Mipango Mkakati; taasisi mbili zimewezeshwa kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Mteja; taasisi moja imesaidiwa kitaalam kujifanyia tathmini ya utoaji huduma wa taasisi (Institutional Self Assessment – ISA).

Vile vile, watumishi 200 wa ajira mpya na waliohamia OR-MUUUB wamepatiwa mafunzo ya uandishi wa nyaraka mbalimbali za kiserikali kama zilivyo kwenye Mwongozo wa Serikali;

(xiii) Maandalizi ya Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Kitaifa yametengenezewa Kamati ya Wataalam wajumbe 12 wanaosimamia shughuli za ufuatiliaji na tathmini Serikalini. Aidha, Sekretarieti ya kamati iliundwa ili kusimamia programu ya uimarishaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini Serikalini ikiwa ni pamoja na kuandaa Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini. Kamati hiyo imeshafanya vikao vitano vya maandalizi ya utekelezaji wa programu hiyo;

(xiv) Maandalizi ya Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini Serikalini ambao utaunganisha Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini iliyopo katika Taasisi zote za Umma yameanzishwa kwa kutengeneza nyenzo (tool) ya kukusanyia taarifa za msingi;

(xv) Vibali vya ajira mpya na mbadala vyenye nafasi 11,064 kwa kada mbalimbali vimetolewa;

(xvi) Mwongozo wa Ikama na Bajeti ya Mishahara ya Watumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 umetolewa kwa Waajiri wote;

(xvii) Ukaguzi na usimamizi sahihi wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) katika Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma umefanyika kupitia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS);

(xviii) Usafishaji na uboreshaji wa taarifa za kiutumishi na mishahara za watumishi kwa waajiri wote wanaotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) umefanyika;

(xix) Watumishi wa umma 23,971 wa kada mbalimbali waliopandishwa vyeo waliidhinishwa kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara;

(xx) Madai ya malimbikizo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma yaliyolipwa na Wizara ya Fedha na Mipango baada ya kuhakikiwa na kuidhinishwa na Ofisi yangu ni jumla ya watumishi 37,388 yenye thamani ya Sh. 69,141,217,747.35 na madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 17,699 yenye thamani ya Sh. 37,474,809,031.55 yanaendelea kuhakikiwa na Ofisi yangu.

(xxi) Katika kuimarisha utawala wa Utumishi wa Umma, waajiri mbalimbali waliwezesha kwa kupewa vibali vya uhamisho vya watumishi wa umma 1,988, kuazimwa 836 na kushikizwa 76;

(xxii) Ofisi imewawezesha waajiri kujaza nafasi za uongozi kwenye taasisi zao kwa kushughulikia maombi ya nafasi za uteuzi kwa Maafisa 407 ambapo kati ya hayo, maombi kwa Maafisa 330 yalirejeshwa kwa waajiri kwa utekelezaji na vibali vya uteuzi 150 vilitolewa kwa nafasi za uongozi ambazo zilipendekezwa kwa afisa zaidi ya mmoja. Aidha, vibali vya ajira za mikataba 49 vilishughulikiwa na vibali 317 vya kukaimu nafasi za uongozi vilitolewa;

(xxiii) Uboreshaji wa taarifa za Viongozi wa Serikali, Maafisa Wakuu na Waandamizi (Kanzidata) umeendelea kufanyika kupitia Mfumo mpya wa HCMIS ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa zao (Position management) kwa lengo la kuwezesha zoezil la upekuzi, uteuzi na uhamisho ili kujaza nafasi wazi za Uongozi katika Utumishi wa Umma;

(xxiv) Fursa za mafunzo zinazotolewa na Wadau wa Maendeleo kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora zimeendelea kuratibiwa ambapo

watumishi wa umma 21 wamepata ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi wa Serikali ya Jamhuri ya Korea. Mafunzo haya ni muhimu kwa watumishi wa umma kwa sababu yanawaongezea ujuzi na maarifa ya kutekeleza majukumu kwa ustadi na ufanisi;

(xxv) Usanifu wa Mfumo wa Kielektroniki wa Uandaaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu (e-HRP) umekamilika na Ofisi inaendelea na ujenzi wa mfumo;

(xxvi) Ufuatiliaji umefanyika kwa Vyuo vya Serikali vyenye jukumu la kutoa mafunzo ili kuhakikisha waajiriwa wapya wanapata mafunzo elekezi ya uendeshaji na utendaji kazi wa serikali. Watumishi wa umma wapya 1,081 walipatiwa mafunzo ya awali katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Chuo cha Serikali za Mitaa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama ili kuwawezesha kuelewa misingi ya Utumishi wa Umma, Sheria, Kanuni na Taratibu za utendaji kazi katika Utumishi wa Umma;

(xxvii) Uratibu wa Ajira za Wataalam wazawa katika Taasisi za Kikanda na Kimataifa ulifanyika ambapo nafasi 20 za ajira. Ajira hizo ni kutoka Mashirika ya Kimataifa ikiwemo Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Utalii (UNWTO), Jumuiya ya Madola, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB);

(xxviii) Ziara zimefanyika kwenye Miradi ya Maendeleo saba ili kukagua namna Wataalam wa Kigeni wanaofanya kazi katika Utumishi wa Umma wanavyotekeleza majukumu yao na kuchangia katika kuwajengea uwezo wataalam wazalendo. Miradi iliyotembelewa ni Wizara ya Maji; Baraza la Wakimbizi la Norway (NRC); Plan International; Shirika la Madaktari Wasio na Mipaka (MSF); Barabara ya Mikumi na Ifakara; Ujenzi wa Daraja la Mto Ruaha na mradi wa Kufua Umeme Rusumo na Murongo/Kikagati mkoani Kagera;

(xxix) Ajira za wataalam wa kigeni katika Utumishi wa Umma zimeendelea kuratibiwa ambapo wataalam 487 wanaofanya kazi kwenye Utumishi wa Umma

wamwezesha kupata vibali vya kazi. Ajira hizi zipo katika Sekta muhimu za Maendeleo ya Uchumi na Huduma za Jamii kama Kilimo, Ujenzi, Nishati, Elimu na Maji. Ajira hizi pia zinachangia katika kuwaongezea ujuzi na maarifa watanania;

(xxx) Taasisi za Umma 17 zimwezesha kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu na Taasisi za Umma 18 zimejengewa uwezo wa kuandaa Mpango wa Urithishanaji Madaraka;

(xxxi) Watumishi wa umma 3,911 kutoka taasisi 37 za umma walipatiwa mafunzo kuhusu umuhimu wa kupunguza malalamiko ya wateja na jinsi ya kushughulikia malalamiko yanayowasilishwa;

(xxxii) Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma zilifanyiwa mapitio na maandalizi ya kuwasilisha rasimu ya mwisho ya Kanuni katika kikao cha wadau yamefanyika;

(xxxiii) Maafisa Malalamiko na wajumbe wa Kamati za Kudhibiti Uadilifu katika Taasisi za Umma tisa wamepatiwa mafunzo ya utekelezaji wa Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko ya Wananchi katika Utumishi wa Umma;

(xxxiv) Kampeni za kimaadili zimefanyika katika Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma, Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Mbinga na Songea na Halmashauri za Wilaya za Mbinga, Songea, Namtumbo na Madaba ambapo watumishi 567 wamepata mafunzo ya Maadili katika Kampeni hizo.

(xxxv) Uhamasishaji wa uzingatiaji wa maadili kupitia vyombo vya habari umefanyika ambapo jumla ya vipindi vya redio 7 na vipindi 9 vya televisheni viliandaliwa na kurushwa;

(xxxvi) Malalamiko 137 ya wananchi yaliyohusu ukiukwaji wa maadili katika Utumishi wa Umma yalipokelewa na kushughulikiwa;

(xxxvii) Taasisi za Umma 29 zilipatiwa mafunzo ya namna ya kuendesha Kamati za Uadilifu. Mafunzo yalitolewa kwa

kushirikiana na Ofisi ya Rais – Idara ya Utawala Bora na Maboresho, Ofisi ya Rais - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa;

(xxxviii) Ujenzi wa mfumo mpya wa HCMIS umekamilika na kuanza kutumika kuingiza Bajeti ya Mishahara (PE Budget) ya Mwaka wa Fedha 2021/22;

(xxxix) Upembuzi yakinifu wa uanzishwaji wa Vituo vya Huduma Jamii kwa ajili ya kutoa Huduma za Serikali sehemu moja umefanyika. Aidha, matayarisho ya kuanza hatua ya majaribio katika mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma yanaendelea;

(x) Maandalizi ya Kanzi data ya wataalamu wa TEHAMA waliopo kwenye Ofisi za Serikali na uwezo wao wa utendaji yamefanyika ili kuwezesha kuwa na mpango jumuishi wa kuwajenga uwezo wataalamu wote katika kujenga na kusimamia mifumo ya TEHAMA ya Serikali;

(xi) Tathmini ya uzingatiaji wa mwongozo wa kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao wa Mwaka 2017 imefanyika katika taasisi za Serikali nne ili kuongeza ubora wa huduma zitolewazo kwa TEHAMA;

(xii) Ukaguzi wa usalama wa mfumo mpya wa HCMIS wa awamu ya kwanza kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 umefanyika mwezi Disemba, 2020 na kubaini maeneo ya maboresho ambayo tayari yamefanyiwa kazi. Hatua ya pili ya ukaguzi wa usalama wa mfumo wa HCMIS na e-OPRAS umepangwa kufanyika mwezi Aprili, 2021;

(xiii) Maandalizi ya kuhuisha Mkakati wa Taifa wa utekelezaji wa Serikali Mtandao yamefanyika kwa kutayarisha madodoso ya kukusanya taarifa za hali ya halisi ya utekelezaji wa Mkakati uliomalizika kama msingi wa mwelekeo wa Mkakati mpya;

(xiv) Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Serikali Mtandao zimeandaliwa, kuidhinishwa na kuanza kutumika mwezi

Februari, 2020. Aidha, mafunzo kuhusiana na utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Serikali Mtandao yametolewa kwa Wakuu wa Idara/Vitengo vya TEHAMA 400 kutoka taasisi za Serikali;

(xv) Maandalizi ya Programu ya Dijitali Tanzania kwa upande wa ndani ya Serikali yamekamilishwa kwa ushirikiano na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (WMTH). Aidha, utekelezaji wa Programu utafanyiwa majadiliano ya mwisho kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia kufikia mwezi Aprili, 2021;

(xvi) Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Usalama wa Huduma za Kielektroniki imefanyika kwa taasisi nne na kusaidia kuboresha miongozo ya kiusalama ya taasisi katika kusimamia shughuli za TEHAMA;

(xvii) Mafunzo ya namna ya kutumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) yametolewa kwa Maafisa Utumishi/Tawala na viongozi 1,139 kutoka Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xviii) Ujenzi wa mfumo wa e-OPRAS ambao utatumika kupanga na kupima utendaji kazi wa watumishi wa umma umekamilika na majaribio ya Mfumo yamefanyika. Watumishi wa OR-MUU wamejengewa uwezo wa kutumia mfumo huo;

(xix) Uwezeshaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) kwenye Taasisi za Umma umefanyika kwa kutoa mafunzo na ushauri wa ujazaji fomu katika Taasisi 15 zilizowakilishwa na watumishi 93;

(xx) Uwezeshaji wa uandaaji na utekelezaji wa mkataba wa utendaji kazi umefanyika kwa kutoa mafunzo kwa taasisi za Umma tano. Mikataba hii inakuza uwajibikaji wa Taasisi kwa umma na taasisi simamizi;

(xxi) Uelewa wa wananchi kuhusu huduma zitolewazo na Ofisi na upatikanaji wake ulitolewa kwa njia mbalimbali za

mawasiliano ikiwemo vipeperushi na vitabu, mikutano ya wadau na semina; Taarifa 41 kwa vyombo vya habari, matukio katika picha za 210, Makala fupi za video 38 katika mitandao ya kijamii ya Ofisi ya Rais-Utumishi (Youtube, facebook na twitter) na kusambazwa kwa wadau wa OR-MUUUB kupitia mtandao wa kijamii wa whatsapp, Makala katika magazeti mbalimbali, Jarida Tando la OR-MUUUB na kupitia matangazo katika Mfumo wa HCMIS na katika matoleo 35 ya Gazeti la Serikali Aidha, Taarifa kuhusu Nyaraka za Kitumishi na taarifa mbalimbali kama vile Nafasi za Kazi, (za ndani na nje ya nchi), nafasi za masomo nje ya nchi zimewekwa katika Tovuti;

(xxii) Maandalizi ya ujenzi wa majengo ya Klabu ya Viongozi katika Utumishi wa Umma (Leaders Club) yamefanyika kwa kupata kiwanja chenye ukubwa wa hekta 30 katika eneo la Njedengwa Hill top - Dodoma, kusafisha eneo na kupanda miti ya matunda na miti kwa ajili ya uzio.

(xxiii) Huduma zimeendelea kutolewa kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Wastaafu 11 na wajane 6) kwa mujibu wa sheria.

## **B. CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA(TPSC)**

**38. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa ili kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma, ushauri wa kitaalam, kufanya utafiti tumizi na kutoa machapisho mbalimbali katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala. Aidha, Chuo kinaendesha kozi za kitaaluma kwa ngazi za Cheti, Stashahada na Shahada katika nyanja za Uhazili, Utunzaji Kumbukumbu, Menejimenti ya Rasilimaliwatu, Utawala na Ununuzi wa Umma. Vile vile, Chuo kinasaidia Serikali kukuza Sera za Utamaduni wa kujifunza na kusaidia utumiaji wa teknolojia miongoni mwa watendaji katika kutekeleza majukumu yao. Chuo kinatekeleza majukumu yake katika Kampasi sita zilizoko kwenye Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga na Mbeya. Pia, Chuo kinatoa huduma za mafunzo kwa njia ya mtandao kutokea katika kituo cha mafunzo kwa njia ya mtandao kilichopo Dar es Salaam.



**39. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Chuo cha Utumishi wa Umma kimeteteleza shughuli zifuatazo:-

(i) Watumishi 375 walipatiwa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mithani ya Utumishi wa Umma kwa Watumishi ili kuimarisha utendaji kazi wao na kutoa huduma bora kwa wananchi;

(ii) Watumishi wa umma 3,910 walipatiwa mafunzo ya Uongozi na Maendeleo, Menejimenti na Usimamizi wa Ofisi katika kuimarisha taswira nzuri ya utumishi wa umma;

(iii) Mafunzo ya awali yalitolewa kwa watumishi wa umma wapya 864 katika kuwajengea uwezo wa kutenda kazi za serikali kwa usahihi na kwa mujibu wa taratibu;

(iv) Wanachuo 9,947 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, na Menejimenti ya Rasilimali Watu, Usimamizi na Manunuzi ya Umma, Uongozi na Utawala Bora ili kuwapatia stadi, weledi na ujuzi wa kazi za Serikali;

(v) Ushauri wa kitaalam katika maeneo manne ulitolewa ili kuwawezesha watumishi wa umma kuboresha mifumo na mbinu za utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa mahitaji halisi ya utumishi wa umma na wadau mbalimbali kwa lengo la kutatua changamoto za utendaji na kuendeleza mchango wa utumishi wa Umma katika ustawi wa Taifa;

(vi) Utaalam wa Kimataifa na Kitaifa katika fani mbalimbali ikiwemo menejimenti ya utumishi umma uliwezesha kwa kufanya midahalo iliyosaidia kubadilishana uzoefu kwa njia ya mtandao kwa washiriki 1,066;

(vii) Kufanikisha mafunzo kwa njia ya mtandao yaliyotolewa kwa washiriki 1,249. Njia hii ilisaidia Serikali kupunguza gharama, kuwa na mazingira rafiki katika kujifunza, kutoa fursa ya kuepuka muingiliano wa mafunzo na majukumu ya kazi na kupunguza safari nje ya vituo vya kazi;

(viii) Katika kujenga hazina bora ya wakufunzi, watumishi 8 wa chuo waliwezesha kuendelea na masomo katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu na Shahada ya uzamili;

(ix) Maandalizi ya kuanza ujenzi wa majengo katika eneo la Mungumaji Singida yameanza kwa kuwasilisha maombi ya kibali cha ujenzi, kumpata Meneja wa Mradi, kutafuta taasisi ya Serikali itakayofanya kazi ya ujenzi. Hivyo, ujenzi huo utanza rasmi katika Robo ya nne ya mwaka 2020/21 baada ya taratibu zote kukamilika. Aidha ujenzi wa majengo kwa ajili ya shughuli za Kampasi ya Tanga utanza baada ya kukamilika kwa taratibu zote. Ujenzi majengo ya Kampasi hizi mbili utafanyika kwa kutumia mfumo wa nguvu kazi (Force Account).

(x) Kazi ya kuandaa michoro ya usanifu majengo (“archtectural design”) kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa majengo ya Kampasi ya Kanda ya Ziwa inaendelea; na

(xi) Ufuatiliaji wa kupata eneo la ujenzi wa kampasi ya Mbeya unaendelea.

### **C. MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA)**

**40. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ilianzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019. Mamlaka ilianzishwa ili Kuratibu, Kusimamia na Kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa taasisi za umma. Mamlaka imerithi iliyokuwa Wakala ya Serikali Mtandao ambayo iliundwa kwa Sheria Na. 30 ya Wakala za Serikali, Sura ya 245 ya Mwaka 1997 na kuwa na jukumu la Kuratibu, Kusimamia na Kukuza Jitihada za Serikali Mtandao nchini bila kuwa na nguvu ya kisheria ya kuhimiza utekelezaji (kuwa chombo rekebu). Wakala ilitekeleza majukumu yake kwa kipindi cha miaka nane (8) tangu kuzinduliwa kwake Mwezi Aprili, 2012 mpaka Mwezi Februari, 2020.

**41. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, imebuni na kutengeneza Mfumo wa Taarifa za Huduma na Ankara za Maji ujulikanao kama "Maji Information System" - (MAJIS) kwa ajili ya matumizi ya Sekta ya Maji ambapo Mamlaka za Maji zipatazo 26 zimeanza kutumia hivyo kuwezesha Mamlaka mbalimbali kusimamia masuala ya maji kielektroniki na wananchi kupata huduma mbalimbali za maji kutoka kwa mamlaka za maji kielektroniki;

(ii) Mamlaka imeongeza taasisi zinazotumia Mfumo wa kutolea huduma kupitia simu za mkononi (Government Mobile Platform) kufikia 176 na kufanya maboresho kwa kuuongezea huduma za "e-Wallet" na "MT charging" zinazowawezesha wananchi kupata huduma kupitia "mobile wallet" kwa maana ya kulipia huduma za kiserikali (GePG) kupitia Salio lililopo kwenye T-Pesa, M-Pesa, Tigo Pesa na Airtel Money moja kwa moja kutoka kwenye \*152\*00#;

(iii) Mifumo Shirikishi ya Barua pepe inayotumiwa na taasisi zaidi ya 500 na ule wa Ofisi Mtandao inayotumiwa na taasisi zaidi ya 120 imeendelea kusimamiwa, kuendeshwa na kuboreshwa. Aidha, Mamlaka imeendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango katika kuhakikisha kuwa Mfumo wa malipo Serikalini wa GePG unafanya kazi ipasavyo.

(iv) Mamlaka imeendelea kusimamia, kuendesha na kuboresha Miundombinu Shirikishi ya TEHAMA inayotumiwa na taasisi za umma, kutoa ushauri wa kitaalamu na kuziwezesha taasisi 265 kuunganishwa kwenye Mtandao wa Serikali (GovNet). Aidha, Mamlaka imeendelea kusimamia Vituo vinavyohifadhi miundombinu na mifumo shirikishi katika kuwezesha Serikali na taasisi zake kutoa huduma kwa wananchi kielektroniki;

(v) Mamlaka imeendelea kusimamia usalama wa miundombinu na mifumo yote inayotoa huduma mbalimbali

kwa wananchi kidijitali sambamba na kutoa msaada wa kiufundi kwa taasisi zote zinazojihusisha na huduma za Serikali kidijitali;

(vi) Mamlaka imekamilisha uanzishwaji wa Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Maendeleo ya TEHAMA kwenye eneo la muda lililopo ndani ya Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Kompyuta na Elimu Angavu (College of Informatics and Virtual Education) baada ya kukarabati iliyokuwa maabara ya zamani ya ndaki hiyo. Katika Mwaka wa Fedha 2020/21, kituo kimeanza kupokea wanafunzi kutoka vyuo vikuu mbalimbali nchini kwa ajili ya kupata mafunzo ya kuchochea ubunifu na ugunduzi kwenye huduma za Serikali mtandao kwa vitendo;

(vii) Mamlaka ya Serikali Mtandao imeweza kujenga ushirikiano na Taasisi nane (8) za elimu ya juu katika shughuli mbalimbali zinazohusiana na utafiti, ubunifu na maendeleo ya TEHAMA Serikalini. Aidha, wanafunzi 35 wanaofanya mafunzo kwa vitendo kutoka vyuo mbalimbali nchini wamesimamiwa katika mafunzo hayo huku wanafunzi wa mwaka wa mwisho wanaochukua kozi za TEHAMA wanaendelea kupatiwa ushauri kwenye kazi za miradi au utafiti kwenye maeneo wanayofanya ili kuhitimu mafunzo yao. Vyuo vinavyoshirikiana na Kituo cha Mamlaka ni UDOM, UDSM, DIT, NIT, IFM, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph cha Teknolojia na Chuo cha Uhasibu Arusha;

(viii) Mamlaka pia imeingia Makatiba wa ushirikiano na vyuo 13 vya elimu ikiwemo Chuo cha Utumishi wa Umma ili kushirikiana kutoa mafunzo ya matumizi ya TEHAMA kwa wafanyakazi wa Umma. Hadi sasa vyuo vya IFM na MZUMBE wamepatiwa mafunzo ya ukufunzi ili kufundisha watumishi wa Umma kwenye matumizi ya mifumo inayotumika Serikalini pamoja na mafunzo ya ukufunzi wa ufundishaji wa Sheria, kanuni, viwango na miongozi ya Serikali Mtandao;

(ix) Mamlaka imekamilisha usanifu wa ujenzi wa Maktaba Mtandao kwa asilimia 90 na vitabu vipya 76 pamoja na

majalada na machapisho vimeongezwa, wakati huo huo, Maabara ya kielektroni (e-Laboratory) inaendelea kuimarishwa kwa kuisheheneza na vifaa mbalimbali vya kielektroni; na

(x) Mamlaka imesanifu na kutengeneza Mifumo minne ambayo ni '**e-Dodoso**' unaohusika na ukusanyaji taarifa za ufuatiliaji na tathmini na '**e-Mikutano na e-Bodi**' inayohusika na kuendesha Mikutano kwa njia ya video/mtandao. Pia, Mfumo wa "**eMalalamiko**" ambao ni Mfumo wa kupokea maoni na malalamiko yanayohusu huduma zinazotolewa na taasisi za umma kwa njia ya mtandao na simu umekamilika na kuanza kutumika na unapatikana kwenye Komputa na Simu za Kupangusa kwa kupitia <https://emalalamiko.gov.go.tz>. **Hivyo, Taasisi zote za Umma zinatakiwa kutumia njia hii kupokea mrejesho wa huduma zake kwa wananchi kidijitali kwa urahisi na usiri unaotakiwa kiutawala bora na kuimarisha dhana ya uwazi na uwajibikaji.** Mifumo hii ni matokeo ya utafiti na ubunifu kulingana na mahitaji yanayoendana na uchumi wa kidijitali na hali yetu halisi ya kitanzania.

## **OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

**42. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ni idara inayojitegemea iliyoanzishwa kwa mujibu wa Kifungu 29 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 ili kusimamia mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma. Katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 067: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliidhinishwa **Shilingi 3,360,526,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2021, **Shilingi 2,514,966,866.43** zilipokelewa na kutumika.

**43. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Sekretarieti imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Matangazo mia moja na themanini na tano (185) yaliandaliwa na kutolewa kwa niaba ya waajiri 51 katika Utumishi wa Umma;

(ii) Usimamizi na uendeshaji wa michakato ya ajira umefanyika mara nane (8) kwa niaba ya waajiri 51 ambapo wasailiwa 2,296 waliofaulu usaili na walipangwa katika vituo vya kazi mbali mbali kama ifuatavyo:- wawili walipangwa katika Ofisi ya Bunge la Tanzania, wawili walipangwa katika Mahakama ya Tanzania, 82 walipangwa katika Wizara, 1,149 walipangwa katika Mashirika ya Umma, watatu walipangwa katika makampuni ya Serikali, 289 walipangwa katika Wakala za Serikali, 305 walipangwa katika Mamlaka mbalimbali, 140 walipangwa katika Mamlaka za Serikali za Mtaa, 87 walipangwa katika Taasisi nyingine za serikali, 79 walipangwa katika Taasisi za Elimu, 13 walipangwa katika Sekretarieti za Mikoa, watatu walipangwa katika Idara zinazojitegemea, 71 walipangwa katika Hospitali za Umma, 16 walipangwa katika Tume za Serikali, watatu walipangwa katika bodi za serikali. Kati ya waajiriwa hao, sita (6) ni wenye mahitaji maalum, kati ya hao wanaume ni watano na mmoja ni mwanamke. Aidha, Wazanzibari walioajiriwa katika Wizara na taasisi za Muungano ni saba (7) kati ya hao wanaume ni 5 na wanawake ni 2 kwa kuzingatia utekelezaji wa makubaliano ya Ajira kwenye Taasisi za Muungano.

(iii) Mamlaka za serikali za mtaa 48 zimesimamiwa na kuwezesha kuajiri watumishi 195 wa kada mbali mbali. Halmashauri hizo ni Chemba, Mpwapwa, Dodoma Jiji, Songea, Nzega, Kaliua, Tunduru, Songwe, Urambo, Maswa, Ushetu, Nachingwea, Korogwe, Tandahimba, Mbarali, Uvinza, Mufindi, Ruangwa , Siha, Iramba, Nyasa, Bahi, Mbinga, Mufindi, Mafia, Mpwapwa, Mkinga, Njombe;

(iv) Utaalam wa masuala ya uendeshaji wa mchakato wa ajira ulitolewa kwenye usaili unaoendeshwa na taasisi zinazotumia Sheria zilizokasimiwa kwa taasisi husika ambapo taasisi 48 zilisimamiwa na kuweza kuajiri watumishi 145 katika kada mbali mbali;

(v) Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira iliyopo Zanzibar imeendelea kuboreshwa ili kurahisisha michakato ya ajira za Muungano kwa kuongeza majukumu ya kawaida pamoja na idadi ya watumishi;

(vi) Watumishi wote wa Sekretarieti ya Ajira wamewezeshwa kuhama kutoka Dar es Salaam kuja Makao Makuu ya nchi jijini Dodoma;

(vii) Taasisi imeanza kufanya tafiti kwa waajiri na wadau mbalimbali ikiwa ni hatua ya kupata mrejesho wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa michakato ya ajira pamoja na utendaji kazi wa Taasisi ili iweze kujitathmini;

(viii) Taasisi imeimarisha utendaji kazi wake kwa kutumia TEHAMA; ambapo imekamilisha zoezi la upokeaji maoni na "design work" ya maboresho katika mfumo wa Ajira (Ajira Portal). Kazi inayoendelea sasa ni ujenzi wa Ajira App ambayo itawawezesha waombaji kazi kuweza kupata taarifa za ajira na mrejesho wa michakato ya Ajira kupitia simu zao za kiganjani;

(ix) Taasisi imeanza Mchakato wa kuboresha mfumo mpya wa uendeshaji usaili kwa kutumia "psychometric Test" na unatarajiwa kumalizika na kujaribiwa katika hatua za awali mwanzoni mwa mwaka ujao wa fedha 2021/2022. Jumla ya wataalamu sita (6) kutoka vyuo vikuu vya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Mwalim Nyerere Memorial Academy (MNMA) na Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) wanaendelea kuutengeneza mfumo huo kwa ufasaha.

(x) Sekretarieti ya Ajira imeendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu fursa mbali mbali za Ajira zilizopo ikiwemo kutoa matangazo mbali mbali ya kazi kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, zaidi ya matangazo 185 yametangazwa kwenye tovuti ya Taasisi kuhusu uwepo wa nafasi wazi za kazi, kuitwa kwenye usaili pamoja na 6 kupangiwa vituo vya kazi. Pia imeendelea kuwaelimisha waombaji kuhusu matumizi ya Mfumo wa maombi ya kazi kadri ya maboresho yanavyoendelea kufanyika;

(xi) Sekretarieti ya Ajira imesimamia usaili mmoja ulizokasimiwa kuendeshwa na Vyuo Vikuu vya Umma nchini. Chuo Kikuu

kilichoendesha usaili huo hadi kufikia Machi, 2021 ni Muhimbili Health and Alliance Sciences (MUHAS);

(xii) Vyeti 958 vilikaguliwa ili kuhakiki taarifa mbalimbali za waombaji kazi, katika vyeti hivyo hakukuwa na vyeti vya kugushi. ***Takwimu hizi zinathibitisha kuwa kiwango cha matumizi ya vyeti visivyo halali kimepungua sana ikiwa ni matokeo ya kuimarika kwa uhakiki na mifumo ya Serikali.***

## OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

**44. Mheshimiwa Spika**, Tume ni chombo rekebu chenye mamlaka na wajibu wa kuhakikisha kuwa masuala ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma yanasimamiwa na kuendeshwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu mbalimbali kama inavyotolewa na Mamlaka. Wajibu huu una lengo la kuimarisha Utawala Bora unaozingatia matokeo. Katika kutekeleza wajibu huu, pamoja na mambo mengine, Tume imeendelea kufanya ukaguzi wa Rasilimaliwatu kwa Mamlaka za Ajira na Nidhamu. Aidha, Tume ya Utumishi wa Umma ni Mamlaka ya Rufaa kwa Watumishi wa Umma dhidi ya Uamuzi unaotolewa na mamlaka zao za nidhamu.

**45. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Fungu 94 Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 5,231,094,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2021 **Sh. 3,609,953,795.51** zilipokelewa na kutumika.

**46. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Tume imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Ukaguzi umefanyika kuhusu uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za usimamizi wa rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma katika Taasisi 86;

(ii) Rufaa na Malalamiko ya Watumishi wa Umma yalishughulikiwa kupitia mikutano miwili ya Tume iliyofanyika



ambapo rufaa 225 ziliamuliwa na malalamiko 67 yalishughulikiwa;

(iii) Elimu kwa wadau kuhusu majukumu ya Tume na Utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma iliitolewa kwa Taasisi za umma 11.

(iv) Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 iliandaliwa na kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(v) Watumishi wa Tume wamejengewa uwezo ambapo watumishi 17 wamepata mafunzo ya muda mrefu na watumishi 100 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika maeneo ya OPRAS, uadilifu, mapambano dhidi ya rushwa, VVU na UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa (MSY) mahali pa kazi. Aidha, watumishi 92 walipatiwa mafunzo ya stadi za uchambuzi wa rufaa na ukaguzi wa Rasilimaliwatu.

#### **BODI YA MISHAHARA NA MASILAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

**47. Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma ilikuwa na jukumu la kufanya mapitio ya mara kwa mara na kupendekeza viwango vya mishahara na masilahi mengine; na kuzishauri mamlaka kuhusu misingi ya miundo ya mishahara katika Utumishi wa Umma.

**48. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 9: Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma lilitengewa **Shilingi 1,445,945,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2021 **Shilingi 1,018,260,288.34** zilipokelewa na kutumika kulipa mishahara na kutekeleza majukumu ya msingi ya Bodi.

**49. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi, 2021, Bodi imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Utafiti umefanyika kuhusu utekelezaji wa Mfumo wa Jumla wa Kimenejimenti wa Motisha katika Utumishi wa Umma.

Utafiti huo uliwezesha kuandaliwa kwa rasimu ya *Taarifa ya Mfumo wa Jumla wa Kimenejimenti wa Utoaji wa Motisha katika Utumishi wa Umma (Total Rewards Management System in the Public Service)* ambayo imewasilishwa kwa wadau Serikalini;

(ii) Utafiti wa awamu ya kwanza kuhusu mazingira magumu ya kazi, hususan kwa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ulifanyika ambapo taarifa za utafiti zilikusanywa kutoka Mikoa 14, Halmashauri za Manispaa 5, Miji 4 na Wilaya 55. Aidha, katika awamu ya pili, taarifa zitakusanywa katika Mikoa 12, Halmashauri 57 (zikiwemo Halmashauri za Manispaa 1 na Wilaya 56) kuanzia mwishoni mwa Mwezi Machi hadi Aprili, 2021. Taarifa ya utafiti kwa awamu zote yenye mapendekezo itawasilishwa kwa mamlaka;

(iii) Taarifa za gharama za maisha ziliandaliwa kwa kila robo mwaka. Uchambuzi wa takwimu za kiuchumi kwa kuzingatia taarifa za NBS na vigezo vya kimataifa ulifanyika ili kuandaa taarifa ya gharama za chini za maisha; na

(iv) Mwongozo wa pamoja wa kuzingatiwa katika utoaji wa Masilahi na Posho katika Utumishi wa Umma umeandaliwa na Mwongozo huo umewasilishwa Serikalini kwa ajili ya hatua zinazofuata.

**50. Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma shughuli zake zimehamishiwa Fungu 32 kama mojawapo ya Idara kuanzia mwaka ujao wa Fedha baada ya Bodi hiyo kufutwa.

## **OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA**

**51. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya mwaka 2002, Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa ina jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma. Aidha, jukumu jingine ni kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004

kwa kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

**52. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 4: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, iliidhiniwa jumla ya **Shilingi 4,564,368,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,564,368,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,000,000,000** kwa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Marchi, 2021, **Shilingi 1,882,782,000.00** zilipokelewa na kutumika.

**53. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Idara ya Kumbukumbu imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya Nchi yetu kutoka taasisi za Umma na watu binafsi zimekusanywa na kuchambuliwa kwa lengo la kutunza historia ya nchi yetu. Katika kutekeleza jukumu hili, majalada 551 ya nyaraka yalikusanywa kutoka Halmashauri za Wilaya ya Muheza (144), Monduli (192) na Karatu (215). Vile vile, nyaraka 399 zinazomhusu Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin William Mkapa, zimetambuliwa na kukusanywa. Aidha, nyaraka zinazomhusu Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati akisoma Shule ya Msingi Chato, zilitambuliwa na kuwekwa katika hifadhi salama katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato;

(ii) Utambuaji, ukusanyaji, utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa umeendelea kufanyika ambapo nyaraka 327 za Waasisi wa Taifa (Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Adeid Amani Karume) zimechambuliwa na kukusanywa kutoka maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuhifadhi historia ya Waasisi wa Taifa letu;

(iii) Vituo vya Kanda vimeendelea kuimarishwa kwa lengo la kuongeza uwezo wa Idara katika ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka. Uboreshaji huo ulihusisha ununuzi

wa mashubaka (shelves) mapya ya kuhifadhia nyaraka na kufungwa katika Kituo cha Kumbukumbu cha Kanda ya Ziwa – Mwanza, hivyo kuwezesha Kituo kupokea majalada ya mashauri yaliyofungwa kutoka Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza, kumbukumbu tuli toka Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Ofisi ya Katibu Tawala Wilaya ya Bukoba, Simiyu na Bariadi. Vile vile, ununuzi wa vitendea kazi likiwemo lori la tani kumi kwa ajili ya kusafirishia nyaraka ulifanyika;

(iv)Ukarabati wa nyaraka zilizohifadhiwa katika Ghala Kuu la Nyaraka umefanyika ambapo nyaraka kongwe 230 zimefanyiwa ukarabati zikiwemo District books (5), Regional books (2), Hansard (20), Gazeti la Serikali (10) na nyaraka za utawala wa Mwingereza (193);

(v) Mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma 36 iliuhishwa ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini. Mifumo hiyo ni Mfumo wa Utunzaji Kumbukumbu za Kiutendaji (Keyword filing system) ambao umewekwa katika taasisi za umma 31 na Mfumo wa Masijala Mtandao (eFile Management System) ambao umewekwa katika taasisi za umma tano (5);

(vi) Uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka katika mifumo ya kielektroniki ulifanyika ili kuweza kudumu kwa muda mrefu, kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi ambapo majalada 1,516 yameingizwa kwenye mfumo na mengine 154 yanaendelea kushughulikiwa ili yainginzwe kwenye mfumo;

(vii) Taasisi za Umma mbili zimewezeshwa kuandaa miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu. Aidha, tathmini ya kumbukumbu tuli katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma ilifanyika ambapo majalada 220 kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Rungwe na Pangani yalihakikiwa. Vile vile, tathmini ilifanyika katika kituo cha Dar es Salaam ambapo majalada 1,365 ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii yalihakikiwa. Pia, majalada 2,886 ya Ofisi ya Makamu wa Rais na 483 ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, yaliyokuwepo katika

kituo cha Dar es Salaam yalihakikiwa na kuhamishiwa katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma;

(viii) Tathmini ya hali ya utunzaji kumbukumbu katika Taasisi za Umma 64 imefanyika ili kuhakiki uzingatiaji wa sheria na taratibu za utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka;

(ix) Taasisi za Umma zimejengewa uwezo katika usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali ambapo Maafisa na wasaidizi wa utunzaji kumbukumbu wa ndani ya idara walijengewa uwezo kupitia kikao kazi. Aidha, mikutano kazi kwenye Taasisi 40 zilizowekewa mifumo ya utunzaji kumbukumbu ya Masijala Mtandao (*e-file management system*) na Mfumo wa Utunzaji wa Kumbukumbu za Kiutendaji (*Keyword file management system*) ilifanyika kwa lengo la kuimarisha uwezo wa watumishi; na

(x)Elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutunza kumbukumbu imetolewa kupitia njia mbalimbali ikiwemo kipindi kimoja cha televisheni ya Taifa (TBC) na mitandao ya kijamii.

## **MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2021/22 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA**

**54. Mheshimiwa Spika**, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 umeandaliwa kwa kuzingatia, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa kuzindua Bunge la 12 pamoja na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), unaotaka Tanzania iwe na Uchumi Shindani na Viwanda kwa maendeleo ya watu. Shughuli zitakazotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:-

### **OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE**

#### **A. OFISI YA RAIS – IKULU**

**55. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa huduma kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;
- (ii) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ratiba ya kila siku;
- (iii) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;
- (iv) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;
- (v) Kuandaa mikutano miwili ya tathmini wa mwaka kati ya Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na wadau wengine;
- (vi) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara;
- (vii) Kuchambua na kutoa ushauri kwa Katibu Mkuu Kiongozi katika masuala ya kiuchumi, kijamii, kisheria, kiulinzi na kiusalama, kimataifa na masuala mengine yote yanayowasilishwa;
- (viii) Kusimika Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Mapambano Dhidi ya Rushwa pamoja na za Utekelezaji wa Programu za Maboresho katika Sekta ya Umma nchini;
- (ix) Kufanya mafunzo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu na Programu za Maboresho katika ngazi za Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa;

(x) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi;

(xi) Kuandaa na Kutekeleza Mkakati mpya wa Taifa wa Mapambano Dhidi ya Rushwa;

(xii) Kuratibu na kuendesha mikutano sita ya uratibu wa Maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa programu za Maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa Maboresho katika Sekta ya Umma nchini;

(xiii) Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu na kukamilisha mfumo wa kielektroniki wa Ufuatiliaji na tathmini wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III);

(xiv) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa 300 na malalamiko 400 ya watumishi wa umma na wananchi;

(xv) Kuendesha mikutano mitatu ya Watendaji na Maafisa wa Serikali kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Katibu Mkuu Kiongozi;

(xvi) Kufanya ziara ya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa sheria na maelekezo yanayotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi na Mkuu wa Utumishi wa Umma yanayohusu masuala ya Usimamizi wa utawala wa Utumishi kwenye Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xvii) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Programu ya Kujenga Uwezo wa Taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT);

(xviii) Kuendelea na uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino; na

(xix) Kukarabati majengo ya Ikulu ya Dar es salaam na Ikulu Ndogo za Mwanza, Arusha, Lushoto, Tabora na Shinyanga na nyumba za wafanyakazi zilizopo Dodoma.

**B. TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)**

**56. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, TAKUKURU imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza;

(ii) Kuendesha kesi 655 zinazoendelea na kesi mpya zitakazofunguliwa Mahakamani;

(iii) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007;

(iv) Kufanya utafiti kuhusu mianya ya rushwa katika sekta za umma na binafsi;

(v) Kufanya uchambuzi wa mifumo katika sekta na idara mbalimbali katika ngazi ya mikoa na wilaya;

(vi) Kuweka mikakati kwa kushirikiana na wadau ili kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati hiyo;

(vii) Kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

(viii) Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa TAKUKURU ili kujenga uwezo na uelewa kuhusu rushwa, ufiada na juhudi za Serikali katika kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kuyashawishi makundi haya kuunga mkono na kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini;

(ix) Kutumia njia za mawasiliano za kimkakati kulifikia kundi la vijana ili washiriki katika shughuli zinazowajenga kimaadili na



kushiriki kupambana na rushwa ili kuwa na jamii inayochukia rushwa;

(x) Kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kubeba agenda ya mapambano dhidi ya rushwa ili kuushirikisha umma katika mapambano hayo;

(xi) Kujenga majengo ya ofisi za TAKUKURU katika mkoa na wilaya;

(xii) Kujenga karakana kwa ajili ya kutengeneza magari ya taasisi ili kupunguza gharama za uendeshaji zinazotumika katika kutengeneza magari hayo;

(xiii) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika taasisi ili kurahisisha na kuwezesha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za wilaya, mkoa na makao makuu; na

(xiv) Kutoa mafunzo ya weledi kwa watumishi ili kuongeza ufanisi.

## C. TAASISI YA UONGOZI

**57. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Taasisi ya UONGOZI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi katika maeneo ya kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine na kuimarisha sifa binafsi za kiongozi;

(ii) Kutoa mafunzo ya Cheti ya Uongozi kwa njia ya mtandao kwa Viongozi 50;

(iii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 24 kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi 735 katika maeneo ya Uongozi na Maendeleo Endelevu, kutokana na mahitaji na maombi ya walengwa;

(iv) Kuandaa mikutano minne ya kimataifa katika masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu ambapo Viongozi 260 wanategemewa kushiriki;

(v) Kuandaa vipindi sita vya runinga vitakavyoshirikisha viongozi waandamizi na wataalam mbalimbali ndani na nje ya nchi, juu ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Vipindi hivi vitarushwa kwenye runinga, tovuti na mitandao ya kijamii na kuonekana katika Bara zima la Afrika;

(vi) Kufanya utafiti kwenye maeneo manne kuhusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu; na

(vii) Kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo yanayohusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu pale utakapohitajika.

#### **D. MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)**

**58. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, MKURABITA imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kuanzisha vituo Jumuishi saba vya urasimishaji na uendelezaji biashara ili kuwawezesha wafanyabishara kupata huduma muhimu sehemu moja katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Sumbawanga, Moshi, Bukoba, Kibaha, Tarime, Mafinga Mji na Shinyanga. Aidha, mafunzo ya kurasimisha na kuendesha biashara yatatolewa kwa wafanyabishara 7,000 kwa lengo la kuwawezesha kusajili biashara zao;

(ii) Kuanzisha vituo Jumuishi viwili vya urasimishaji wa biashara Zanzibar, katika Wilaya ya Kusini, Unguja na Chakechake, Pemba ili kuwawezesha wafanyabiashara kupata huduma muhimu sehemu moja ambapo wafanyabiashara 300 watapata mafunzo na kusajili biashara zao;

(iii) Kutoa mafunzo kuhusu fursa na matumizi bora ya Hati za Haki Milki za Kimila kwa wakulima 2,000 wa mazao ya miwa na chai waliorasimisha ardhi zao katika Halmashauri za Wilaya

tatu za Chamwino, Kilolo na Kilosa. Aidha, kwa upande wa Zanzibar mafunzo yatatolewa kwa wamiliki 2,000 wa ardhi katika Wilaya za Kusini, Magharibi B, Mkoani na Chakechake;

(iv) Kukamilisha urasimishaji wa ardhi mjini katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Miji ya Mufindi, Kigoma, Singida, Kahama, Ilala, Dodoma, Morogoro, Tunduma, Babati, Chamwino, Arusha, Njombe, Makete na Makambako kwa Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar, urasimishaji wa ardhi mjini utafanyika Wilaya ya Micheweni na Wete. Jumla ya Hati Miliki 20,000 zitaandaliwa na kutolewa;

(v) Kukamilisha Kukamilisha uandaaji na utoaji Hati za Haki milki za Kimila 6,500 kwa wananchi katika Halmashauri za Wilaya za Nyang'wale, Makete, Bahi, Bukoba Vijijini, Lindi na Newala za Tanzania Bara. Aidha, kwa upande wa Zanzibar Hati Milki 2,000 zitatolewa katika maeneo ya Micheweni, Kusini Unguja na Wilaya ya Kati;

(vi) Kukamilisha ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji katika Halmashauri za Wilaya 11 za Mbarali (Kijiji kimoja), Moshi (Kijiji kimoja), Nachingwea (Vijiji viwili), Mvomero (Kijiji kimoja), Kibiti (Kijiji kimoja), Itigi (Kijiji kimoja), Masasi (Vijiji Viwili), Makete (Vijiji viwili), Sumbawanga (Kijiji kimoja), Kalambo (Kijiji kimoja) na Mbinga (Kijiji kimoja);

(vii) Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa shughuli za Urasimishaji ardhi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Kibiti, Rufiji, Mbarali, Iringa, Mwanza, Kahama, Arusha na Wilaya za Mjini, Kaskazini A, Wete na Chakechake kwa upande wa Zanzibar;

(viii) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya maboresho ya sheria za ardhi na biashara katika Wizara za Kisekta;

(ix) Kuandaa vipindi 48 vya redio na runinga kuhusu utekelezaji wa Shughuli za urasimishaji Tanzania Bara na Zanzibar; na

(x) Kurasimisha wachimbaji wadogo 1,000 wa madini katika Mkoa wa Geita.

## E. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

**59. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, TASAF imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kufanya zoezi la kutambua hali za ustawi wa maisha ya Kaya za Walengwa wa Mpango zipatazo 886,724 iwapo zimeimarika kiuchumi kwa kutumia vigezo vya umaskini na utaratibu uliokubaliwa kitakwimu. Vile vile kutambua na kuandikisha Kaya 455,726 kutoka katika Vijiji/Mitaa/Shehia ambazo hazikufikiwa katika Kipindi cha Kwanza cha Mpango;

(ii) Kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini 1,146,723 zilizokidhi vigezo vya kuingia katika kipindi cha Pili cha Mpango;

(iii) Kutekeleza Miradi ya Jamii 2,578 iliyoibuliwa na wananchi ya Kutoa Ajira ya Muda kwa Kaya za Walengwa kutoka maeneo ya utekelezaji 51. Miradi hiyo itatoa Ajira za muda kwa Kaya za Walengwa 176,516. Vilevile kutafanyika maandalizi ya miradi ya kutoa Ajira za Muda 6,218 kutoka Halmashauri 123;

(iv) Kuwezesha jamii kutekeleza miradi ya kuendeleza Miundombinu ya huduma za jamii katika sekta ya Elimu, Afya, Maji, Mazingira, Barabara Vijijini na miradi ya ujasiriamali. Jumla ya miradi 495 itatekelezwa katika Vijiji na Mitaa ya Halmashauri 33 za mikoa mitano ya Arusha, Njombe, Simiyu, Geita na Mwanza;

(v) Kuwezesha uundaji wa Vikundi vya Kuweka Akiba , Kukupeshana na kuwekeza katika maeneo ya utekelezaji 52. Jumla ya vikundi 10,000 vya jamii vya kuweka akiba, kukupeshana na kuwekeza vyenye wanachama takribani 150,000 vitaundwa katika hamashauri 34. Aidha, Walengwa 50,000 kutoka Halmashauri 18 waliokamilisha Mipango yao ya biashara inayokidhi vigezo vilivyowekwa watapatiwa ruzuku ya uzalishaji mali ili kutekeleza mawazo ya biashara zao;

(vi) Kuongeza Maeneo ya Utekelezaji 99 yatakayoshiriki malipo kwa njia ya Kieletroniki kwa kutumia Benki na Mitandao ya Simu na hivyo kukamilisha Halmashauri zote 186 nchini;

(vii) Kuendelea kuimarisha Mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa Kumbukumbu za Walengwa, uendeshaji na utoaji wa taarifa ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mpango hususan kuimarisha mawasiliano Kati ya Maeneo ya utekelezaji na TASAF Makao Makuu Dodoma;

(viii) Kuimarisha Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli za Mpango pamoja na matumizi ya rasilimali ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika Ngazi zote za utekelezaji wa Mpango; na

(ix) Kufanya Mapitio ya pamoja baina ya Timu ya Serkali na Wadau wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mpango.

## **F. WAKALA YA NDEGE ZA SERIKALI**

**60. Mheshimiwa Spika**,katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Wakala ya Ndege za Serikali imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa viongozi wakuu wa kitaifa;

(ii) Kusimamia mikataba ya ukodishaji wa ndege kwa Kampuni ya Ndege ya Taifa (ATCL);

(iii) Kufanya matengenezo makubwa ya ndege zinazowahudumia viongozi wakuu wa kitaifa na ununuzi wa vipuri vya ndege za Serikali;

(iv) Kufanya ukarabati wa karakana ya Ndege za Serikali iliyopo Dar es salaam na kuanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa karakana mpya inayotarajiwa kujengwa Mjini Dodoma;

(v) Kulipia gharama za bima za ndege;

(vi) Kugharamia uendeshaji wa Ofisi na kulipia gharama za mafuta ya ndege; na

(vii) Kutoa mafunzo kwa wanahewa yanayohusu uhuishaji wa leseni zao.

**61. Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2021/22, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba kiasi cha **Shilingi 24,577,764,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba kiasi cha **Shilingi 639,780,318,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 467,921,917,000** Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 171,858,401,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

**62. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupokea Matamko ya Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na Madeni yanayopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(ii) Kupokea na kushughulikia malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa maadili kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(iii) Kuchunguza tuhuma za ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma;

(iv) Kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 2,000;

(v) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;

(vi) Kutoa elimu kwa Viongozi wa Umma na wananchi kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Hati ya Ahadi ya Uadilifu;

(vii) Kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti na kuiwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(viii) Kuanzisha na kuendeleza Klabu za Maadili katika shule na vyuo nchini; na

(ix) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Makao Makuu na ile ya Kanda ya Kati Jijini Dodoma.

**63. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22, Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 9,216,921,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 7,366,921,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,850,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## **OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE**

### **A. MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (MUU)**

**64. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Fungu 32, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa.

Aidha, Ofisi itahakikisha inasimamia Utawala wa Utumishi wa Umma, mikataba ya utendaji kazi Serikalini, Orodha ya Mishahara katika Utumishi wa Umma na Maadili ya watumishi wa Umma. Pia, itahakikisha Mipango na uendelezaji rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma inafanyika kwa ubora zaidi. Kwa kuzingatia pia kuwa Serikali imeingia awamu nyingine, Ofisi itaandaa na kusimamia miundo, mifumo ya utendaji kazi na uboreshaji wa utoaji huduma wa Utumishi wa Umma pamoja na kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji

na uwazi. Ofisi pia, itasimamia utendaji kazi na uendelezaji wa rasilimaliwatu katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa nafasi yake kama wizara mama, Ofisi itasimamia taasisi, programu na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**65. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuwezesha Taasisi za Umma 50 kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu, Mipango ya Urithishanaji Madaraka na Mipango ya Mafunzo ili kujenga misingi ya utekelezaji wa usimamizi wa Rasilimaliwatu utakaohakikisha kuwa wanakuwepo watumishi wa umma wenye sifa stahiki na weledi katika nafasi zote kwenye utumishi wa umma (Meritocracy) katika muda wa kati na muda mrefu;

(ii) Kuziwezesha taasisi za umma kuandaa mipango ya rasilimaliwatu yenye ubora unaotakiwa kwa kuzipatia Mwongozo utakaoandaliwa wa Mfumo wa Kielektroniki wa uandaaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu katika utumishi wa umma. Pia, Mwongozo wa Kitaifa wa kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma utaandaliwa;

(iii) Kuratibu upatikanaji wa fursa za mafunzo zitolewazo na washirika wa maendeleo kwa ajili ya kuwajengea uwezo na ustadi watumishi wa Umma ndani na nje ya nchi;

(iv) Kuratibu utoaji wa mafunzo kwa Viongozi katika utumishi wa umma ili kuwajengea uwezo katika usimamizi na utoaji wa maamuzi ya kimkakati;

(v) Kusimamia Mikataba ya Ushirikiano wa Kimataifa na Kikanda ili kuhakikisha kuwa watumishi wa umma wanapata fursa za ajira katika taasisi ambazo Tanzania ni mshirika;

(vi) Kuratibu na kufuatilia ajira za wageni katika utumishi wa umma na miradi ya kimkakati ili kuhakikisha pia kuwa wazalendo wanapata fursa ya kujifunza kama waambata kwa wataalamu hao wa kigeni;



(vii) Kusimamia na kuwezesha Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kutekeleza majukumu yake;

(viii) Kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi wa Kielektroniki (e-OPRAS) katika Taasisi za Umma;

(ix) Kujenga uwezo wa Taasisi za Umma katika kutekeleza Mikataba ya Utendaji Kazi;

(x) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mifumo ya Utendaji ya OPRAS na Mikataba ya Utendaji Kazi ya Taasisi;

(xi) Kusimamia utekelezaji wa mfumo mpya wa HCMIS katika taasisi 600 za Serikali kwa kutoa huduma za usaidizi za TEHAMA;

(xii) Kusanifu na kujenga mifumo ya kielektroniki ya utoaji huduma za Utumishi (Utumishi/Watumishi Mtandao);

(xiii) Kuimarisha na kuboresha miundombinu ya TEHAMA kwa ajili ya kuwezesha utendaji kazi wa mifumo na watumiaji wa mifumo;

(xiv) Kuratibu ukaguzi wa usalama na ufanisi wa mifumo ya TEHAMA ya HCMIS, e-OPRAS, eHRP;

(xv) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa sheria na miongozo ya Serikali Mtandao katika taasisi 50 za Serikali;

(xvi) Kuhuisha Mkakati wa Taifa wa Serikali Mtandao na Mkakati wa Serikali wa Kujikinga na Majanga ya Mtandao;

(xvii) Kuratibu uanzishwaji wa Vituo vitatu (3) vya Huduma Jamii (One Stop Centres);

(xviii) Kuratibu utekelezaji wa mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania) eneo la Serikali Mtandao;

(xix) Kusimamia na kuwezesha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kutekeleza majukumu yake;

(xx) Kusimamia ajira za Watumishi wa Umma ambapo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 44,096 ambapo kada ya Elimu 10,297, Afya 11,215, Kilimo 1,383, Mifugo 1,250, Uvuvi 733, Jeshi la Polisi 1,782, Magereza 843, Jeshi la Zimamoto na Uhamiaji 512 na Hospitali za Mashirika ya Kidini na hiari 1,240.

Aidha, Serikali itaajiri watumishi 14,841 wa kada mbalimbali ikiwemo wahadhiri wa Vyuo Vikuu vyote vya Umma nchini pamoja na kada nyingine ambazo haziko kwenye sekta zilizoainishwa awali. Hata hivyo, watumishi 92,619 wa kada mbalimbali watapandishwa vyeo na watumishi 2,360 watabadilishwa kada katika utumishi kulingana na maelekezo yatakatolewa wakati huo;

(xxi) Kuchambua na kuhakiki madai ya malimbikizo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma 17,699 yenye thamani ya **Shilingi 37,474,809,031.55** na kuchukua hatua ipasavyo;

(xxii) Kukagua na kuidhinisha watumishi wapya wanaostahili kuingizwa katika Orodha ya Malipo ya Mishahara;

(xxiii) Kuendesha mafunzo ya namna ya kutumia Mfumo mpya wa HCMIS kwa maafisa Utumishi/Tawala na viongozi wa Taasisi za Umma;

(xxiv) Kuidhinisha taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya Mishahara katika utumishi wa umma;

(xxv) Kutoa vibali vya ajira mpya na mbadala ili kujaza nafasi stahiki kwenye Taasisi mbalimbali za Umma;

(xxvi) Kufanya uhakiki wa watumishi kwenye Taasisi za Umma ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma sambamba na kusafisha na kuboresha taarifa za kiutumishi na mishahara kupitia Mfumo wa HCMIS;

(xxvii) Kuwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma 20 kuandaa Orodha ya Kazi

na Maelezo ya Kazi ili kupata uwiano mzuri wa watumishi katika kutekeleza majukumu ya Taasisi husika;

(xxviii) Kuboresha michakato ya utoaji huduma na kuimarisha usimamizi wa Mifumo na Viwango vya utendaji kazi kwa kufanya ufuatiliaji pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam katika Taasisi za Serikali ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi;

(xxix) Kuandaa Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Kitaifa na kuwezesha utekelezaji wake;

(xxx) Kuandaa Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini Serikalini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ambao utaunganisha Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini iliyopo katika Taasisi zote za Umma;

(xxxi)Kufanya Tathmini ya kina ya Utendaji kazi wa Wakala za Serikali ili kubaini utekelezaji wa malengo ya dhana ya uanzishaji wa Wakala hizo katika Utumishi wa Umma;

(xxxii)Kuwezesha uandaaji na uhuishaji wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi katika Utumishi wa Umma;

(xxxiii) Kuwianisha na kuoanisha mishahara na mipango ya motisha katika Utumishi wa Umma;

(xxxiv)Kusimamia utawala wa utumishi wa umma kwa kushughulikia mahitaji ya vibali vya uhamisho, kushikizwa, kuazimwa na likizo bila malipo kwa watumishi na baina ya waajiri mbalimbali katika Utumishi wa Umma;

(xxxv) Kuimarisha uwepo wa viongozi wenye sifa stahiki, weledi na maono ya utumishi wa umma wenye kuzingatia dira ya maendeleo na mikakati mbali mbali ya kitaifa kwa kupokea na kushughulikia mapendekezo ya nafasi za uteuzi, mikataba ya ajira na vibali vya kukaimu nafasi za uongozi kadiri maombi hayo yatakavyokuwa yanawasilishwa na waajiri mbalimbali;

(xxxvi) Kuimarisha upatikanaji wa taarifa (Kanzidata) za Viongozi wa Serikali waliopo kwenye nafasi na wanaoonesha mwelekeo na uwezo wa kukidhi uteuzi katika nafasi za uongozi; ili kuwa na viongozi wenye kukidhi matarajio ya utumishi wa umma na watanzania;

(xxxvii) Kujenga uwezo wa Taasisi za Serikali katika kuandaa Sera za Kisekta zinazozingatia utafiti ili kuziwanisha na kuondoa migongano na urudufu wakati wa utekelezaji;

(xxxviii) Kufanya mapitio ya Sheria na Miongozo ya Kiutumishi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi pamoja na kutoa miongozo ya kuimarisha Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia nyaraka za kiutumishi;

(xxxix) Kufanya ufuatiliaji na kuhamasisha ujumuishwaji wa masuala ya Anuai za Jamii ili kuhakikisha makundi yote katika jamii yanapata huduma zinazozingatia usawa;

(x) Kukamilisha upatikanaji wa kiwanja katika eneo la Mtumba karibu na Mji wa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nyingine 600 ambazo zitakuwa na gharama nafuu zitakazojengwa katika awamu nne;

(xi) Kufanya uhamasishaji wa uzingatiaji wa maadili kupitia vyombo vya habari na kuelimisha watumishi wa Umma na waajiri kuhusu umuhimu wa kupunguza malalamiko ya wateja na kushughulikia ipasavyo malalamiko yanayowasilishwa;

(xii) Kujenga uelewa wa wadau kuhusu Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma zilizofanyiwa mapitio;

(xiii) Kufanya Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma;

(xiv) Kuimarisha mifumo na uwezo wa matumizi ya mfumo wa kushughulikia malalamiko ya watumishi kuhusu mambo

mbali mbali ikiwemo haki zao na ya wananchi kuhusu huduma za utumishi wa umma kwenye ngazi ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma.

(xv) Kufanya utafiti wa uzingatiaji wa maadili katika utumishi wa umma (*Public Service Integrity Survey*) kwa nia ya kubaini kiwango cha uzingatiaji wa maadili na kutoa ushauri wa uboreshaji unaozingatia taarifa sahihi za utafiti;

(xvi) Kufanya kampeni za uimarishaji wa uzingatiaji wa maadili kwenye taasisi za umma na vyama vya Kitaaluma;

(xvii) Kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu huduma zitolewazo na Ofisi na namna ya upatikanaji wake kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo magazeti, radio, runinga, tovuti, mitandao ya kijamii, Gazeti la Serikali, majarida, vipeperushi na vitabu, mikutano ya wadau na semina;

(xviii) Kuanza maandalizi ya ujenzi wa Klabu ya Viongozi katika Utumishi wa Umma (Leaders Club) kwenye eneo la Ndejengwa Hill top – Dodoma;

(xix) Kuendelea kutoa huduma kwa Viongozi wa Kitaifa Wastaafu (Viongozi 11 na wajane sita) kwa mujibu wa sheria.

## **B. CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA (TPSC)**

**66. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2021/22 Chuo cha Utumishi wa Umma kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya mitihani ya Utumishi wa Umma kwa watumishi 700 ili kuwajengea uwezo wa utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi;

(ii) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Maendeleo, Menejimenti na Usimamizi wa ofisi kwa watumishi wa umma 5,000 ili kuendeleza stadi, weledi na ujuzi katika maeneo hayo. Vile vile, yatatolewa mafunzo hayo kwa njia ya mtandao kwa watumishi wa umma 2,500;

(iii) Kutoa Mafunzo ya Awali katika Utumishi wa Umma kwa watumishi wa umma 2,600 ili kujenga uelewa wa kitendaji wa serikalini kwa waajiriwa wapya;

(iv) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 13,800 katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, na Menejimenti ya Rasilimali Watu, Usimamizi na Manunuzi ya Umma, Uongozi na Utawala Bora;

(v) Kutoa ushauri katika maeneo mbali mbali 6 ya kitaalam kwa Taasisi za Umma kwa ajili ya kutambua changamoto halisi za utendaji na kuchangia katika utoaji wa maamuziyanayozingatia matokeo ya utafiti;

(vi) Kufanya utafiti wa aina nne wa maeneo ya Utumishi wa Umma yanayolenga kuboresha utoaji huduma kwa wananchi;

(vii) Kuratibu midahalo kwa njia ya mtandao katika maeneo 32 kwa watumishi wa umma na sekta binafsi itakayowezesha kufanyika kwa midahalo kwa washiriki wa ndani na nje ya nchi wapatao 2,000 ili kupunguza gharama za Serikali kupeleka watumishi nje ya nchi na kubadilishana uzoefu wa kitaalam;

(viii) Kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 5 wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika ngazi za Shahada ya Uzamivu na Shahada ya Uzamili;

(ix) Kuendelea na ujenzi wa majengo yatakayotumika kwa ajili ya madarasa, maktaba na ofisi katika Kampasi za Singida, Tanga na Kanda ya Ziwa;

(x) Kufuatilia uhamishaji wa umiliki wa kiwanja na 46 kilichopo eneo la Shangani Mtwara ambacho Chuo kilipatiwa na Wakala ya Majengo (TBA) kwa ajili ya ujenzi wa mabweni;

(xi) Kufuatilia upatikanaji wa eneo la Chamwino – Dodoma na Mbeya kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi za Dodoma na Mbeya;

(xii) Kutoa mafunzo ya kuwajengea uelewa kuhusu Mkakati wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa, maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI pamoja na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa mahali pa kazi kwa watumishi 238;

### C. MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA)

**67. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2021/22, Mamlaka ya Serikali Mtandao imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuboresha Mfumo wa kurahisisha ubadilishanaji wa Taarifa Serikalini (***Government Enterprise Service Bus***);

(ii) Kuboresha Vituo maalum vya kuhifadhi Mifumo ya Serikali Kimtandao (***Government Private Cloud***);

(iii) Kuhuisha, kusimamia na kuendeleza Mifumo shirikishi ya TEHAMA ikiwemo Mfumo wa kutoa Huduma kwa Njia ya Simu za Mkononi; Mfumo wa Barua Pepe Serikalini (GMS), Ofisi Mtandao (e-office), Mfumo wa Kusimamia Rasilmali za Taasisi (ERMS), n.k.

(iv) Kuhakikisha kuwa mifumo ya serikali na miundombinu ya TEHAMA inafanya kazi na kutoa huduma kwa taasisi za umma na wananchi wakati wote kwa ufanisi na usalama wa mawasiliano;

(v) Kuiwezesha Mifumo ya TEHAMA ya kimkakati na ya kisekta kubadilishana taarifa kwa kutumia Viwango na Miongozo ya TEHAMA ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma;

(vi) Kusimamia, kuendesha na kuendeleza Miundombinu Shirikishi na Vituo vya Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya TEHAMA ya Serikali na Kujikinga na Majanga ili kuongeza Usalama wa Mifumo na taarifa za Serikali sambamba na kupunguza gharama;

(vii) Kutoa mafunzo ya Serikali Mtandao kwa Viongozi, Wasimamizi wa TEHAMA na watumiaji wa huduma za Serikali

Mtandao kwa Taasisi za Serikali ili kuongeza umiliki (ownership), uelewa wa Taasisi za Umma katika kutumia TEHAMA, kuongeza ufanisi wa kiutendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi;

(viii) Kutoa ushauri wa kitaalam na msaada wa kiufundi kwenye maeneo ya TEHAMA kwa taasisi za Serikali; na

(ix) Kutoa ushauri na kusimamia jitihada mbalimbali za matumizi ya TEHAMA Serikalini ikiwa ni pamoja na Miradi ya TEHAMA ili iweze kutoa matokeo yenye tija na inayozingatia viwango.

**68. Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2021/22, Fungu 32 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inaomba kiasi cha **Shilingi 41,117,235,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 33,467,235,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 7,650,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

**69. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kusimamia na kuendesha michakato ya ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;

(ii) Kushiriki kama wataalam waalikwa kwenye usaili unaoendeshwa na taasisi zinazotumia Sheria zilizokasimiwa kwa taasisi husika;

(iii) Kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira iliyopo Zanzibar ili kurahisisha michakato ya ajira kwa ajira za Muungano;

(iv) Kuimarisha utendaji kazi wa taasisi kwa kutumia TEHAMA;



(v) Kuboresha mifumo ya uendeshaji wa usaili kwa kutumia mbinu za kisasa, ikiwemo matumizi ya "psychometric test";

(vi) Kuhakiki vyeti vya waombaji kazi na kupata taarifa nyingine muhimu ili kupunguza kesi zinazotokana na kugushiwa kwa vyeti; na

(vii) Kutoa taarifa na elimu kwa Umma ili kukuza uelewa kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

**70. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22, Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 3,388,771,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

#### **OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

**71. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Tume imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: -

(i) Kufanya ukaguzi wa kawaida katika Taasisi za Umma 150 na Ukaguzi Maalum katika Taasisi za Umma 10 kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kufanya mikutano minne (4) ya kisheria ya Tume kujadili na kutolea uamuzi rufaa, malalamiko, taarifa za ukaguzi na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa;

(iii) Kuhuisha Miongozo ya Tume ya uzingatiaji wa masuala ya Ajira na Nidhamu na kuisambaza kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu;

(iv) Kuelimisha Taasisi za Umma na Watumishi wa Umma kuhusu majukumu ya Tume na utekelezaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma kupitia ziara za Makamishna, vikao vya kazi, vyombo vya habari, machapisho na tovuti;

(v) Kuandaa Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2020/21 na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(vi) Kutoa huduma kwa watumishi wa Tume wenye mahitaji maalum; na

(vii) Kutoa elimu kwa watumishi wa Tume kuhusu VVU, UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na Mapambano Dhidi ya Rushwa.

**72. Mheshimiwa Spika**, Ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2021/22, Fungu 94, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kutumia kiasi cha **Shilingi 5,300,834,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

#### **OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA**

**73. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itatekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kukusanya taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya Nchi yetu kutoka taasisi za Umma, watu na taasisi binafsi;

(ii) Kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa;

(iii) Kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini;

(iv) Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za taifa kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa ili kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi;

(v) Kufanya tathmini (appraisal) ya kumbukumbu tuli za Taasisi za Umma zilizohifadhiwa katika Kituo cha Taifa cha

Kumbukumbu Dodoma ili kubaini zenye umuhimu wa kuendelea kuhifadhiwa na zile ambazo umuhimu wake wa matumizi umefikia ukomo kwa lengo la kuziteketeza kwa mujibu wa Sheria;

(vi) Kujenga uwezo wa taasisi za umma katika usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kwa kuandaa mikutano kazi kwa menejimenti za taasisi za umma na mafunzo kazi kwa Waratibu na Watunza kumbukumbu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali;

(vii) Kufanya ukarabati wa nyaraka kongwe zilizohifadhiwa katika Ghala Kuu la nyaraka na zile zinazotarajiwa kukusanywa;

(viii) Kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu tuli kutoka katika Taasisi za Umma kwenda Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu - Dodoma;

(ix) Kuwezesha Taasisi za Umma kutengeneza Miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu;

(x) Kufanya Tathimini ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma;

(xi) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka katika maendeleo ya Taifa letu; na

(xii) Kuimarisha uwezo wa utendaji wa Watumishi wa Idara.

**74. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22, Fungu 4: Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 4,571,018,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 2,571,018,000**ni kwaajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## MAJUMUISHO

**75. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais ndiyo inayohusika na uwezeshaji wa maamuzi ya juu ya nchi, sambamba na menejimenti ya Utumishi wa Umma ambayo ni nguzo muhimu katika uendeshaji na uendelezaji wa nchi. Utumishi wa Umma umeendelea kutoa mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi ambayo sasa imefikia uchumi wa kipato cha kati. Tuna matarajio makubwa kuwa mchango wa watumishi wa umma utaendelea kuwezesha nchi kufikia uchumi wa kati wa kiwango cha juu. Aidha, maendeleo hayo yanatarajiwa kuongezeka kwa kuimarisha uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu kama inavyoshajiishwa katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III).

**76. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais itaendelea kuimarisha uwezeshaji wa vyombo vinavyosaidia kwenye maamuzi ya nchi, usalama na kuimarisha vita dhidi ya rushwa. Maadili kwa viongozi wote na watumishi wa umma yanatarajiwa kusimamiwa ipasavyo ili yachangie kwenye kuongeza tija ya rasilimaliwatu na rasilimalifedha ili kupata thamani ya fedha ya rasilimali hizo, kwa maendeleo ya watu. Kati ya mambo ambayo Serikali itayapa kipaumbele ni usimamizi thabiti wa maeneo hayo.

**77. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa ujumla inafanya maboresho ya kisekta na ya maeneo mbalimbali yaliyo mtambuka. Ofisi ya Rais ndio mratibu wa jumla wa maboresho yote katika Serikali. Hivyo, wajibu huo utatekelezwa kwa kuhakikisha kuwa maboresho yanayofanyika katika nchi yetu bila kuleta urudufu na yanaleta tija katika Utumishi wa Umma na kuchochea maendeleo. Aidha, Ofisi yangu itahakikisha kunakuwepo na utawala bora ulio imara kuanzia ngazi ya juu ya uongozi hadi chini. Katika kuimarisha uwazi Ofisi ya Rais itahakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu maamuzi ya Serikali.

**78. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza awali, tutaimarisha mifumo na uwezo wa matumizi ya mfumo wa kushughulikia malalamiko ya watumishi kuhusu mambo mbali mbali

ikiwemo haki zao na ya wananchi kuhusu huduma za utumishi wa umma kwenye ngazi zote ili kupunguza kwa kiwango kikubwa kero hizo. **Aidha, natoa rai kwa Maafisa Utumishi wote kushughulikia changamoto zote za watumishi haraka. Narudia kusisitiza kuwa tukitembelea kwa mwajiri yeyote tukakuta malalamiko yanayoweza kutatuliwa na mwajiri tutachukua hatua kali, ikiwemo kuwavua madaraka waliozembea. Pia, nawaomba wabunge kuleta kero na malalamiko ya watumishi wa umma kutoka katika majimbo yenu moja kwa moja kwangu wakati wowote. Nimedhamiria kupunguza kama sio kumaliza kabisa malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi yanayohusu Ofisi yangu.**

**79. Mheshimiwa Spika,** Kwa nchi yetu na kwa mujibu wa miundo na mgawanyo wa majukumu kwa mawaziri, utekelezaji kwa ujumla unajumuisha, Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

**80. Mheshimiwa Spika,** Mipango na Bajeti kwa Mafungu niliyoyataja bila kujumuisha Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma ambayo imefutwa yamezingatia vipaumbele vya Serikali kwenye eneo la kuimarisha utendaji kazi wa Utumishi wa Umma na kuifanya nchi yetu iondokane na matumizi mabaya ya rasilimali fedha, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na kupunguza urasimu usio wa lazima katika utoaji huduma na hivyo kuongeza tija katika kutekeleza masuala yenye masilahi mapana kwa Taifa letu.

**81. Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imelenga kuwa na Utumishi wa Umma unaotoa huduma bora kwa haraka na staha, kuzingatia Katiba, Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na taratibu ili kujenga imani zaidi kwa wananchi. Vile vile, Bajeti imelenga

kuweka mazingira bora ya ufanyaji biashara nchini ili kuendana na kauli mbiu ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Katika kuendana na wakati, jitihada zaidi zitawekwa kwenye kujenga uwezo na mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa TEHAMA ndani ya Serikali pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara Tanzania.

**82. Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 na Mipango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi yetu kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

**(i) Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu**

Matumizi ya Kawaida Sh. 24,557,764,000

**Jumla Sh. 24,557,764,000**

**(ii) Fungu 30: Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Matumizi ya Kawaida Sh. 467,921,917,000

Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 171,858,401,000

**Jumla Sh. 639,780,318,000**

**(iii) Fungu 33: Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Matumizi ya Kawaida Sh. 7,366,921,000

Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 1,850,000,000

**Jumla Sh. 9,216,921,000**

**(iv) Fungu 32: Ofisi ya Rais,  
Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

Matumizi ya Kawaida Sh. 33,467,235,000

Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 7,650,000,000

**Jumla Sh. 41,117,235,000**

(v) Fungu 67: Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma  
Matumizi ya Kawaida Sh. 3,388,771,000  
Jumla Sh. 3,388,771,000

(vi) Fungu 94: Ofisi ya Rais,  
Tume ya Utumishi wa Umma  
Matumizi ya Kawaida Sh. 5,300,834,000  
Jumla Sh. 5,300,834,000

(vii) Fungu 04: Ofisi ya Rais,  
Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa  
Matumizi ya Kawaida Sh. 2,571,018,000  
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 2,000,000,000  
Jumla Sh. 4,571,018,000

**83. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge**, Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais (Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka 2021/22, ni kama ifuatavyo:-

Jumla kuu - Matumizi ya  
Kawaida Sh. 544,574,460,000

Jumla kuu - Matumizi ya  
Miradi ya Maendeleo Sh. 183,358,401,000  
Jumla kuu kwa Mafungu yote Sh. 727,932,861,000

**84. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge**, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha. **"Ahsanteni sana kwa kunisikiliza" 85.**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Mohamed O. Mchengerwa (Mb.)  
**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS**  
**(MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NAUTAWALA BORA)**

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, ahsante sana kwa kuisoma hotuba yako vizuri, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Humphrey Polepole, karibu muda wako siyo zaidi ya nusu saa. *(Makofi)*

**MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ninaomba taarifa yote yenye zaidi ya ukurasa hamsini ingiie kwenye Taarifa ya *Hansard* pamoja na orodha ya Wajumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mtaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyogeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge.

Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kujadailiwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Noamba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi huo ulifanyika baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ili kuonesha mawanda ya uchambuzi, nilikumbushe Bunge lako kuwa Bajeti ya Ofisi ya



Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imewekewa makadirio katika mafungu nane yafuatayo; Fungu 20 - Ofisi ya Rais - Ikulu; Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Fungu 33 -Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Fungu 94 - Ofisi ya Rais,Tume ya Utumishi wa Umma na Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Spika, nitangulie kusema kuwa taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne ambayo ni matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ambayo ni; uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati kufanya ziara siku ziara kuanzi tarehe 11 hadi 14 Machi, 2021 kwa kukagua miradi iliyotengewa fedha katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ufafanunzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha na kukaguliwa katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitengewa kiasi cha shilingi 182,824,821,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mafungu manne kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri shilingi 168,219,571,000.

(ii) Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma shilingi 10,955,250,000.

(iii) Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma shilingi 1,850,000,000.

(iv) Fungu 04 - Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa shilingi 2,000,000,000

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati imebaini kwamba Mpango wa Ruzuku kwa Kaya maskini umesaidia kuboresha maisha ya wanufaika kwa kuwawezesha kumudu gharama mbalimbali za maisha; matumizi ya teknolojia ya mawasiliano yameongeza ufanisi katika kujifunza mambo mbalimbali ya utendaji na uendeshaji wa shughuli za Serikalini; Wakala wa Ndege za Serikali imekuwa ikipata fedha kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi jambo linaloathiri ufanisi na mafanikio ya kukidhi matarajio.

Mheshimiwa Spika, pia Wakala wa Ndege za Serikali inadaid taasisi mbalimbali za Serikali kiasi kikubwa cha fedha na haina mkakati maalumu wa kudai madeni hayo ya muda mrefu; Chuo cha Utumishi wa Umma kinahitaji kuboresha miundombinu muhimu inayohusika na mafunzo; na pamoja na kuwepo kwa Chuo cha Utumishi wa Umma, bado kuna waajiri katika utumishi wa umma, hawatekelezi wajibu wa kuwapeleka waajiriwa wavya kwenye mafunzo elekezi yanayotolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na utekelezaji wa bajeti kwa mafungu niliyoyataja awali, Kamati ilifanya uchambuzi wa mambo makuu mawili ambayo ni uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na utekelezaji wa bajeti ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu matokeo ya uchambuzi wa Kamati ili kupata ulinganisho utakaosaidia katika mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti

ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulilenga kulinganisha upatikanaji wa fedha na idhini ya Bunge kuhusu bajeti kwa kuzingatia malengo ya bajeti. Njia zilizotumiwa kufanya uchambuzi ni pamoja na kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati. Kwa namna hiyo, muhtasari wa matokeo yaliyobainika ni kama inavyoonekana katika katika Jedwali Na. 01.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa jumla ya kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia mwezi Februari, 2021 ni asilimia 68 ya bajeti iliyoidhinishwa ambao ni mwenendo unaoridhisha katika upatikanaji wa fedha; fedha za matumizi ya maendeleo zinatolewa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na fedha za matumizi ya kawaida ambapo fedha za maendeleo zilizopatikana ni asilimia 71.3 ya fedha ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo; fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ilitolewa kwa kiasi cha asilimia 66.8 na fedha zimekuwa zikitoka wa wakati na bila kuathiri utekelezaji wa malengo ya bajeti yaliyokusudiwa ya ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa jumla wa Kamati umebaini kwamba, mtiririko wa fedha kutoka Hazina ni mzuri ikilinganishwa na miaka mingine iliyopita. Kwa mfano, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida hadi kufikia mwezi Februari, 2020 ilikuwa ni asilimia 63.35 wakati kwa mwezi Februari, 2021 ilikuwa ni asilimia 66.8; upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo mwezi Februari, 2020 ulikuwa ni asilimia 44.85 wakati hadi kufikia mwezi Februari, 2021 ilikuwa ni asilimia 71.3.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika mambo kumi. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imezingatia kikamilifu baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati na inaendelea kuzingatia

sehemu ya maoni na ushauri. Mfano wa ushauri uliozingatiwa unahusu kuanza kwa ujenzi wa majengo ya Chuo cha Utumishi wa Umma eneo la Mungumaji – Singida. Kukamilika kwa majengo hayo kutasaidia kupunguza gharama za kukodi majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, mfano wa ushauri ambao unaendelea kuzingatiwa ni ule wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini - *TASAF* kuongeza wigo wa kutumia mfumo wa kielektroniki (mitandao ya simu na benki) kufanya malipo kwa wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, ambapo imefikia Halmashauri 39 ikilinganishwa na 16 zilizokuwa zimefikwa katika mwaka uliopita wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufanya uamuzi sahihi kuhusu hoja ya Serikali kuhusu kuidhinisha matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kamati imefanya uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2021. Naomba kutoa taarifa kuhusu matokeo ya uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, unajumuisha mafungu saba ambayo ni 04, 20, 30, 32, 33, 67 na 94 unalenga kuwezesha utekelezaji wa malengo 175 baadhi ya malengo hayo ni kama ilivyoainiswa kwenye kurasa wa 11 mpaka 16 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishwa jumla ya shilingi 727,932,861,600. Kati ya fedha hizo shilingi 544,574,460,600 sawa na asilimia 74.81 ya bajeti inayoombwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 183,358,401,000 sawa na asilimia 25.19 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida shilingi 36,452,420,000 sawa na asilimia 5.01 ya bajeti yote ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 508,122,040,600 sawa na asilimia 69.8 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti inayoombwa kuidhinishwa kwa mwaka ujao wa fedha imeongezeka kwa shilingi 27,976,541,600 sawa na asilimia 3.99 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo ilikuwa shilingi 699,956,320,000. Aidha, kwa upande wa matumizi ya kawaida katika mwaka ujao wa fedha kuna ongezeko la shilingi 27,442,961,600 sawa na asilimia 5.31 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi 517,131,499,000.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeendelea kubaini kwamba kiasi cha fedha za maendeleo kunachoombwa kimeongezeka kwa shilingi 533,580,000 sawa na asilimia 0.29 ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 ambacho kilikuwa shilingi 182,824,821,000.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mpango wa Maendeleo wa Taifa, kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ili kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika mwaka ujao wa fedha. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia chati.

Mheshimiwa Spika, mambo yafuatayo yalibainika kutokana na uchambuzi; Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni shilingi bilioni 727.93 ni sawa na asilimia 2.01 ya bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2021/2022 ni shilingi bilioni 36,258.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 3.9 ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; wakati Bajeti ya Ofisi ya

Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imeongezeka kwa asilimia 3.99 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021; na Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 2.76 katika fedha za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 36.68 ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022; wakati bajeti ya maendeleo ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambayo ni sawa na asilimia 2.01 ya Bajeti ya Taifa, imeongezeka kwa asilimia 0.29 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, aidha, matokeo ya ulinganisho wa bajeti ya Taifa dhidi ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yameoneshwa sawia kupitia Chati Na. 01 na Na. 02 kama zinavyoonyeshwa kwenye ukurasa wa 21 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Moja; Serikali iangalie namna ya kutatua changamoto ya upungufu wa watumishi hasa wa kada za ualimu, afya, uhandisi, maafisa ugani na maendeleo ya jamii ambao kwa sehemu kubwa umechangiwa na watumishi kustaafu, kufariki na baada ya kufanyika kwa zoezi la uhakiki wa watumishi.

Mbili; Kamati inatambua na kupongeza juhudi za Serikali katika kujenga uchumi, hatua ambayo imeiwezesha nchi yetu kuingia katika kundi la nchi zenye uchumi wa kati (*middle income countries*). Ni maoni ya Kamati kwamba baada ya mafanikio hayo, sasa ni wakati mwafaka kwa Serikali kuangalia uwezekano wa kuboresha zaidi maslahi ya watumishi ikiwa ni pamoja na kuwaongezea mishahara na motisha nyingine. (*Makofi*)

Tatu; Serikali ichukue hatua ili kudhibiti ucheleweshaji wa watumishi wa umma kupanda madaraja na kubadilishiwa mishahara, hali ambayo imesabababisha baadhi yao kustaafu bila ya kupata au kupunjwa stahiki na haki zao. *(Makofi)*

Nne, Serikali iboreshe zaidi utaratibu wa kuwahudumia wastaafu kwa kuhakikisha watumishi wastaafu wanapata huduma madhubuti, bora na kwa wakati ili kuwaondolea usumbufu unaoweza kujitokeza wakati wanafuatilia stahiki na maslahi yao baada ya kustaafu. *(Makofi)*

Tano; Kamati inatambua na kupongeza uamuzi wa Serikali wa kuiwezesha Wakala wa Ndege za Serikali kukarabati Hanga (karakana ya matengenezo ya ndege) iliyopo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere *(Terminal I)* jambo ambalo litaiwezesha kufanya ukarabati wa ndege zake zikiwa zimeegeshwa katika mazingira salama na hivyo kutoathirika na mvua wala jua. *(Makofi)*

Hivyo, basi Kamati inashauri Serikali kupeleka fedha za maendeleo kikamilifu kwa Wakala hiyo ili kuwezesha ukarabati huo kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sita, Serikali ihakikishe Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma zinawapeleka watumishi wake hasa wapya katika Chuo cha Utumishi wa Umma *(TPSC)* kwa lengo la kupata mafunzo kuhusiana na utumishi wa umma. Ni katika taasisi hii ndipo watumishi wa umma wapya wataweza kujifunza kuhusiana na maadili, utamaduni, miiko na desturi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, saba, Serikali ihakikishe inatoa fedha za maendeleo kwa Chuo cha Utumishi wa Umma *(TPSC)* ili kukiwezesha kuboresha miundombinu ya kufundishia kwa wakufunzi na kujifunzia kwa wanachuo na hivyo kuondoa usumbufu uliopo.

Mheshimiwa Spika, nane, Serikali ihakikishe viongozi wanaoteuliwa kushika nyadhifa za utumishi wa umma

wanapata uelewa wa kutosha kuhusu maadili ya viongozi wa umma kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao. Utaratibu huu utasaidia kuwakumbusha viongozi hao kuzingatia maadili ya kiutendaji, kujiepusha na mgongano wa kimaslahi na kutekeleza wajibu wao kwa kuzingatia kiapo cha ahadi ya uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tisa, Serikali iwezeshe Taasisi ya Uongozi kwa maana ya *(Uongozi Institute)* kuandaa mafunzo maalum *(tailor made trainings)* kwa makundi maalum ya viongozi kama vile Wabunge, Madiwani na kadhalika ili kuwaongezea viongozi hao ujuzi na hivyo kuwawezesha kutekeleza shughuli zao kwa weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumi, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiwezesha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufungua ofisi 28 za mikoa, Ofisi 111 za Wilaya na vituo maalumu sita ambazo zimewezesha taasisi hiyo kusogeza huduma zake karibu zaidi na wananchi. Hata hivyo, uendeshaji wa ofisi hizo unakumbana na changamoto ya upungufu wa watumishi 153, magari 189 na vitendea kazi vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumi na moja, Serikali iangalie uwezekano wa kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Na. 11 ya mwaka 2007, kwani imekaa muda mrefu na inahitaji kuboreshwa kulingana na mazingira ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumi na mbili, Serikali iitumie kikamilifu Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kuhuisha na kuoanisha ama kwa kiingereza *harmonize* mifumo ya Teknolojia ya Habari ya Mawasiliano (TEHAMA) inayotumiwa na Wizara na Taasisi za Serikali ili isomame kusomana ili kuwezesha ufanisi katika matumizi ya mifumo hiyo pamoja na kuhakikisha usalama wa taarifa za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumi na tatu, Serikali ihakikishe asilimia 30 ya kaya maskini zilizo nje ya mpango wa ruzuku



kwa kaya maskini unaotekelezwa na *TASAF* zinaingizwa katika utekelezaji wa sehemu ya pili ya awamu ya tatu ya mpango huo ili kutoa fursa kwa wananchi hao kuwezesha kujinusuru na umaskini. Jumla ya vijiji/mitaa/shehia 5,693 viliachwa nje ya mpango huo na hivyo kuwanyima wakazi wake fursa ya kunufaika.

Mheshimiwa Spika, kumi na nne, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa asilimia 89.23 ya mchango wake ambao inapaswa kuutoa katika mwaka huu wa fedha kuchangia utekelezaji wa mpango wa kaya maskini.

Mheshimiwa Spika, kumi na tano, Kamati inaipongeza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kuwezesha taasisi na idara zake kuzingatia masuala ya kijinsia katika utekelezaji wa shughuli zake. Mfano ni *TASAF* ambayo imekuwa ikizingatia masuala ya kijinsia katika utekelezaji wa miradi inayolenga kuwezesha kaya zinazonufaika na ruzuku kwa Kaya maskini kujiongezea kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumi na sita, Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa Ikulu ya Chamwino, Dodoma ambao unatekelezwa na Watanzania wenyewe. Ujenzi wa Ikulu hiyo ambayo ni alama ya nchi yetu, umeipa Serikali na nchi yetu heshima kubwa kutoka kwa wananchi na mataifa mengine. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, hitimisho; kwa niaba ya Kamati, Wajumbe wote, napenda kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa namna mnavyotekeleza majukumu yenu kwa umakini na weledi wa hali ya juu, ambavyo vimeliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao na namna ambavyo wamejitoa kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Katika kipindi hiki cha kushughulikia bajeti ya Ofisi ya

Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wajumbe walijitoa kikamilifu na kutekeleza majukumu ya uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu, bila kujali ufinyu wa muda uliotengwa ikilinganishwa na mafungu mengi yaliyo chini ya ofisi hii. Hali hiyo ni udhirisho tosha kwamba Wajumbe wa Kamati hii kama ilivyo kwa Wajumbe wa Kamati nyingine, wako tayari kulitumikia Bunge, Taifa na wananchi wakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa Wajumbe wa Kamati ningetamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao wako wote hapa. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mb), kwa kuteuliwa na Mheshimwa Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Deogratius John Ndejemi (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wakiongozwa na Makatibu Wakuu Dkt. Moses Kusiluka (Ikulu), Dkt. Laurean Ndumbaro (Utumishi) na Naibu Katibu Mkuu (Utumishi) Dkt. Francis Michael, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru kwa dhati kabisa Wakuu wa Taasisi, Idara na Vitengo vilivyopo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala

Bora, kwa ushirikiano wao na utekelezaji makini wa bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu yetu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara za Kamati Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge, Ndugu Gerald Magili, Makatibu wa Kamati, Ndugu Chacha Nyakega, Ndugu Eunice Shirima na Ndugu Rabisante Moshi wakisaidiwa na Ndugu Pauline Mavunde, kwa uratibu wao mzuri sana wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa kwa unyenyekevu mkubwa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI YA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa Taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyogeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kujadailiwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Noamba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uchambuzi huo ulifanyika baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuonesha mawanda ya uchambuzi, nilikumbushe Bunge lako kuwa, Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imewekewa makadirio katika Mafungu Nane (8) yafuatayo:-

i) **Fungu 20:** Ofisi ya Rais, Ikulu;

ii) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;

iii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

iv) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

v) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

vi) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na

vii) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, nitangulie kusema kuwa taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne (04) ambayo ni:-

i) Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo;

ii) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## **2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, katika ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulitokana na masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayotaka Kamati kufanya ziara siku zisizozidi saba zitumike kwa ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kamati ilizingatia masharti hayo kwa kufanya ziara tarehe 11 hadi 14 Machi, 2021 kwa kukagua miradi hiyo. Naomba kutoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi huo kama ifuatavyo:-

### **2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha na kukaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ilitengewa kiasi cha **Tsh 182,824,821,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mafungu manne (4) kama ifuatavyo:-

**i) Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri – **Tshs 168,219,571,000**

**ii) Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma – **Tsh.10,955,250,000**

**iii) Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma – **Tshs. 1,850,000,000**

**iv) Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa – **Tshs .2,000,000,000**

## 2.2 Yaliyobainika

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kwamba:

a) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umesaidia kuboresha maisha ya wanufaika kwa kuwawezesha kumudu gharama mbalimbali za maisha;

b) Matumizi ya tekonolojia ya mawasiliano yameongeza ufanisi katika kujifunza mambo mbalimbali ya utendaji na uendeshaji wa Shughuli za Serikalini;

c) Wakala wa Ndege za Serikali imekuwa ikipata fedha kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi jambo linaloathiri ufanisi na mafanikio ya kukidhi matarajio;

d) Wakala wa Ndege za Serikali inadai taasisi mbalimbali za Serikali kiasi kikubwa cha fedha na haina mkakati maalumu wa kudai madeni hayo ya muda mrefu;

e) Chuo cha Utumishi wa Umma kinahitaji kuboresha miundombinu muhimu inayohusika na mafunzo; na

f) Pamoja na kuwepo kwa Chuo cha Utumishi wa Umma, bado kuna waajiri katika utumishi wa umma, hawatekelezi wajibu wa kuwapeleka waajiriwa wapya kwenye mafunzo elekezi yanayotolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na utekelezaji wa bajeti kwa mafungu niliyoyataja awali, Kamati ilifanya uchambuzi wa mambo makuu mawili ambayo ni:

a) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021; na

b) Utekelezaji wa bajeti ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu matokeo ya uchambuzi wa Kamati ili kupata ulinganisho utakaosaidia katika mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

### 3.1 Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulilenga kulinganisha upatikanaji wa fedha na idhini ya Bunge kuhusu Bajeti kwa kuzingatia malengo ya bajeti. Njia zilizotumiwa kufanya uchambuzi ni pamoja na kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati. Kwa namna hiyo, muhtasari wa matokeo yaliyobainika ni kama inavyoonekana katika katika **Jedwali Na. 01**.

**Jedwali Na.01** Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha kilichopatikana

BAJETI ILIYOIDHINISHWA			UPATIKANAJI WA FEDHA HADI FEBRUARI		
Mchanganuo	Kiasi	%	Mchanganuo	Kiasi	%
<b>Jumla</b>	699,956,320,000	<b>100</b>	<b>Jumla</b>	476,004,282,503.75	<b>68.00</b>
<b>Kawaida</b>	517,131,499,000	<b>36</b>	<b>Kawaida</b>	345,593,812,338.84	<b>66.83</b>
<b>Maendeleo</b>	182,824,821,000	<b>64</b>	<b>Maendeleo</b>	130,410,470,170.30	<b>71.33</b>

**Chanzo:** Uchambuzi wa Randama zilizowasilishwa.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa:

a) Jumla ya kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia mwezi Februari, 2021 ni asilimia 68 ya bajeti iliyoidhinishwa, ambao ni mwenendo unaoridhisha katika upatikanaji wa fedha;

b) Fedha za matumizi ya maendeleo zinatolewa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na fedha za matumizi ya kawaida

ambapo fedha za maendeleo zilizopatikana ni asilimia 71.3 ya fedha ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo;

c) Fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ilitolewa kwa kiasi cha asilimia 66.8); na

d) Fedha zimekuwa zikitoka wa wakati na bila kuathiri utekelezaji wa malengo ya bajeti yaliyokusudiwa ya ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa ujumla wa Kamati umebaini kwamba, mtiririko wa fedha kutoka Hazina ni mzuri ikilinganishwa na miaka mingine iliyopita. Kwa mfano:

a) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida hadi kufikia mwezi Februari, 2020 ilikuwa ni asilimia 63.35 wakati kwa mwezi Februari, 2021 ilikuwa ni asilimia 66.8

b) Upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo mwezi Februari, 2020 ulikuwa ni asilimia 44.85 Wakati hadi kufikia mwezi Februari, 2021 ilikuwa ni asilimia 71.3.

### 3.2 Uchambuzi wa Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika mambo Kumi (10). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imezingatia kikamilifu baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati na inaendelea kuzingatia sehemu ya maoni na ushauri.

Mfano wa ushauri uliozingatiwa unahusu kuanza kwa ujenzi wa majengo ya Chuo cha Utumishi wa Umma eneo la Mungumaji – Singida. Kukamilika kwa majengo hayo kutasaidia kupunguza gharama za kukodi majengo.

Aidha, mfano wa ushauri ambao unaendelea kuzingatia ni ule wa TASAF kuongeza wigo wa kutumia mfumo wa kielektroniki (mitandao ya simu na benki) kufanya malipo kwa



wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, ambapo imefikia Halmashauri 39 ikilinganishwa na 16 zilizokuwa zimefikiwa katika mwaka uliopita wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ushauri ambao haukuzingatiwa kabisa, mfano wake ni ushauri kuhusu kutolewa kwa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo kwa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, ambapo huu ni mwaka wa nne (4) mfululizo haijawahi kupokea fedha yoyote ya maendeleo. Taarifa ilionesha kuwa hakuna kiasi cha fedha kilichotolewa kati ya **Shilingi 2,000,000,000** zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri uliotolewa, Kamati ina maoni kuwa bado kuna umuhimu wa kuendelea kuzingatia ushauri ambao haujafanyiwa kazi na hakuna sababu za msingi za kutouzingatia. Kwa mfano, ushauri kuhusu umuhimu wa Serikali kuongeza mshahara kwa watumishi wa umma unafaa kufanyiwa kazi inavyostahili.

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge lako tukufu kufanya uamuzi sahihi kuhusu hoja ya serikali kuhusu kuidhinisha matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kamati imefanya uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2021. Naomba kutoa taarifa kuhusu matokeo ya uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

#### **4.1 Uchambuzi wa makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, unajumuisha mafungu saba (7) (04, 20, 30, 32, 33, 67 na 94) na umeandaliwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

i) Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano Awamu ya Tatu (2021/22 - 2025/26);

ii) Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2020;

iii) Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022; pamoja na

iv) Maeneo muhimu ya kuzingatia kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Kwa ujumla Ofisi hii pamoja na mafungu yake imepanga kutekeleza malengo 175 kwa mwaka ujao wa fedha na baadhi ya malengo hayo ni haya yafuatayo:-

i) Kutoa huduma kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

ii) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya siasa, uchumi, jamii, sheria, diplomasia, mawasiliano na habari, uhusiano wa kikanda, kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

iii) Kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Programu ya Kujenga Uwezo wa Taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT);

iv) Kukarabati Majengo ya Ikulu ya Dar es Salaam na Ikulu ndogo za Mwanza, Arusha, Lushoto, Tabora na Shinyanga na nyumba za wafanyakazi zilizopo Dodoma;

v) Kuendelea na Uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino;

vi) Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu na kukamilisha mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III);

vii) Kufanya mafunzo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP) na programu za maboresho katika ngazi za Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa;

viii) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maafisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na waratibu wa shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara;

ix) Kuratibu na kuendesha mikutano sita ya uratibu wa maboresho kwa Makatibu Wakuu na waratibu wa Programu za maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa maboresho katika sekta ya umma nchini;

x) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;

xi) Kuandaa mkutano wa kimataifa na kikanda na mikutano saba ya kitaifa katika masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

xii) Kuendelea na urasimishaji wa Wachimbaji wadogo wa madini katika Mkoa wa Geita;

xiii) Kutekeleza miradi 2,390 ya Sekta ya afya, elimu, maji, ujasiriamali na barabara za vijiji chini ya mpango wa kutoa ajira za muda katika Halmashauri 42 pamoja na Unguja na Pemba;

xiv) Kufanya Mapitio ya pamoja baina ya Timu ya Serikali na wadau wa Maendeleo kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini;

xv) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa viongozi wakuu wa kitaifa;

xvi) Kusimamia mikakati ya ukodishaji wa ndege kwa kampuni ya Ndege ya Taifa (ATCL);

xvii) Kupokea matamko ya viongozi wa Umma kuhusu rasilimali na madeni yanayopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

xviii) Kufanya mapitio ya sheria na miongozo ya kiutumishi katika utumishi wa Umma kwa kwa lengo la kuboresha utendaji kazi;

xix) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitahani ya Utumishi wa Umma kwa Watumishi 1,115;

xx) Kuendesha mafunzo kwa njia ya mtandao ili kusaidia Serikali kupunguza gharama, kuwa na mazingira rafiki katika kujifunza, kutoa fursa ya kuepusha muingiliano wa mafunzo na majukumu ya kazi kupunguza safari nje ya mahali pa kazi na kuepuka kuwa mbali na familia;

xxi) Kusanikisha katika taasisi za umma, mfumo shirikishi wa kusimamia shughuli za Rasilimali za Taasisi;

xxii) Kuwezesha mifumo ya TEHAMA ya kimkakati na ya kisekta kubadilishana taarifa;

xxiii) Kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira iliyopo Zanzibar ili kurahisisha michakato ya ajira kwa ajira za Muungano;

xxiv) Kufanya mikutano ya Kisheria ya Tume ili kujadili na kutolea uamuzi rufaa na malalamiko, taarifa za ukaguzi na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa;

xxv) Kufanya utafiti kuhusu mazingira magumu ya kazi; na

xxvi) Kukusanya taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu kutoka taasisi za umma, taasisi na watu binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa

Umma na Utawala Bora, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 727,932,861,600**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 544,574,460,600/=** sawa na asilimia 74.81 ya bajeti inayoombwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 183,358,401,000** sawa na asilimia 25.19 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 36,452,420,000** sawa na asilimia 5.01 ya bajeti yote ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 508,122,040,600** sawa na asilimia 69.8 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti inayoombwa kuidhinishwa kwa mwaka ujao wa fedha imeongezeka kwa **Shilingi 27,976,541,600** sawa na asilimia 3.99 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo ilikuwa **Shilingi 699,956,320,000**.

Aidha, kwa upande wa matumizi ya kawaida katika mwaka ujao wa fedha kuna ongezeko la **Shilingi 27,442,961,600** sawa na asilimia 5.31 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa **Shilingi 517,131,499,000**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeendelea kubaini kwamba kiasi cha fedha za maendeleo kunachoombwa kimeongezeka kwa **Shilingi 533,580,000** sawa na asilimia 0.29 ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 ambacho kilikuwa **Shilingi 182,824,821,000**.

#### **4.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022**

**Mheshimwa Spika**, uchambuzi wa kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mpango wa Maendeleo wa Taifa, kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ulinganisho huo ulilenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika mwaka ujao wa fedha.

Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika:-

i) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni **Shilingi Bilioni 727.93** ni sawa na asilimia 2.01 ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2021/2022 ni **Shilingi Bilioni 36,258/=**.


ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 3.95 ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; wakati Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imeongezeka kwa asilimia 3.99 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021; na

iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 2.76 katika fedha za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 36.68 ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022; wakati bajeti ya maendeleo ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambayo ni sawa na asilimia 2.01 ya Bajeti ya Taifa, imeongezeka kwa asilimia 0.29 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021.


**Jedwali Na.02:** Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais (MUUB) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa Fedha 2021/2022

**Chanzo:** Uchambuzi wa randama zilizowasilishwa kwenye Kamati

Aidha, matokeo ya ulinganisho wa bajeti ya Taifa dhidi ya bajeti ya Ofisi ya Rais (MUUB), yameoneshwa sawia kupitia Chati Na.01 na Na.02 kama ifuatavyo:-



**Chati Na. 02 Bajeti ya OR - MUUB kwa ajili ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**



**Chanzo:** Uchambuzi wa Randama zilizowasilishwa.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa

mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

i) Serikali iangalie namna ya kutatua changamoto ya upungufu wa watumishi hasa wa kada za ualimu, afya, uhandisi, maafisa ugani na maendeleo ya jamii ambao kwa sehemu kubwa umechangiwa na watumishi kustaafu, kufariki na kukumbwa na zoezi la uhakiki wa watumishi;

ii) Kamati inatambua na kupongeza juhudi za Serikali katika kujenga uchumi, hatua ambayo imeiwezesha nchi yetu kuingia katika kundi la nchi zenye uchumi wa kati "middle income countries". Ni maoni ya Kamati kwamba baada ya mafanikio hayo, sasa ni wakati mwafaka kwa Serikali kuangalia uwezekano wa kuboresha zaidi maslahi ya watumishi ikiwa ni pamoja na kuwaongezea mishahara na motisha nyingine;

iii) Serikali ichukue hatua ili kudhibiti ucheleweshaji wa watumishi wa Umma kupanda madaraja na kubadilishiwa mishahara, hali ambayo imesababaisha baadhi yao kustaafu bila ya kupata au kupunjwa stahiki na haki zao;

iv) Serikali iboreshe zaidi utaratibu wa kuwahudumia wastaafu kwa kuhakikisha Watumishi Wastaafu wanapata huduma madhubuti, bora na kwa wakati ili kuwaondolea usumbufu unaoweza kujitokeza wakati wanafuatilia stahiki na maslahi yao baada ya kustaafu;

v) Kamati inatambua na kupongeza uamuzi wa Serikali wa kuiwezesha Wakala wa Ndege za Serikali kukarabati Hanga "Karakana ya Matengenezo ya Ndege" iliyopo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (Terminal I) jambo ambalo litaiwezesha kufanya ukarabati wa Ndege zake zikiwa zimeegeshwa katika mazingira salama na hivyo kutoathirika na mvua wala jua. Hivyo, basi Kamati inashauri Serikali kupeleka fedha za maendeleo kikamilifu kwa Wakala hiyo ili kuwezesha ukarabati huo kukamilika kwa wakati;



vi) Serikali ihakikishe Wizara na Taasisi zake ambazo zinadaiwa na Wakala wa Ndege za Serikali zinalipa madeni yake kwa wakati na ukamilifu ili kutokwamisha Wakala hiyo kutekeleza majukumu yake ya msingi;

vii) Serikali ihakikishe Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma zinawapeleka watumishi wake hasa wapya katika Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) kwa lengo la kupata mafunzo kuhusiana na utumishi wa umma. Ni katika taasisi hii ndipo watumishi wa umma wapya wataweza kujifunza kuhusiana na maadili, utamaduni, miiko na desturi katika utumishi wa Umma;

viii) Serikali ihakikishe inatoa fedha za maendeleo kwa Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) ili kukiwezesha kuboresha miundombimu ya kufundishia kwa Wakufunzi na kujifunzia kwa wanachuo na hivyo kuondoa usumbufu uliopo;

ix) Serikali ihakikishe viongozi wanaoteuliwa kushika nyadhifa za Utumishi wa Umma wanapata uelewa wa kutosha kuhusu maadili ya viongozi wa umma kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao. Utaratibu huu utasaidia kuwakumbusha viongozi hao kuzingatia maadili ya kiutendaji, kujiepusha na mgongano wa kimaslahi na kutekeleza wajibu wao kwa kuzingatia kiapo cha ahadi ya uadilifu;

x) Serikali iwezeshe Taasisi ya Uongozi (uongozi institute) kuandaa mafunzo maalum (tailor made trainings) kwa makundi maalum ya viongozi kama vile Wabunge, Madiwani n.k ili kuwaongezea viongozi hao ujuzi na hivyo kuwawezesha kutekeleza shughuli zao kwa weledi;

xi) Kamati inapongeza Serikali kwa kuiwezesha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufungua ofisi 28 za mikoa, 111 za Wilaya na vituo maalumu Sita (6) ambazo zimewezesha taasisi hiyo kusogeza huduma zake karibu zaidi na wananchi. Hata hivyo, uendeshaji wa ofisi hizo unakumbana na changamoto ya upungufu wa Watumishi 153, magari 189, na vitendea kazi vingine;

xii) Serikali iangalie uwezekano wa kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Na. 11 ya Mwaka 2007, kwani imekaa muda mrefu na inahitaji kuboreshwa kulingana na mazingira ya sasa;

xiii) Serikali iitumie kikamilifu Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kuhuisha na kuiwezesha "*harmonize*" mifumo ya Teknolojia ya Habari ya Mawasiliano (TEHAMA) inayotumiwa na Wizara na Taasisi za Serikali kusomana ili kuwezesha ufanisi katika matumizi ya mifumo hiyo pamoja na kuhakikisha usalama wa taarifa za Serikali;

xiv) Serikali ihakikishe asilimia 30 ya kaya maskini zilizo nje ya mpango wa ruzuku kwa kaya maskini unaotekelezwa na TASAF zinaingizwa katika utekelezaji wa sehemu ya pili ya awamu ya tatu ya mpango huo ili kutoa fursa kwa wananchi hao kuwezesha kujinusu na umaskini. Jumla ya Vijiji/Mitaa/Shehia 5,693 viliachwa nje ya mpango huo na hivyo kuwanyima wakazi wake fursa ya kunufaika;

xv) Serikali ihakikishe Maafisa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii, wanawaelimisha na kuwasimamia kikamilifu wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili kuhakikisha wanaelekeza sehemu ya ruzuku wanazopata kwenye shughuli za kiuchumi kwa kuanzisha miradi ili kuongeza kipato kitakachowasaidia kupunguza au kuondokana kabisa na umaskini;

xvi) Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa **asilimia 89.23** ya mchango wake ambao inapaswa kuutoa katika mwaka huu wa fedha kuchangia utekelezaji wa mpango wa kaya;

xvii) maskini unaotekelezwa na TASAF. Hadi mwezi Machi, 2021 Serikali ilikuwa imechangia **shilingi bilioni 3.15** kati ya **shilingi bilioni 3.5** inazopaswa kuchangia.

Aidha, Kamati inashauri Serikali kupunguza madeni ya miaka ya nyuma ili kuwezesha utekelezaji sawia wa mpango huo.

Tangu kuanza kutekelezwa kwa mpango huu mwaka wa fedha 2013/2014 hadi taarifa hii inaandaliwa deni la Serikali ni **shilingi bilioni 61.53. Jedwal.Na 03** linatoa ufafanuzi kuhusu mchango wa Serikali na kiasi ilichotoa hadi Machi, 2021.

Na.	Mwakawa Fecha	Bajeti iliyochinishwa (Tsh. Bilioni)	Kiasi kilichotolewa (Tsh. Bilioni)	Bakaa (Tsh. Bilioni)
1.	2013/2014	18.50	3.00	15.50
2.	2014/2015	14.00	0.00	14.00
3.	2015/2016	14.00	0.60	13.40
4.	2016/2017	14.00	0	14.00
5.	2017/2018	3.00	0.75	2.25
6.	2018/2019	3.00	3.00	0
7.	2019/2020	3.51	1.51	2.00
8.	2020/2021	3.51	3.14	0.38
<b>JUMA</b>		<b>73.53</b>	<b>11.99</b>	<b>61.53</b>

**Chanzo:** Uchambuzi wa randama zilizowasilishwa kwenye Kamati

xviii) Kamati inapongeza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kuwezesha taasisi na idara zake kuzingatia masuala ya kijinsia katika utekelezaji wa shughuli zake. Mfano ni TASAF ambayo imekuwa ikizingatia masuala ya kijinsia katika utekelezaji wa miradi inayolenga kuwezesha kaya zinazonufaika na ruzuku kwa Kaya maskini kujiongezea kipato; na

xix) Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa Ikulu ya Chamwino, Dodoma ambao unatekelezwa na Watanzania wenyewe. Ujenzi wa Ikulu hiyo ambayo ni alama ya nchi yetu, umeipa Serikali na nchi yetu heshima kubwa kutoka kwa wananchi na mataifa mengine.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimwa Spika**, kwa niaba ya Kamati napenda kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa namna mnavyotekeleza majukumu yenu kwa umakini na weledi wa

hali ya juu, ambavyo vimeliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao na namna ambavyo wamejitoa kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Katika kipindi hiki cha kushughulikia bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wajumbe walijitoa kikamilifu na kutekeleza majukumu ya uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu, bila kujali ufinyu wa muda uliotengwa ikilinganishwa na mafungu mengi yaliyo chini ya ofisi hii. Hali hiyo ni udhihirisho tosha kwamba, Wajumbe wa Kamati hii kama ilivyo kwa Wajumbe wa Kamati nyingine, wako tayari kulitumikia Bunge, Taifa na Wananchi wakati wowote.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa Wajumbe wa Kamati ningetamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Humphrey Hesron Polepole, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mwantum Mzamili Zodo, Mb
4. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb
5. Mhe. Dkt. Theo Medard Ntara, Mb
6. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb
7. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb
8. Mhe. Rehema Juma Migila, Mb
9. Mhe. Dkt Alice Karungi Kajjange, Mb
10. Mhe. Amandus Julius Chinguile, Mb
11. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
12. Mhe. Michael Constantino Mwakamo, Mb
13. Mhe. Dennis Lazaro Londo, Mb
14. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb
15. Mhe. Condester Michael Sichwale, Mb
16. Mhe. Irene Alex Ndyamkama, Mb

17. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb
18. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb
19. Mhe. Mwantum Dau Haji, Mb
20. Mhe Shanif Jamal Mansoor, Mb
21. Mhe. Zacharia Paul Issaay, Mb
22. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb
23. Mhe. Seif Salum Seif, Mb
24. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb
25. Mhe.Dkt Pindi Hazara Chana, Mb
26. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamisi, Mb

**Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb), kwa kuteuliwa na Mheshimwa Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.Deogratus John Ndejembji (Mb), Naibu Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wakiongozwa na Makatibu Wakuu Dkt. Moses Kusiluka (Ikulu), Dkt Laurean Ndumbaro (Utumishi), na Naibu Katibu Mkuu (Utumishi) Dkt.Fransic Michael, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Aidha, nawashukuru kwa dhati kabisa wakuu wa Taasisi, Idara na vitengo vilivyopo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa ushirikiano wao na utekelezaji makini wa Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara za Kamati Ndg, Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge, Ndg Gerald Magili, Makatibu wa Kamati, Ndg.

Chacha Nyakega, Ndg. Eunike Shirima na Ndg. Rabisante Moshi wakisaidiwa na Ndg. Paulina Mavunde, kwa uratibu wao mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Humphrey H. Polepole, Mb  
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU  
YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA**  
22 Aprili, 2021

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge za Serikali za Mitaa Mheshimiwa Humphrey Polepole kwa hotuba yako ukiwakilisha Kamati yako, kwa maoni mazuri ambayo nawashauri Waheshimiwa Wabunge myasome wakati tutakapokuwa tunaendelea na mjadala wa jambo huu. Ratiba ya mjadala ni kwamba Wizara hii ni ya siku mbili, lakini leo jioni tuna kazi maalum, kwa hiyo, kesho baada ya maswali tutaanza kuchangia moja kwa moja na tutahitimisha mjadala wa Wizara hii kesho. Kwa hiyo, wachingiaji wetu tunaweza tukaenda dakika tano tano lakini tutajitahidi tupate wengi tunavyoweza.

Kwa hiyo, tuendeleo kujiandaa baada ya maswali kesho tutaanza na uchangiaji moja kwa moja na jioni ya kesho tutahitimisha mafungu ya Ofisi ya Mheshimiwa Rais kazi itakamilika kesho Ijumaa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jioni ya leo tuhakikishe kwamba..., milango yetu hapa itafunguliwa kuanzia saa nane kamili tunawashauri Waheshimiwa Wabunge kwa vyovyote vile basi angalau saa tisa kamili uwe umekaa

kwenye kiti chako na vizuri kuwahi *parking* hata za nje zitakuwa na shida kidogo kwa sababu tuna ugeni mkubwa sana, kwa hiyo *earlier the better*. Ratiba nyingine tutapeana kadri ya hali inavyokwenda, nia yetu tusizidishe saa tano kamili kwa sababu yanatakiwa masaa matatu ya kuweka ukumbi sawasawa kwa ajili ya ujio wa leo jioni, kuweka ukumbi sawasawa kila kiti hapa lazima kiangaliwe kikaguliwe, kwa hiyo, unahitajika muda wa kufanyia kazi mambo haya.

Nadhani jana sijui Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini alitaka mwongozo wangu kuhusu habari ambazo zinapatikana katika mitandao ya kijamii endapo zinaweza kutumika kama rejea, kama *reference* katika majadiliano humu Bungeni, nafikiri mnakumbuka.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kifupi sana nitoe mwongozo huo kama ifuatavyo; kwamba taarifa za mitandao ya kijamii tuzitumie lakini kwa tahadhari na ungalifu mkubwa sana hasa katika majadiliano hapa Bungeni, Mheshimiwa Mbunge usifanye rejea taarifa hizo bila ya kufanya kwanza uthibitisho na utafiti zaidi kuhusu ukweli wake.

Kanuni zetu zinazuia Mbunge kutoa taarifa za uongo Bungeni na endapo Mbunge unayetoa taarifa hizo utatakiwa kuthibitisha ukweli wake utalazimika kufanya hivyo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge. Utakapotakiwa kufanya hivyo rejea yako ikawa mitandao ya kijamii maana yake hutakuwa na ushahidi na kwa hiyo unaweza ukajikuta kwenye matatizo kidogo na huo ndio mwongozo wangu kuhusu hilo. (*Makofi*)

Basi baada ya shughuli hizi za leo kukamilisha, sisitishi bali naahirisha shughuli za Bunge hadi leo saa kumi kamili jioni.

(*Saa 4.53 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Saa 10.00 Jioni*)

(*Saa 9.20 Jioni Misafara ya Viongozi wa Kitaifa Ilianza Kuingia Ukumbini*)

**NDG. KATHERINE KAIHULA – MSHEREHESHAJI:**

Waheshimiwa Wabunge na wageni waalikwa, msafara wa kwanza kuingia Ukumbini utakuwa wa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na Spika wa Bunge la Afrika Mashariki, Mheshimiwa Martin Ngoga, wakiongozwa na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza akitanguliwa na Mpambe wa Bunge, Bi. Fatma Hamza na kufuatiwa na Makatibu Mezani, Bi. Neema Msangi na Bwana Emmanuel Mpanda. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar - Mhe. Zubeir Ali Maulid na Spika wa Bunge la Afrika Mashariki - Mhe. Martin Ngoga, uliingia Ukumbini)*

**NDG. KATHERINE KAIHULA – MSHEREHESHAJI:**

Msafara wa pili ni wa Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mheshimiwa Omar Othman Makungu. *(Makofi)*

Msafara huu utaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, akitanguliwa na Mpambe wa Bunge, Bwana Habib Shedafa na kufuatiwa na Makatibu Mezani, Bi. Zainab Issa na Bwana Mossy Lukuvi. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Jaji Mkuu wa Tanzania - Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Omar Othman Makungu, uliingia Ukumbini)*

**NDG. KATHERINE KAIHULA – MSHEREHESHAJI:**

Waheshimiwa Wabunge na wageni waalikwa, ninawaomba misafara yetu inapokuwa inaingia tuweze kusimama.

Waheshimiwa Wabunge na wageni waalikwa, msafara wa tatu ni wa Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah. *(Makofi)*

Msafara huu utaongozwa na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, akitanguliwa na Mpambe wa Bunge, Bi. Ruth



Kaijage na kufuatiwa na Makatibu Mezani, Bi. Asia Minja na Bwana Athuman Hussein. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar - Mhe. Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar - Mhe. Hemed Suleiman Abdullah, uliingia Ukumbini)*

**NDG. KATHERINE KAIHULA – MSHEREHESHAJI:**

Waheshimiwa Wabunge na wageni waalikwa, msafara wetu wa nne ni wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi/Vigelele)*

Msafara huu utaongozwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, akitanguliwa na Mpambe wa Bunge, Bwana Rashid Kapongo na kufuatiwa na Makatibu Mezani Bwana Joshua Chamwela na Bi. Ruth Makungu. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, uliingia Ukumbini)*

**NDG. KATHERINE KAIHULA – MSHEREHESHAJI:**

Waheshimiwa Wabunge na wageni waalikwa, msafara wa tano ni wa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Msafara huu utaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika wa Bunge, akitanguliwa na Mpambe wa Bunge, Bwana Silvano Mkanza na kufuatiwa na Makatibu Mezani, Bwana Lawrence Makigi, Bi. Pamela Pallangyo na Bwana Bakari Kishoma. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, uliingia Ukumbini)*

**NDG. KATHERINE KAIHULA – MSHEREHESHAJI:**

Waheshimiwa Wabunge na wageni waalikwa, baada ya

misafara hii yote kuingia Ukumbini, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, wataingia ndani ya Ukumbi huu wa Bunge wakitanguliwa na Mpambe wa Bunge, Ndugu Mohamed Mwanga, akifuatiwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai na Makatibu Mezani Ndugu Nenelwa Mwihambi na Ndugu Ramadhan Issa Abdallah. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mhe. Samia Suluhu Hassan akiongozana na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mhe. Job Y. Ndugai, uliingia Ukumbini)*

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Hapa Wabunge walipiga makofi, vigelegele na kuimba wimbo wa tuna imani na Samia.

**SPIKA:** Tukiwa tumesimama sasa ni Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki. *Brass band.*

### **WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zillimbwa)*

**SPIKA:** Nawaomba tukae.

Mheshimiwa Rais, mbele yako ni Bunge la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Ninayofuraha kubwa kukuaribisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluh Hassan katika ukumbi huu wa Bunge ambao wewe ni mzoefu nao, maana ulikuwepo hapa kama Mbunge, ulikuwepo hapa kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, ukikaa maeneo haya ninavyokumbuka na ukitumia *microphone* hiyo kujibu maswali ya Wabunge. *(Makofi)*

Lakini mtakumbuka kwamba wakati wa Bunge la Katiba pia ulikuwa hapa hapa na ukiwa Makamu Mwenyekiti ulikaa kiti hiki hiki ninachokaa Spika na Bunge lile lilikuwa gumu sana, lakini mnakumbuka jinsi ambavyo Mama Samia aliliongoza kwa ushupavu mkubwa sana. *(Makofi)*

Nafurahi pia kuwepo kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu hadi majuzi hapa, Mheshimiwa Makamu wa Rais, karibu. *(Makofi)*

Lakini pia ninayofuraha kumkaribisha Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambaye naye si mgeni kabisa katika ukumbi huu. *(Makofi)*

Pia napenda kumkaribisha Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud na Makamu wa Pili Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, vilevile tunaye Jaji Mkuu, Profesa Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Zanzibar Omar Othman Makungu. Pia Spika wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na Spika wa Bunge la Afrika Mashariki Mheshimiwa Martin Ngoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, Bunge letu bado lipo kwenye robo ya kwanza kabisa ya uhai wake na katika kutekeleza majukumu yake haya ya mwanzo mwanzo na huu ni Mkutano wa Tatu tu tangu limeanza, tayari maswali zaidi ya 250 yameshaulizwa na Wabunge na yamejibiwa na Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, tayari katika muda huu mfupi Bunge hili limeshapitisha Miswada miwili ya Sheria. Tayari Bunge hili limeshaidhinisha Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, lakini pia, Bunge hili limeshapitisha tayari maazimio mawili; moja likiwa linaenzi Maisha ya Hayati

Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Azimio la pili ambalo limeshapitishwa na Bunge hili linakupongeza wewe kuwa Rais wa Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, pia Bunge hili, limeshapitisha bajeti mbili, Bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Bajeti ya Ofisi yako Mheshimiwa Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Na leo tumeshaianza na tunaendelea nayo bajeti ya Ofisi yako upande wa Utumishi na Utalawa Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, naomba baada ya kusema hayo nikushukuru tena kwa mara nyingine kwa kutenga muda na kuja kuzungumza na Bunge hili na kupitia Wabunge hawa utazungumza na watanzania kwa ujumla na hata wale watanzania walio nje ya nchi utakuwa unaongea nao moja kwa moja ni imani yetu kwamba ujio wako utakuwa na baraka nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge nikukaribishe sana Mheshimiwa Rais wetu kwa ajili ya kutoa hotuba yako. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Spika wa Zanzibar, Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Viongozi Wastaafu, Marais Wastaafu mliopo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Marais Wastaafu mliopo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Waheshimiwa Makamu wa Rais Wastaafu mliopo, Mawaziri Wakuu Wastaafu mliopo, Maspika Waastafu mliopo hapa, Mama zetu Wake wa Viongozi mliopo, Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa

Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Waheshimiwa Mabalazi na Wakilishi wa Jumuiya za Kimataifa wa Mashirika ya Kimataifa, Ndugu Wanahabari, Wageni Waalikwa kama mimi nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Kazi iendelee. *(Makofi)*

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema na rehema zake, niruhusu niseme kuwa ni miaka takribani sita imepita tangu niondoke kwenye jengo hili adhimu la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi, leo ninayo furaha kurudi tena na kupata fursa hii ya kulihutubia Bunge ambalo limenilea, limenijenga, limeninoa na ni Bunge hili lililofanya uwezo wangu uonekane na wote mpaka kuweza kushika nafasi hii niliyonayo. *(Makofi)*

Nimefarijika kuona baadhi ya wenzangu niliokuwa nao bado wapo ndani ya Bunge hili, lakini nimepata faraja zaidi baada ya kuziona sura mpya zenye ari na matumaini ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa ukarimu wako pamoja na Waheshimiwa Wabunge kunikaribisha leo hii ndani ya Bunge hili. Nimekuja kulihutubia Bunge baada ya nchi yetu kupita kwenye kipindi kigumu cha historia ya uongozi. Kama inavyokumbukwa, tarehe 17 Machi, 2021, Taifa letu lilipatwa na msiba mkubwa wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa sababu hiyo, kabla sijaendelea mbele na hotuba yangu, naomba sote tusimame kwa dakika moja tumuombe Hayati Rais Magufuli.

*(Hapa Wabunge walisimama kwa dakika moja na kumuombea aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli)*

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi. Amina.

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Amina.

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Naomba tukae.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba Mheshimiwa Hayati Rais Dkt. Magufuli alikuwa kiongozi hodari, jasiri na shupavu, mwenye maono, ambaye aliipenda nchi yetu na kuitumikia kwa uaminifu na uadilifu mkubwa. Hivyo basi, napenda nitumie fursa hii kurudia tena kutoa pole nyingi sana kwa familia, hususan kwa Mama Mzazi wa Marehemu Mama Susan Magufuli, lakini pia kwa Mama Mjane wa Marehemu Mama Janeth Magufuli, watoto, ndugu pamoja na jamaa.

Aidha, napenda kutoa pole kwa Bunge hili Tukufu ambalo kabla ya kuwa Rais alikuwa mwenzenu kwa miaka 20 humu ndani. Kama mnavyofahamu, kwa mujibu wa Katiba yetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni sehemu ya Bunge hili, hivyo basi, sina budi kutoa pole nyingi kwa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kurudia kuwapa pole nyingi Watanzania wote kwa kumpoteza Kiongozi wetu mpendwa. Kwa hakika, Taifa letu limeondokewa na mmoja wa viongozi mahiri, mzalendo, mwana mwema wa Tanzania ambaye tulimpenda na tunathamini mchango wake kwa Taifa. Mapenzi haya ya Watanzania yalidhihirika wazi wakati tukiwa kipindi cha maombolezo na mazishi ambapo sote tulishuhudia idadi kubwa ya wananchi wakijitokeza kumuaga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia kifo cha Hayati Rais Dkt. Magufuli, tarehe 19 Machi, 2021, kwa kuzingatia Katiba ya nchi yetu, niliapishwa kushika hatamu za uongozi wa Taifa letu. Hivyo basi, napenda kwanza kabisa kumshukuru

Mwenyezi Mungu kwa kutupitisha salama au kulipitisha salama Taifa letu kwenye kipindi cha mabadiliko ya uongozi wa nchi. *(Makofi)*

Namshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kushusha kudra yake kwangu mimi mja wake, kwani dhamana hii ni kubwa na yenye mitihani mingi. Kwa hakika sina budi niombe sana Mungu anisaidie katika nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nikishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi ambacho kimenijengea uwezo mkubwa na wakati wote kimeniamini. Kama nisingeaminiwa na chama changu, huenda leo nisingekuwa mbele yenu kulihutubia Bunge hili. *(Makofi)*

Nawashukuru pia viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali, ambao wamenilea na kunijengea uwezo na pia kujiamini. Na hapa naomba niwashukuru kwa moyo wa dhiti kabisa, Waheshimiwa Marais Wastaafu wote pamoja na viongozi wote wakuu wa Kitaifa kwa kuwa nami bega kwa bega katika nyadhifa zangu mbalimbali za utumishi nilizopata kushika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, napenda kutambua mchango na malezi ya Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, wastaafu Mheshimiwa Amani Abeid Karume na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Niseme wazi kuwa uwezo wangu wa uongozi uliibuliwa na Mheshimiwa Amani Karume aliyenipa nafasi ya Uwaziri katika kipindi changu cha awali na cha pili nikiwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Malezi haya yaliendelezwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliyenipa Uwaziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baadaye kuniamini kwenye nafasi ya kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Fursa hii ilinipa nafasi ya kuwajua na kufanya kazi na baadhi yenu humu ndani na ndiyo fursa iliyonitambulisha kwa Watanzania. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana, ingawa hatuko naye duniani, Hayati Rais Dkt. Magufuli kwa kuniamini kuwa Mgombea Mwenza wake kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na vilevile Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Kuniamini kwake hatimaye kumeweza au kumeniwezesha kuwa mwanamke wa kwanza nchini kushika wadhifa..... *(Makofi/Vigelele)*

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nirudie. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, kuaminiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kumenifanya niwe mwanamke wa kwanza nchini kushika nafasi ya Umakamu wa Rais na hatimaye sasa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, nalishukuru Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa ambao limenipa tangu nimechukua dhamana ya kuliongoza Taifa letu. Nalishukuru sana Bunge kwa kupitisha Azimio la Kunipongeza na kuniahidi ushirikiano mkubwa, lakini pia nalishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuridhia pendekezo langu la kumteua Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa kukubali uteuzi huo na kwamba sasa amejipanga kuchapa kazi sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwezi kuhitimisha shukrani zangu bila kuwashukuru viongozi wengine wa Serikali kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa tangu nimekabidhiwa dhamana ya kuliongoza Taifa letu.

Namshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na Serikali yake, tumeanza kufanyakazi kwa ukaribu zaidi. Namshukuru pia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi/Vigelele)*



Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa na nadhani mmemuona alivyoanza kuchakarika na kwenda mbio na kazi. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Jaji Mkuu na kupitia yeye Mhimili wa Mahakama; nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri; Katibu Mkuu Kiongozi - Ndugu Hussein Kattanga; Wakuu wa Mikoa; Makatibu Wakuu pamoja na viongozi wengine wote wa Serikali. Kwa namna ya pekee, navishukuru vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama ambavyo kwa ari kubwa vinaendelea kulinda amani na usalama wa nchi yetu na mipaka yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napende pia kuwashukuru Viongozi wetu wa Dini ambao wakati wote wamekuwa wakifanya dua na sala kuliombea Taifa letu. Nawashukuru viongozi wa Vyama vya Siasa kwa ushirikiano wanaonipa. *(Makofi)*

Mwisho si kwa umuhimu, navishukuru Vyombo vya Habari kwa kuendelea kutoa taarifa na kuwaelimisha Watanzania kuhusu masuala mbalimbali yanayojitokeza nchini. Lakini pia kwa namna ya pekee ni nawashukuru Watanzania wote, kwa kuendelea kuniamini na kuiunga mkono Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu nchi yetu imefikisha miaka 57 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar pamoja na Muungano wetu na tutasherehekea miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Katika kipindi hicho chote, mafanikio mengi makubwa yamepatikana. Napenda nitumie fursa hii kuzishukuru na kuzipongeza Awamu zote za uongozi wa nchi yetu. Kuanzia Awamu ya Kwanza iliyoongozwa na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere; Awamu ya Pili, iliyoongozwa na Mzee Ali Hassan Mwinyi; Awamu ya Tatu ya Hayati Mzee Benjamin William Mkapa, Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Awamu ya Tano iliyoongozwa na mtangulizi wangu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, kwa mafanikio hayo ambayo tumeyapata ndani nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa upande wa Zanzibar, nazishukuru Awamu zote Nane za uongozi kwa kujenga ustawi na maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar mpaka hatua tuliyofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami hapa leo mwanzoni kabisa naomba nieleze Bunge hili Tukufu pamoja na Watanzania kwa ujumla kuwa dira na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita itakuwa ni kudumisha mazuri ya awamu zilizopita, kuyaendeleza mema yaliyopo na kuleta mengine mapya. Na hii kimsingi ndio dhana na maana halisi ya kauli mbiu au salaam yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi lendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaenzi na kuendeleza mambo yote mazuri lakini pia tutafanya mabadiliko pale itakapobidi kwa lengo la kukuza ufanisi na tija, huku tukiongozwa na dira ya maendeleo ya mwaka 2020/2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063 na Ajenda ya Dunia ya Malengo Endelevu ya mwaka 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo utakumbuka kuwa wakati akizindua Bunge hili tarehe 13 Novemba, 2020. Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alieleza mambo mbengi muhimu ambayo yangepewa kipaumbele na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwenye miaka mitano hii. Kwa kuzingatia ilani yetu ya uchaguzi ya mwaka 2020/2025 hivyo basi, kwa kuwa nilishiriki kikamilifu katika kuinadi ilani hiyo na kwa kuwa kama nilivyowahi kusema na leo nataka nirudie tena kusema kuwa mimi na hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli tulikuwa kitu kimoja. Kwa maana hiyo, mambo mengi ambayo Serikali ninayoiongoza imepanga kuyatekeleza ni yale ambayo yalielezwa na Rais, hayati Dkt. John Pombe Magufuli wakati akilizindua Bunge hili. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa mniruhusu nitaje baadhi ya masuala muhimu ambayo Serikali ya Awamu ya Sita itayapa kipaumbele kwenye miaka mitano hii.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza na muhimu kabisa tutakalolipa kipaumbele kwenye miaka hii mitano ni kuendelea kulinda na kudumisha Tunu za Taifa letu yaani amani, umoja na mshikamano, uhuru wa nchi yetu, Mapinduzi matukufu ya Zanzibar pamoja na Muungano wetu. Kama mnavyofahamu, amani na umoja ni msingi mkuu wa maendeleo katika Taifa lolote. Hivyo basi, nawasihi sana Watanzania tushirikiane kwa pamoja katika kulinda tunu hizi. Tanzania ni yetu sote, kila mmoja wetu anao wajibu wa kuhakikisha anazilinda na kuzitetea tunu hizi mahali popote alipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na kulinda na kuzitunza tunu hizi za Taifa letu, tunakusudia kuelekeza nguvu kubwa katika kusimamia ukuzaji uchumi na kama mnavyofahamu kwenye miaka ya hivi karibuni, hususan kwenye miaka mitano iliyopita Taifa letu limepata mafanikio makubwa ya kiuchumi. Tumesimamia ukuaji wa uchumi kwa wastani wa asilimia 6.9 kwa mwaka; tumedhibiti mfumuko wa bei kwa wastani wa asilimia 4.4; na kupunguza umasikini hadi kufikia asilimia 26.6. Muhimu zaidi, mwaka jana mwezi Julai 2020 Taifa letu lilifanikiwa kuingia kwenye kundi la nchi za uchumi wa kati, ambapo pato la wastani wa kila Mtanzania limeongezeka hadi kufikia Dola za Marekani 1,080; zaidi ya kigezo cha dola za Marekani 1,036 cha kuingia kwenye kundi hilo. Haya bila shaka ni mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na mafanikio hayo makubwa, ni wazi kuwa jitihada zaidi zinahitajika ili kukuza uchumi na kupambana na umasikini nchini. Hii ni kwa sababu licha ya mafanikio yaliyopatikana, kasi ya ukuaji uchumi bado ni ndogo. Wataalam wa uchumi wanatueleza kwamba ili kuweza kupambana na umasikini, uchumi wetu unatakiwa ukuwe angalau kwa asilimia nane kwa mwaka. Lakini kutokana na dunia kukumbwa na janga la Corona, kiuhalisia takwimu zinaonesha kwamba chumi nyingi duniani zimeshuka. Tanzania nayo imeathirika kwa kushuka kwa kiwango cha uchumi kutoka wastani wa asilimia 6.9 hadi asilimia 4.7. Hii inamaanisha kwamba katika miaka mitano

ijayo tunahitajika uwekezaji mkubwa sana katika sekta za uzalishaji na zitazotoa ajira kwa wingi. *(Makofi.)*

Mheshimiwa Spika, hatua mahsusi tutakazozichukua katika kukuza uwekezaji, ni pamoja na kufanya marekebisho kadhaa katika sera, sheria na kanuni zetu na kuondoa vifungu vitakavyobainika kusababisha vikwazo katika kukuza uwekezaji. *(Makofi)*

Tutaendelea kuboresha sera zetu za uchumi wa jumla pamoja na sera za fedha na kuhakikisha viashiria vyote vya uchumi ikiwemo thamani ya sarafu yetu, mfumuko wa bei pamoja na viwango vya riba vinabaki kwenye hali ya utulivu. Sambamba na hilo, hatutokuwa tayari kuvumilia uvivu, uzembe, wizi na ubadhirifu wa mali na fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tutachukua hatua madhubuti za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ili kuivutia sekta binafsi kushiriki vizuri kwenye shughuli za kiuchumi. Mwelekeo utakuwa kurudisha imani kwa wawekezaji na kutoa vivutio kwa wawekezaji mahiri; vivutio kwa wawekezaji mahiri yaani *strategic investors* ikiwa ni pamoja na kuwezesha uwekezaji kufanyika kwa haraka. Uwekezaji upo mkubwa watu wanapokuwa kutaka kuwekeza. Serikali ya Awamu ya Sita tunakwenda kukomesha hilo, na uwekezaji sasa utakwenda kufanyika kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutakuwa na sifa na matakwa maalum yatakayowekwa kwa uwazi katika kutambua miradi ya kimkakati itakayostahiki vivutio vya kikodi au vivutio vinginevyo. Suala la upatikanaji wa mitaji nalo halina budi kuangaliwa kwa umakini mkubwa na kama mnavyofahamu ili sekta binafsi iweze kushiriki vizuri, hatuna budi kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara. Nchi yetu imekuwa ikilalamikiwa kwa kutokuwa na mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji ikiwemo kutokuwa na sera zinazotabirika, utaratibu wa kodi usio na utulivu, urasimu mwingi katika kutoa

huduma kwa wawekezaji na matatizo mengine yanayokwamisha ustawi wa biashara na uwekezaji. *(Makofi.)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Serikali ya Awamu ya Sita inakusudia kufanya maboresho makubwa kwenye eneo hilo. Kwanza, tutahakikisha tunatekeleza kikakamilifu mpango wetu wa kuboresha mazingira ya biashara nchini. Zaidi ya hapo, nimeiweka Wizara ya Uwekezaji chini ya uangalizi wa Waziri Mkuu ili kurahisisha uratibu wa pamoja na ukaribu katika kuhakikisha tunaondoa urasimu kwenye masuala ya uwekezaji. Urasimu katika masuala ya uwekezaji inajumuisha pia ucheleweshaji wa kutoa vibali na leseni. Tunataka jambo hili lifanyike kwa muda mfupi sana. Lakini vilevile upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji; wawekezaji wamekuwa wakizunguka mbele - nyuma, kulia - kushoto na wanachelewa kupata ardhi kwa ajili ya uwekezaji, tunataka tukaweke hilo nalo sawa ili uwekezaji ufanyike kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitoe wito na narudia kutoa wito wangu, kwamba huko nyuma nilizungumzia kuharakisha kutengeneza dirisha moja la mfumo wa kutoa huduma kwa mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa tunakusudia kufanya mageuzi ya kiutendaji kwenye mfumo wa utozaji na ukusanyaji wa kodi, kuweka mfumo utakaorahisisha na kuvutia walipa kodi na kutengeneza wigo mpana zaidi wa walipa kodi, ikilinganishwa na walipa kodi waliopo leo. Tumejitahidi sana katika Awamu ya Tano kuongeza makusanyo ya kodi kutoka wastani wa shilingi bilioni 850 mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa shilingi trilioni 1.9 hivi sasa. Makusanyo haya yanatokana na Kodi ya Forodha ambayo ni asilimia 40 na kodi za ndani ambayo haizidi asilimia 20. Hii ina maana kwamba ni Watanzania wachache ndio wanaolipa kodi, kati ya Watanzania wanaokadiriwa kufikia milioni 60. *(Makofi)*

Hivyo basi, kuna kila haja ya kutanua wigo wa walipa kodi na vilevile, kuweka mifumo rafiki ya ulipaji na ukusanyaji

wa kodi. Ningependa kuona wafanyabiashara, wawekezaji na wananchi wanalipa kodi bila shuruti na bila ya matumizi ya nguvu, wakitambua kwamba kodi ni maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumedhamiria pia kufanya mapitio ya uchambuzi wa kina kwenye uendeshaji wa mashirika ya umma tukiwa na lengo la kuyafanya yaweze kujendesha kwa faida. Mashirika yaliyo mengi yanaendeshwa kwa kususua kiasi kwamba unapofika wakati wa kutoa gawio Serikalini, uongozi na Bodi za Mashirika hayo yanahangaika huku na kule kutafuta gawio la Serikali wakihofia nafasi na ajira zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika vilevile, tutaendelea kufanya kazi kwa karibu sana na sekta binafsi kwa kutambua kuwa wao ndio kiini cha ukuaji wa uchumi. Kwa kudhihirisha hilo, pamoja na mambo mengine, Serikali tunashirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) kuanzisha mfumo wa kupokea na kushughulikia changamoto za wawekezaji nchini kwa njia ya mtandao. Lengo la mfumo huo ni kurahisisha ushughulikiaji wa changamoto za wawekezaji kwa njia ya haraka na kuleta ufanisi katika kuwahudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa pia na malalamiko mengi kwenye upatikanaji wa vibali vya kazi kwa wageni. *(Makofi)*

Kuna msemo unao sema ukimuona mtu mzima analia ujue kuna jambo. Hapa napo kwa kuwa malalamiko yamezidi hatuna budi kuliangalia upya suala hili huku tukilinda maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa hatua hizi, pamoja na nyingine ambazo sikuzitaja, zitavutia wawekezaji na wafanyabiashara wengi ikiwemo wa ndani, kuwekeza kwenye sekta mbalimbali nchini na hivyo kusaidia juhudi za Serikali za kukuza uchumi, kupambana na umasikini na kukabiliana na tatizo la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania ni wakulima ambao wanajishughulisha na kilimo cha mazao, ufugaji na uvuvi. Hivyo basi, ni ndoto kwetu kufikiria kwamba tutaongeza kasi ya kukuza uchumi na kukabiliana na umasikini bila ya kuelekeza nguvu kubwa au ya kutosha katika sekta hizo. *(Makofi)*

Ni kweli, kwenye miaka mitano iliyopita tumeweza kupata baadhi ya mafanikio kwenye sekta ya kilimo. Mathalani, sekta hii kwa sasa inachangia asilimia 100 ya chakula kinacholiwa nchini, asilimia 60 ya malighafi za viwandani, asilimia 27.7 ya Pato la Taifa na asilimia 25 ya fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, sekta ya kilimo bado inakabiliwa na matatizo mengi, lakini kubwa zaidi ni udogo wa tija au uhaba wa mavuno. Nimeeleza hivi punde kuwa zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania ni wakulima, lakini mchango wao kwenye Pato la Taifa ni asilimia 27 tu. Hii inatokana na tija ndogo inayopatikana kwenye kilimo cha mazao mbalimbali hasa mazao ya biashara. Kwa mfano, kilimo cha mahindi chenye tija kinawezesha uvunaji wa tani nane kwa hekta, lakini kwa hapa kwetu wastani wa uzalishaji kwa hekta ni tani 1.9 tu. *(Makofi)*

Aidha, tunazalisha pamba kilo 250 kwa ekari moja wakati zipo nchi wanazalisha kati ya kilo 1,000 hadi 1,250 kwa ekari. Na hali hii ipo kwenye mazao takribani yote tunayozalisha nchini. Ukiachilia mbali tija ndogo kwenye kilimo cha mazao, nchi yetu licha ya kushika nafasi ya pili kwa mifugo Barani Afrika, sekta ya mifugo inachangia asilimia 7.4 tu kwenye Pato la Taifa. Mwaka 2019/2020 tulizalisha tani 701,679 za nyama na lita bilioni tatu za maziwa. Hii inatokana na matumizi madogo ya mbinu za kisasa za ufugaji. Mathalan, ng'ombe wetu kwa wastani wanazalisha lita tatu za maziwa kwa siku wakati kwa kutumia mbinu za kisasa wanaweza kuzalisha hadi lita 20 hadi 30 kwa siku. Ng'ombe wetu wanatoa nyama isiyozidi wastani wa kilo 150 lakini mahali

kwingine duniani ng'ombe wanafikisha kutoa kilo 500 – 600 za nyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi, nako hali iko vivyo hivyo licha ya kuwa na maeneo mengi makubwa yenye kufaa kwa uvuvi, ikiwemo mwambao wenye urefu wa takribani kilometa 1,400; maziwa makubwa pamoja na mito mingi, mauzo ya samaki nje ya nchi ni madogo na wakati mwingine nchi yetu inaagiza samaki kutoka nje. Hii inadhihirisha kuwa tija kwenye sekta ya kilimo bado ni ndogo sana. *(Makofi)*

Hivyo basi, kwenye miaka hii mitano tunayokwenda nayo, tutaelekeza nguvu kubwa katika kujenga misingi imara wa sekta ya kilimo kwa lengo la kuongeza tija. Tutajitahidi kuwekeza katika kilimo cha biashara, kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kwa kuongeza uwekezaji kwa Taasisi za Serikali za *TAR/na ASA* ili zizalishe na kuhamasisha matumizi ya mbegu bora kwa wakulima. Taasisi hizo tutazipa fedha za kuanzia kama mtaji na tutazitaka ziendeleo kuzalisha kibiashara. Hii itasaidia kutumia fedha nyingi kuagiz ambegu kutoka nje. Utaalam upo ndani, tutatumia wataalam wa ndani kuzalisha mbegu ili tuweze kuzalisha kwa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine kwenye sekta hii ni upatikanaji wa mbolea ya kutosha na kwa wakati, kuboresha afya ya udongo, kukuza huduma za utafiti na huduma za ugani, kujenga masoko imara kwa kujenga miundombinu na mfumo wa kuwezesha uuzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi yetu, pamoja na upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu. Tutaongeza pia eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 561,383 hadi hekta milioni 1.2 ifikapo mwaka 2025 ili kupunguza kilimo cha kutegemea mvua. Tutakamilisha ujenzi wa skimu za umwagiliaji zilizopo na kuhakikisha zinafanya kazi kwa tija. Lakini hapa napo tunakwenda kuwafanya wakulima katika skimu za kumwagilia wachangie Mfuko wa Umwagiliaji Maji, kwa sababu Serikali inatengeneza skimu za umwagiliaji maji, wakulima wanatumia skimu zile kulima kibiashara, lakini



hawachangii kitu kwenye Mfuko wa Umwagiliaji. Kwa hiyo tunakwenda kufanya mabadiliko hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tutaendeleza ujenzi wa vihenge na maghala maeneo mbalimbali nchini ili kuondoa tatizo la upotevu wa mazao baada ya kuvunwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufugaji, kama nilivyowahi kusema tunalenga kuachana na uchungaji wa kuhamahama. Pia kama alivyosema Rais Mstaafu Kikwete, kwamba uchungaji huu hauna tija, ng'ombe hanenepi na mchungaji hanenepi. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa katika kutimiza azma hii, tutaelekeza nguvu kubwa katika kuhamasisha ufugaji wa kisasa. Tutajielekeza kwenye uzalishaji kwa njia ya uhamilishaji kwa lengo la kubadili kosaafu. Ndugu zangu hiki ni Kiswahili kipya, kosaafu ni *breed*, ni sifa ya ng'ombe, kosaafu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutabadilisha kosaafu ya mifugo yetu, ili kuwawezesha wafugaji kuwa na mifugo michache yenye sifa za uzalishaji mkubwa uwe wa nyama au maziwa na kuongeza tija. Pia tutaongeza vivutio vya kuzalisha mbegu bora na pia kuongeza uzalishaji wa chakula cha mifugo viwandani kutoka tani 900,000 hadi tani milioni nane, kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunakusudia kuongeza maeneo ya ufugaji kutoka hekta 2,788,901 za sasa hadi hekta 6,000,000. Lengo ni kupunguza tabia ya sasa ya wafugaji kuhamahama ambayo inasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira pamoja na kuzusha migogoro kati yao na wakulima. *(Makofi)*

Kwa upande wa uvuvi, tutaimarisha usimamizi wa uvuvi wa Bahari Kuu ili Taifa letu linufaike na rasilimali zake. Na katika hilo, tumepanga kununua meli nane za uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la *IFAD* ili zishiriki katika uvuvi wa Bahari Kuu ambapo meli nne zitafanya kazi upande wa Zanzibar na nne upande wa Tanzania Bara. *(Makofi)*

Aidha, tunakusudia kujenga bandari kwa ajili ya meli zitakazofanya uvuvi katika maeneo ya ukanda wa Bahari Kuu ya Tanzania. Tunajipanga kuanza utengaji wa vizimba vya kuvua samaki ndani ya bahari, utoaji wa vibali vya uvuvi katika Bahari Kuu na uwekezaji katika zana bora za kuvulia pamoja na uanzishaji wa viwanda vya uchakataji wa samaki na mazao mengine ya majini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, tunakusudia kuendelea kuimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kuiwezesha kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. Zaidi ya hapo, tunakusudia kuliangalia kwa karibu zaidi suala la bima ya kilimo na kuliwekea misingi imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukuza sekta ya kilimo, hatuna budi pia kuifungamanisha sekta ya kilimo na sekta ya viwanda. Kama nilivyosema awali kwamba kilimo kinachangia kwa kiasi kikubwa malighafi viwandani, aidha, viwanda navyo vinawahakikishia wakulima soko kwa mazao yao. Kwa bahati nzuri, kwenye miaka mitano iliyopita, tuliweza kuhamasisha ujenzi wa viwanda vingi nchini, kati yao vikiwemo vya kusindika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Hivyo basi, Serikali ya Awamu ya Sita itaendeleza jitihada za kuhamasisha ujenzi wa viwanda hivi nchini, hususani vile vinavyotumia malighafi za ndani. Tunakusudia pia kutenga maeneo ya viwanda kulingana na mazao yanayozalishwa. Aidha, njia nyingine itakayotumika kuongeza kasi ya viwanda ni kutenga na kuendeleza maeneo huru ya biashara, kipaumbele ni kwenye maeneo ya mipakani au maeneo yenye miundombinu ya usafiri, kama reli, bandari na barabara zinazotuunganisha na nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hapa nataka nitoe ufafanuzi kidogo, kumekuwa na mjadala mkubwa Bungeni na nadhani Spika ndiyo *champion* wake wa *industrial parks*. Nataka niwaambie, ili tukuze ajira na uchumi nchini lazima twende kwenye *industrial parks*. *(Makofi)*

Kongano ni muhimu, sasa inategemea kama zitawekwa Bagamoyo, Kizimkazi Zanzibar, wapi, kokote kule lakini *industrial parks* ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema tutaendelea kukuza miundombinu ya usafiri na usafirishaji tukiwa na lengo la kuzitumia vyema fursa za kibiashara kupitia itifaki mbalimbali kama vile Itifaki ya Afrika Mashariki, biashara huru Afrika Mashariki, *SADC*, lakini pia eneo huru la biashara la Afrika na kadhalika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini, ambayo kwa sasa imetoa ajira zipatazo milioni 1.5 ina nafasi kubwa ya kuchochea ukuaji uchumi nchini. Kwenye miaka mitano iliyopita, tumepata mafanikio makubwa kwenye sekta hii. Mchango wake kwenye Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 5.2 mwaka 2019. Mapato yake yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 168 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 527 mwaka 2020. Zaidi ya hapo mwaka 2019 Sekta ya Madini iliongoza kwa kuliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni, dola za Marekani bilioni 2.7. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inakusudia kuendeleza mafanikio hayo kwa kusimamia Sheria yetu ya Madini ya mwaka 2017, kuendeleza kuziba mianya ya utoroshaji wa madini yetu na kuendelea kuangalia kwa umakini mkubwa na kuondoa vikwazo vya uwekezaji katika sekta hii ili kuvutia na kurahisisha mijadala ya Serikali kuingia ubia na wachimbaji wakubwa duniani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tutaendelea pia kuimarisha masoko na minada ya uuzaji madini, kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa za madini. Mkazo utawekwa kwenye teknolojia bora na sio tu viwanda, lakini viwanda vyenye teknolojia bora! Tutawaendeleza wachimbaji wadogo na kuwapatia mafunzo, mikopo pamoja na vifaa. (Makofi)

Vilevile tutaliimarisha zaidi Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) ili liweze kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini ndani ya nchi, lakini pia na nje ya nchi. Hatua hizi naamini, zitaifanya Sekta ya Madini ikuze mchango wake kufikia asilimia 10 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sekta nyingine ambayo tutaipa mkazo mkubwa kwenye miaka hii mitano ni utalii. Kama mnavyofahamu, nchi yetu imebarikiwa kuwa na vivutio vingi vya utalii na sekta hii imeajiri takriban watu milioni nne. Kwenye miaka mitano iliyopita, mafanikio mengi yamepatikana kwenye Sekta ya Utalii ikiwemo kuongeza idadi ya watalii waliotembelea nchini kutoka milioni 1.1 mwaka 2015 hadi watalii milioni 1.5 mwaka 2019. Mapato nayo yaliongezeka kutoka dola za Kimarekani bilioni 1.9 mwaka 2015 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019. Hivyo basi, kwenye miaka hii mitano tunayokwenda nayo, pamoja na uwepo wa janga la Corona, tunalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwa kuongeza idadi ya watalii hadi kufikia milioni tano mwaka 2025 na mapato kutoka dola za Marekani bilioni 2.6 za sasa hadi kufikia dola za Marekani bilioni sita. Hatua ambazo tunakusudia kuzichukua ni pamoja na kupanua wigo wa vivutio vya utalii, ikiwemo kukuza utalii wa mikutano, malikale na fukwe, ambapo tunakusudia kujenga miundombinu ya kuwezesha meli za kitalii kuweza kuzuru nchini kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tutahamasisha pia wawekezaji kuwekeza kwenye miundombinu ya utalii, ikiwemo hoteli, ili kupunguza gharama za malazi. Tunajipanga kusomesha vijana wengi katika taaluma ya utalii ili waweze kuendesha maeneo mbali mbali ya sekta hiyo bila kutegemea wataalamu kutoka nje. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ili kuchochea shughuli za kiuchumi na uzalishaji nilizozitaja yaani kilimo, viwanda, madini na utalii tutaendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu ya usafiri ambayo ni moyo wa ukuzaji uchumi. Kwenye miaka mitano iliyopita, jitihada kubwa zilifanyika na kuimarisha usafiri wa barabara, reli, maji na anga. Jumla ya kilometa 3,537 za

barabara za lami zilijengwa pamoja na madaraja makubwa 12. Usafiri wa reli kutoka Dar es Salaam – Tanga – Moshi – Arusha ulifufuliwa pamoja na kuanza ujenzi wa Reli ya *standard gauge* kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora (Dodoma), ambapo kipande cha Dar es Salaam – Morogoro kimefikia asilimia 91 na Morogoro – Makutupora zaidi ya asilimia 58.2 hadi kufikia mwezi huu wa Aprili tulio nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa maji, umefanyika upanuzi mkubwa wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala Mkoani Pwani. Kwenye Ziwa Victoria tumejenga chelezo, tumekarabati meli mbili (MV. Victoria na MV. Butiama) pamoja na kujenga meli mpya. (*Makofi*)

Katika Ziwa Tanganyika umefanyika upanuzi na ukarabati mkubwa wa Bandari za Kigoma, Kalema, Kasanga na Kabwe; na kwenye Ziwa Nyasa zimejengwa meli mpya tatu na kufanya upanuzi wa Bandari za Kiwira na Itungi. Kuhusu usafiri wa anga, jumla ya viwanja vya ndege 11 vimepanuliwa ama kukarabatiwa na ndege mpya 11 zilinunuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye miaka hii mitano tunayokwenda nayo, tutatekeleza yaliyoagizwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kuendeleza ujenzi wa miundombinu hiyo ya usafiri na usafirishaji. Tutaendelea kukamilisha ujenzi wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Kigoma na kujenga barabara hususan kwenye maeneo ya kimkakati ambako shughuli za uzalishaji zinafanyika. Pia tukamilisha ujenzi wa madaraja makubwa, likiwemo Daraja la Kigongo – Busisi, Wami, *Tanzanite* na Daraja la Pangani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa reli; tutakamilisha ujenzi wa reli ya Dar es Salaam – Makutupora na kuanza ujenzi wa vipande vingine, kikiwemo cha Mwanza – Isaka ambapo tunakwenda kusaini na mkandarasi hivi karibuni, lakini pia tutaendelea na *lot* ya tatu ya Makutupora – Tabora na *lot*

ya nne ya Tabora – Isaka na baadaye tutamalizia Kaliua – Kigoma na Kaliua – Mpanda. *(Makofi)*

Aidha, tunakusudia kuimarisha usafiri wa TAZARA kwa lengo la kuiongezea ushindani Bandari yetu ya Dar es Salaam na pia kunufaika na fursa nyingine za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa majini. Tutakamilisha ujenzi wa meli mpya na kuanza ukarabati wa meli ya mabehewa yaani *ferry wagon* kwenye Ziwa Victoria na pia kuikarabati meli ya MV. Liemba na kuanza ujenzi wa meli mpya kwenye Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa anga; tutaendelea na utanuzi wa viwanja vya ndege mikoani na kujenga Kiwanja kipya cha Kimataifa cha Msalato hapa Makao Makuu Dodoma. Aidha, tutaendelea kulilea Shirika letu la Ndege la ATCL kimkakati. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, nimesema tutaendelea kulilea shirika letu la ndege kimkakati ili liweze kujiendesha kwa ufanisi na ninaposema kimkakati ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kutoa unafuu wa madeni na baadhi ya kodi na tozo, kama inavyofanyika kwenye nchi nyingine, ili liweze kuku ana liweze kuweka mahesabu yake sawa. Shirika letu sasa hivi linasomeka kwamba ni shirika la *deficit*, halina thamani, lakini ni kwa sababu ya kurithi madeni makubwa ya nyuma. Hivyo kama Serikali tunakwenda kulitua mzigo wa madeni makubwa, lakini pia, tutalipa unafuu wa kodi na tozo ili liweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa biashara ya ndege ni ngumu. Tutajitahidi kusoma mwenendo wa biashara hii ulimwenguni na kuepuka mambo yote yasiyo na tija kwa shirika letu. Hatutakubali kuona shirika linaendelea kupata hasara baada ya uwekezaji mkubwa tulioufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutawekeza kwenye kupata rasilimali watu wenye uwezo na weledi wa kuendesha shirika

kibiashara na hii ina maana tunakwenda kulifanyia uchambuzi wa kina na kuhakikisha tutakaowaamini kuliendesha shirika ni watu wenye weledi na wataweza kuliendesha shirika kibiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbali na miundombinu hiyo migumu tutaimarisha pia miundombinu laini hususan miundombinu ya teknolojia ya mawasiliano. Kama inavyofahamika, dunia ipo kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda, ambayo yanaongozwa na Sekta ya Teknolojia ya Mawasiliano (TEHAMA) na kwa maana hiyo, uchumi wa dunia pamoja na shughuli nyingi duniani kwa sasa, zinafanyika kwa kutumia TEHAMA. Hivyo basi, sisi Tanzania nasi hatuna budi kuweka mkazo mkubwa katika kukuza sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, tumepanga kwenye miaka mitano ijayo, pamoja na masuala mengine kuongeza kasi ya kufikisha miundombinu ya Mkongo wa Taifa kwenye maeneo mengi ya nchi yetu, hususan katika ngazi za Wilaya na pia kuongeza wigo wa matumizi ya mawasiliano ya kasi yaani *broadband* kutoka asilimia 45 ya sasa hadi asilimia 80 itakapofika mwaka 2025. (*Makofi*)

Aidha, tunakwenda kuongeza watumiaji wa *internet* kutoka asilimia 43 ya sasa hadi asilimia 80 mwaka 2025. Vilevile tunakwenda kuboresha upatikanaji wa mawasiliano ya simu kwa nchi nzima. Tutatoa kipaumbele kwenye masuala ya utafiti na ubunifu kwenye TEHAMA pamoja na kuimarisha usalama kwenye masuala ya mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye miaka mitano iliyopita, tumepata mafanikio makubwa kwenye sekta ya nishati. Tumeongeza uzalishaji umeme hadi kufikia megawati 1,602.3 ambapo mahitaji ya juu ya umeme ndani ya nchi yetu kwa sasa ni megawati 1,200. Tumefanikiwa pia kufikisha umeme kwenye vijiji 10,294 sawa na asilimia 83.3 ya vijiji 12,317 vilivyopo. Tumeanza pia utekelezaji wa mradi mkubwa wa umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere utakaozalisha megawati 2,115. Mradi huu kwa sasa umefikia asilimia 45; hivyo basi, Serikali ya Awamu ya Sita itaendeleza jitihada za

kuimarisha upatikanaji wa nishati nchini, ikiwemo kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Nyerere na kufikisha umeme kwenye vijiji 1,974 vilivyobakia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajipanga pia kuanza kutekeleza miradi ya kuzalisha umeme wa maji katika maeneo ya Ruhudji megawati 358, Rumakali megawati 222, Kikonge megawati 300 na pia umeme wa gesi asilia kule Mtwara megawati 13, Somanga Fungu megawati 330, Kinyerezi III megawati 600 na Kinyerezi IV megawati 300. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasi ya mabadiliko ya tabianchi, tunahitaji pia kuchanganya vyanzo vya nishati ili kuwa na uhakika wakati wote. Hivyo basi, tutaangalia uwezekano wa kutekeleza miradi ya nishati jadidifu inayotokana na jua, upepo na jotoardhi. Tutafanya hivyo kwa kuwa kwa kuwa vyanzo hivi ni endelevu na tunatarajia katika miaka hii mitano kuzalisha megawati 1,100 kupitia vyanzo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyengine, tutaendelea kutekeleza miradi ya kujenga njia za kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Nyerere hadi kituo kikuu pale Chalinze na njia zinazoelekea kwenye maeneo ambayo hayajaunganishwa na Gridi ya Taifa ili kupunguza gharama za uzalishaji umeme wa mafuta na pia kuokoa asilimia ya umeme inayopotea. Sambamba na hayo, tunatarajia kuanza utekelezaji wa miradi ya kielelezo ya bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Chongoleani kule Tanga, lenye urefu wa kilometa 1,445 pamoja na Mradi wa Kusindika Gesi Asilia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mradi huu wa LNG mazungumzo yake tunafika miaka sita sasa, kwa hiyo, tunakwenda kumaliza mazungumzo na kufanya mradi uanze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na shughuli hizo za kuchochea ukuaji wa uchumi nilizozitaja katika kipindi hiki cha



miaka mitano, tutaendelea kuimarisha na kuboresha huduma za jamii hususan afya, elimu na maji.

Kuhusu afya, kama mnavyofahamu, kwenye miaka mitano iliyopita tumepata mafanikio makubwa ikiwemo kujenga vituo vya kutolea huduma za afya 1,887 zikiwemo zahanati 1,198, vituo vya afya 487, hospitali za wilaya 99, hospitali za rufaa za mikoa 10 na hospitali za rufaa za kanda tatu. *(Makofi)*

Katika miaka mitano hii tunayokwendanayo mpaka 2025, tutaimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa kuendelea kujenga miundombinu, kuongeza watumishi, vifaa tiba, dawa na vitendanishi. Aidha, juhudi za kupunguza vifo kwa wajawazito na watoto zitaendelezwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge huu ni mradi wangu wa moyoni kabisa. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa Makamu wa Rais nilizindua Kampeni ya Jiongeze Tuwavushe Salama, ili kutilia mkazo uwajibikaji wa wadau wote katika kupunguza vifo vya mama na mtoto. Binafsi, huwa nasikitika sana kuona akinamama wanakufa wanapojifungua kwa sababu ambazo zinaweza kuzuilika. Kampeni ile niliyoizindua imetusaidia kupunguza vifo vya akinamama kwa kiasi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha tutaelekeza nguvu pia katika kinga na tiba, ikiwemo kwa magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza ambayo yanasababisha vifo vingi na kugharimu Serikali fedha nyingi. Tutaimarisha pia huduma za matibabu ya kibingwa na kuzipeleka huduma hizi kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa. *(Makofi)*

Tutaimarisha utoaji wa huduma za matibabu kwa wazee na tutaweka mipango maalum kuhudumia makundi yenye magonjwa adimu. Tutaimarisha Mifuko ya Taifa ya Bima ya Afya ili kufikia lengo la kuwa na Bima ya Afya kwa Watanzania wote. Kwa sasa inasikitisha kuona kwamba ni

Watanzania 8,224,271 peke yake ndio wanaotumia bima ambayo ni asilimia 14 tu ya Watanzania wote. Vilevile tutahamasisha ujenzi wa viwanda vya kutengeneza dawa, vitendanishi, vifaa tiba pamoja na chanjo mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ugonjwa wa *corona*; kama mnavyofahamu, ugonjwa huu umeathiri dunia nzima na ubaya zaidi ni kwamba, janga hili linapungua na kurudi tena na linaporudi linarudi katika mifumo tofauti. Mpaka sasa bado hakujawa na dalili za kupatikana kwa tiba ya maradhi haya. Njia pekee iliyopo ni kujikinga na maradhi haya kwa kuchukua hatua mbalimbali za kinga na tahadhari. Hapa nchini tumekuwa tukifuata miongozo kadhaa ya kinga inayotolewa na wataalam na kwa kiasi fulani kutumia njia zetu za asili au tiba asili tumeweza kwa kiasi kikubwa kupunguza kushusha kiwango cha maambukizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tumeamua kuunda Kamati ya Wataalamu ambao kwa kushirikiana na taasisi za afya na zile za Kikanda za *East Africa* na *SADC* wataliangalia suala hili kwa undani, kufanya uchambuzi wa kina na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua na jinsi ya kuendelea kupambana na maradhi hayo. Hivyo basi, wakati tukisubiri majibu ya kazi inayofanywa na kamati iliyoundwa, napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari zote zinazoshauriwa na wataalam. Nawaomba kila mmoja awajibike kwani ulinzi wa afya yako unaanza na wewe mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta ya Elimu; katika kipindi cha miaka mitano iliyopita udahili wa wanafunzi katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari uliongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na Sera ya Elimu Bila Malipo. Ongezeko hilo limeilazimisha Serikali kuweka nguvu kwenye ujenzi wa miundombinu ya elimu, kuongeza idadi ya walimu hasa walimu wa sayansi na hisabati na kusambaza vitendea kazi mashuleni. Kumekuwa na ongezeko la kiwango cha mfuko wa elimu ya juu ambao umeongeza pia idadi ya vijana wanaojiunga na vyuo vikuu. Awamu ya Sita itaendeleza kazi nzuri iliyofanywa katika miaka mitano iliyopita. Aidha,

tutajielekeza katika kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na kufanya marekebisho kwenye mitaala iliyopo ili ielekezwe kwenye kutoa elimu ujuzi. Tunataka mitaala yetu ijielekeze kwenye kutoa elimu ujuzi kulingana na mazingira ya nchi na soko la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji; licha ya mafanikio yaliyopatikana kwenye miaka mitano iliyopita tatizo la maji bado ni kubwa kwenye maeneo mengi nchini. Hali hii inachangiwa na usimamizi usioridhisha wa miradi na vilevile matumizi mabaya ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya upatikanaji wa maji safi na salama. Miradi mingi imekuwa ikitekelezwa kwa kutumia fedha nyingi, lakini baada ya muda mfupi maji hayapatikani. *(Makofi)*

Hivyo basi, katika miaka hii mitano, tunaweka mkazo mkubwa katika kuimarisha usimamizi kwenye utekelezaji wa miradi ya maji. Na hapa niseme, nakwenda kufanya mabadiliko makubwa ya ma-*engineer* wa maji huko kwenye mikoa kwa sababu fedha nyingi zimekuwa zikitoka Wizarani kwenda Mikoani, lakini utekelezaji kwenye mikoa unasuasua. Sasa walioshindwa kutuletea maji na kutumia fedha nyingi wakae upande watupishe tuingize damu mpya. Lengo ni kufikia azma ya kufikisha maji kwa wananchi kwa asilimia 95 mijini na asilimia 85 vijiji ifikapo mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na katika hilo nataka nimwambie Waziri wa Maji, yupo? Eeh, ile kauli yako ambayo na mimi niliikopa kwako unayowaambia wenzio ukinizingua tutazinguana, inarudi kwako. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa Waziri wa Maji - Mhe. Jumaa Hamidu Aweso, Alisimama)*

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, tunakwenda kutunisha Mfuko wa Miradi ya Maji. Tunakwenda kuangalia vyanzo vingine ambavyo vitakwenda kutunisha Mfuko wa Maji ili twende tukatekeleze upelekaji wa maji kwa wananchi kwa haraka, lakini kama nilivyosema tunakwenda kuondosha

utendaji mbovu na kuweka utendaji mpya. Sasa na hapo napo tukishindwa Waziri wa Maji kabla ya kusema mimi itabidi uondoke mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine tutakalokwenda kulifanya kwenye masuala ya maji ni utunzaji wa vyanzo vya maji na kulinda mazingira. Maeneo mengi yanapata shida ya maji kwa sababu, hakuna vyanzo vya maji au vimekauka kwa hiyo, tutakwenda kulinda na kutunza vyanzo vya maji, lakini kwa maeneo ambayo hayana kabisa vyanzo vya maji tunakwenda kuchimba mabwawa ya kuvuna maji ya mvua. *(Makofi)*

Vilevile tutaziimarisha Kamati za Maji za Mitaani na Vijijini ili ziweze kusimamia miradi yao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mahusiano na ushirikiano na mataifa mengine na taasisi za kidunia, Serikali ya Awamu ya Sita imejipanga kutekeleza shughuli za Kidiplomasia kuendana na Sera ya Diplomasia ya Uchumi. Hivyo basi, tutaimarisha na kukuza uhusiano na mataifa mengine pamoja na Jumuiya za Kikanda na Taasisi za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza azma hiyo, tunakusudia kuimarisha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Balozi zetu zilizoko nchi mbalimbali duniani, kwa kuajiri watumishi wenye sifa na weledi wa kazi na kusambaza vitendea kazi, pamoja na kutumia kiuchumi majengo na viwanja ambavyo ni mali ya Tanzania vilivyoko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafanya hayo kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji mzuri wa Diplomasia ya Uchumi na tutafungua na kuanzisha pia Balozi mpya, Konseli pamoja na vituo vya biashara kwenye miji ya kimkakati ili kutangaza vivutio vyetu vya utalii, kuvutia wekezaji na kutafuta masoko ya bidhaa zetu. Tutafanya uchambuzi wa kitaalamu utakaobaini nafasi ya kila Ofisi ya Ubalози katika kukuza biashara, uwekezaji na utalii. Uchambuzi huo ndio utatumika

sasa kupanga Maafisa kulingana na uwezo wa kila Ubalози.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo tutaendelea kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za Kimataifa, ikiwemo ushiriki wetu kwenye kulinda amani duniani. Tunakusudia pia kufanya mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2000 ili iendane na mahitaji ya sasa ya dunia. Maeneo mengine ni pamoja na kuendelea kulinda misingi ya demokrasia na uhuru wa watu pamoja na vyombo vya habari. Kama mnavyofahamu, uhuru na demokrasia ni msingi wa amani katika nchi na pia vinasaidia kuchochea maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba niseme kuwa, hakuna uhuru wa kidemokrasia usiolindwa na kusimamiwa na sheria, taratibu na kanuni. Hivyo basi, pamoja na demokrasia na uhuru wa watu, niwaombe Watanzania tujidhatiti kufanya shughuli zetu tukizingatia masharti ya sheria za nchi. Hapa vilevile katika kulinda uhuru wa kidemokrasia nakusudia kukutana na viongozi wa vyama vya siasa Tanzania ili kwa pamoja tuweke mwelekeo wa kuendesha shughuli za kisiasa zenye tija na maslahi kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, tutashirikiana pia na Mhimili wa Mahakama katika kuimarisha mifumo ya utoaji haki, ikiwemo kuendelea kujenga miundombinu ya Mahakama, kuongeza idadi ya Majaji na Mahakimu na kukuza matumizi ya TEHAMA ili kuongeza kasi ya kusikilizwa au usikilizwaji wa kesi na uwekaji mzuri wa kumbukumbu za Mahakama. Niombe Mahakama kupitia Jaji Mkuu kwamba vyombo vya utoaji haki vijielekeze zaidi au zielekeze nafsi zao zaidi katika kutenda na kuhukumu yaliyo ya haki kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na katika hilo, tutaendelea kuziimarisha taasisi nyingine za usimamiaji haki ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa

ya Mashtaka, Polisi, TAKUKURU, Magereza, na Taasisi nyingine za aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita kama ilivyokuwa ya awamu ya tano, itaendeleza jitihada za kuimarisha nidhamu na uwajibikaji kwenye utumishi wa umma. Tunakusudia kuimarisha taasisi na pia kuweka mifumo ya uwajibikaji, ambayo itahakikisha kwamba viongozi na watumishi wa umma katika ngazi zote wanawekewa malengo yanayopimika. Mfumo uliopo sasa ikiwemo mikataba kati ya kiongozi na walio chini yake pamoja na OPRAS tutaingalia upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutawapima viongozi na watumishi kwa namna wanavyotimiza majukumu yao. Hatutawaonea aibu viongozi na watumishi wazembe, wezi na wabadhirifu wa mali za umma. Tutaendeleza pia juhudi za kupambana na rushwa kwenye utumishi wa umma na wajibu huu wa wafanyakazi nataka niseme wajibu huu wa wafanyakazi wa umma ni lazima uendane na haki zao. Hivyo basi, tutasimamia mageuzi katika utumishi wa umma na kutazama maslahi ya watumishi, ikiwemo suala la upandishaji vyeo na mishahara. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tutaendelea na jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi, hususan makundi yale maarufu ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Pia tutaendelea kutoa mikopo ya asilimia 10 kupitia Halmashauri zetu kama mgao ulivyo na vilevile tutaendelea kuimarisha mifuko mingine ya uwezesaji wananchi kiuchumi, tutaendelea pia kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa wajasiriamali wadogo, machinga, mama lishe, baba lishe, waendesha boda, bajaji na watu kama hao, ikiwemo kwa kuwatengea maeneo mazuri ya biashara na kuwawekea miundombinu pamoja na kuviboresha vitambulisho vyao ili viwe na taarifa muhimu zitakazowawezesha kuendesha shughuli zao kwa uhuru bila

bughudha, lakini pia kutambulika kwenye Taasisi mbali mbali wanakofuata huduma mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya sanaa, michezo na utamaduni inakua kwa kasi kubwa. Vijana wetu wengi wamepata ajira kupitia sekta hii. Hivyo basi, kama ilivyoahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwenye miaka hii mitano tunakusudia kuikuza zaidi sekta hii, hususan kwa kuimarisha usimamizi wa masuala ya hati miliki ili wasanii waweze kunufaika na kazi zao, tutahuisa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili kuwasaidia wasanii wetu, ikiwemo kupata mafunzo na mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tutaanzisha kidogo kidogo kuanza kutenga fedha kwa ajili ya kuziandaa timu zetu za Taifa, zikiwemo za wanawake. Tumechoka kuitwa lile jina alilolisema Mzee Mwinyi tunakwenda nje na ushabiki mkubwa, tukirudi kichwa cha mwendawazimu. Kwa hiyo tutajitahidi kuiangalia sekta hiyo angalau basi ipate msukumo na kupandisha ari za wachezaji ili Tanzania nasi tuingie kwenye ramani ya wacheza *football*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala mengine ambayo yatapewa kipaumbele na Serikali ya Awamu ya Sita ni kuendeleza ujenzi wa Makao Makuu ya Serikali Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Aidha, kwa kuzingatia vigezo na sifa tutakuza usawa wa kijinsia kwa kuteua wanawake wengi zaidi. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, tutateua wanawake wengi zaidi katika ngazi mbalimbali za uongozi, lakini kama nilvyosema kuendana na sifa na vigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo tutazidisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya, uendelezaji na uboreshaji wa makazi wa wananchi, ambapo tutahakikisha vifaa vya ujenzi vinapatikana kwa gharama nafuu na mikopo ya ujenzi inapatikana kwa riba nafuu, tutaimarisha taasisi zetu

za utafiti na kuendelea kushughulikia kero mbalimbali za wananchi, ikiwemo migogoro ya ardhi kazi ambayo Waziri wa Ardhi ameifanya vizuri sana, lakini bado ana kazi kubwa mbele na tutamtaka asimamie bado kutatua migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaweka mkazo katika kushughulikia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi ili kupunguza athari zinazotokana na mabadiliko hayo kwa maisha ya watu na shughuli zao za kiuchumi na kijamii. Kitaifa mbali na Sheria yetu ya Mazingira ya mwaka 2004, Bunge liliridhia Mkataba wa Mabadiliko ya tabianchi wa Paris na tutaendelea kushirikiana na mataifa mbalimbali katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi. Tayari tumeandaa Mpango wa Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris ambayo itakwenda mwaka 2021 hadi 2026 unaolenga kujenga uwezo katika kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi katika sekta za kilimo, mifugo, misitu, nishati, uvuvi, maji, utalii, makazi, afya, miundombinu na kukabiliana na maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza masuala hayo yote niliyoeleza, Bunge hili lina umuhimu wa pekee sana, kama mnavyofahamu mbali na kutunga sheria, Bunge lina wajibu wa kuisimamia Serikali. Aidha, ninyi Wabunge ni wawakilishi wa wananchi na kwa maana nyingine ninyi ni sauti ya wananchi, sitarajii sauti za wananchi ndani ya nyumba hii tukufu ziende zikajadili mambo yaliyo nje ya kazi za nyumba hii. Kwa hiyo, bila ushirikiano na Bunge hili itakuwa vigumu sana kwa Serikali kuweza kutekeleza masuala yote niliyoyaeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, napenda kutumia fursa hii kuliomba Bunge hili tukufu kutoa ushirikiano mkubwa kwa Serikali. Tukosoeni pale inapobidi na naomba mtukosoe vikali sana, Mawaziri wangu wakileta vitu visivyoeleweka wakosoweni vikali sana, lakini wakosolewe katika lugha ya Kibunge. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, nami nataka niwaahidi kuwa Serikali itakuwa tayari wakati wote, kupokea ushauri wenu na pia ushauri wa watu wengine wenye nia ya kuletea maendeleo nchi yetu. *(Makofi)*

Nitumie pia fursa hii kuwaomba wananchi, kuendeleo kuiunga mkono Serikali kwa kudumisha amani, kuchapa kazi kwa bidii na bila kusahau kulipa kodi ili kwa pamoja tuweze kutimiza tuliyo yakusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge sasa naomba mniruhusu nitumie jukwaa hili la Bunge au Bunge lako Tukufu kusema mambo mawili madogo; la kwanza ni kuwaonya wale wote wanaodhani kuwa usimamizi wa mali za umma, kusimamia ukwepaji wa kodi, kusimamia uzibaji wa mianya ya kupoteza mapato kukemea uzembe na wizi yameondoka kuendana na kuondoka kwa Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli,... *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme Hayati mpendwa wetu amekwenda peke yake na kama nilivyosema siku ile tunamsindikiza kwamba maono, falsafa na mikakati aliyotuachia tunaendelea kuifanyia kazi. Hivyo basi wale wanaodhani yale yamekwenda naye wamejidanganya yapo na tunayatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona niliseme hili kwa sababu tayari kuna baadhi ya watu Mashirika yameanza kulegalega kwenye utendaji, wizi umeanza kushamiri katika baadhi ya maeneo, lakini kuna wawekezaji ambao walikuwa kwenye njia nzuri ya majadiliano na Serikali wameanza kuvuta nyuma. Nataka niwaambie kwamba mwendo ni ule ule. *(Makofi)*

*(Hapa Wabunge waliimba tuna imani na  
Mheshimiwa Samia)*

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, hapa tulipofika hatutakubali tena kurudishwa kwenye kuchezea

rasilimali za nchi kwa gharama ya maendeleo ya wananchi.  
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nilitaka kulizungumza hapa, na hapa nikemee vikali wale waliopo kwenye mitandao. Ndugu zangu dini zetu zinasema na ndio kanuni ya maisha, tunakuja duniani lakini tutaondoka duniani, na dini zetu zinasema kila nafsi iliyokuja duniani itapatwa na mauti. Lakini kila mauti yana sababu zake.

Ndugu zangu nimekuwa nikiona kwenye mitandao na nadhani wanaofanya hivyo wanajua kwamba hatutaweza kuwapata wanatumia mifumo hiyo huko mingine ambayo bado hatujakuwa na uwezo wa kuwatafuta. Lakini niwaambie tutawatafuta. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiona kwenye mitandao taarifa za uchonganishi. Taarifa tuliyopewa na madaktari wetu ya kifo cha mpendwa wetu ni kutokana na tatizo la dhaifu wa moyo ambao ameishi nalo kwa takribani miaka kumi. Kuna watu wanajitokeza katika mitandao huko, fulani na fulani na fulani wamempa sumu, fulani na fulani na fulani walikuwa wametega kitu hiki.

Sasa mimi niwaambie kama wana taarifa za maana waje tuwasikilize. Vyombo vya upelelezi na uchunguzi vipo, waje tuwasikilize, *short of that* wasimame kuleta uchonganishi ndani ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, taarifa wanazozitoa ni za kugonganisha ukoo na ukoo, makabila na makabila ni hivyo, waache kuleta uchonganishi ndani ya nchi. Lakini kama wanajidhatiti wanafanya hivyo kwa sababu hatutawapata, basi warudi tu kwa Mungu wao, wakajiulize kwamba hili wanalolifanya lina uhalali au lina maana gani? Warudi tu kwa Mungu kwa sababu nao ni viumbe pia warudi kwa Mungu wakajiulize. Je, wanayoyafanya ndio? Wangeambiwa wao hivyo wangekubali? Kwa hiyo, mimi nitumie jukwaa lako hili kukemea hayo mawili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia niseme hii ni mara yangu ya kwanza kwenye historia ya Taifa letu au nchi hii ni mara yetu ya kwanza kwenye historia ya Taifa letu kupata Rais mwanamke; kwa sababu hiyo, ninajua watakuwepo baadhi ya watu kama nilivyosema mwanzo wenye wasiwasi kwamba kutokana na jinsia yangu sitoweza kuyatimiza yote niliyoyasema hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie jukwaa hili kuwaondoa hofu kwamba kwanza, Mwenyezi Mungu hakuumba ubongo hafifu kwa mwanamke na ubongo makini kwa mwanaume hapana wote tulizaliwa sawa. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, makuzi na umakini wa akili hutegemea jamii inayokuzunguka na shughuli zinazokuzunguka katika makuzi yako. Nataka nikuhakikishieni kuwa nimekuzwa kwenye jamii sahihi na kwamba nina uzoefu wa kutosha kwenye Serikali, lakini pia kwenye chama changu cha siasa Chama cha Mapinduzi. Hivyo basi ninajamini kuwa ninao uwezo wa kuliongoza Taifa hili. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni kwamba haya niliyoyasema hapa siendi kukaa na kuyatekeleza peke yangu, nitashirikiana na Watanzania wote katika ngazi zetu tofauti tofauti. *(Makofi/Vigelegele)*

Hivyo wito wangu kwenu ndugu zangu Watanzania, tushirikiane, tushikamane na kuwa kitu kimoja katika kulijenga Taifa letu. Binafsi naamini, kwamba tukiwa na upendo, mshikamano na kuheshimiana, na kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, tutaweza kufika kule ambako sote tunamani tufika *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nimalizie kwa kumuomba Mungu alibariki Bunge hili pamoja na Wabunge wake, Mwenyezi Mungu aibariki Tanzania, na niseme nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi/Vigelegele)*

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Kazi lendelee.

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN - RASI WA JAMHURI YAMUUNGANO WA TANZANIA:** Ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Wabunge waliimba wimbo wa anaweza mama yetu huyo, anaweza kutufikisha anaweza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba taarifa ziende kila kona ya nchi yetu, nchi jirani na duniani kote kwamba Tanzania yuko Rais anaitwa Samia Suluhu Hassan na kwamba anaweza. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yako hii nzuri sana na tunakushukuru pia kwa kutuahidi kutusaidia na kufanya kazi na sisi Bunge, na sisi Bunge tunaahidi kabisa tutachukua nafasi yetu ya kukusaidia kazi ya kwenda pamoja na wewe na tukiwa pamoja na Mungu wetu tuna hakika tutafika. *(Makofi)*

Basi kwa niaba yetu nitafute mtu wa kutoa shukrani kwa niaba yetu hapa, sijui nielekee wapi! Hebu tujaribu Mheshimiwa Jumanne Kishimba. Mheshimiwa Kishimba karibu tafadhali kwa niaba yetu. *(Makofi)*

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, napenda kutoa shukrani zangu za dhati na za kipekee kwa kupatiwa nafasi hii kuwawakilisha Wabunge wenzangu kwa kutoa neno dogo la shukrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, kwa hotuba uliyoitoa na makofi yaliyoshangiliwa hapa nisingependa kuweka neno lolote kwenye hotuba hiyo ili nisije nikaipa shida kwenye masikio ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, sisi Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu tunayoimani kubwa sana juu yako na kwa hotuba ambazo umeanza kuzitoa toka umeingia madarakani wapiga kura wetu pia wamekuwa na imani kubwa sana. *(Makofi)*

Kwa niaba ya Wabunge wenzangu tutaendelea kuwa na wewe pamoja na Serikali yako tukisaidiana na wananchi na wapiga kura wetu wote kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania kwa imani kubwa wananchi waliyonayo juu yako Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, wote tumempoteza Rais wetu kipenzi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Lakini kwa nguvu hiyo hiyo Mwenyezi Mungu ametupatia wewe na sisi tutakuwa na wewe bila kinyongo wala shida yoyote tunakuahidi na kama ulivyoona makofi na ushangiliaji uliokuwepo toka mwanzo wa hotuba ni kuashiria kabisa Wabunge wanaimani kubwa na wewe Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais kwa kuwa nimepewa kuongea neno dogo la shukrani kama nilivyosema mwanzo na muda huu ni Mfungo wa Ramadhani mwezi huu, nisingependa kuwachelewesha watu na kukuchelewesha wewe nikutakie kila la kheri na hotuba yako hii sisi kama Wabunge tutajadili kwa muda wetu na tutajadiliana maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, nikutakie kila la kheri kwa mwezi Mtukufu huu wa Ramadhani na sisi tutafikisha salamu kwa wapiga kura wetu wa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, haada ya hayo nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Kishimba kwa kutoa salamu hizo kwa niaba yetu Wabunge wote tumpigie makofi ya shukrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, Bunge hili limesheheni watu wenye...., muda wetu hautoshi lakini limesheheni watu wenye busara nyingi sana, lina mchanganyiko wa kona zote za Watanzania kuanzia Pemba mpaka Kagera mpaka Mtwara, Kigoma, Tanga wapi, wanawake kwa wanaume wasomi wa kila aina na darasa la saba wamo pia Mheshimiwa Rais ni uwakilishi halisi kabisa wa Watanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa kama tulivyokumbushwa na Mheshimiwa Kishimba kwanza niwataarifuni kwamba Mheshimiwa Rais ameandaa futari kwa ajili yetu sote Waheshimiwa Wabunge wote, Watumishi wa Bunge na wageni wetu wote mlioko kwenye *galleries* msiondoke baada ya shughuli hizi tujiunge pamoja unapotoka mkono wa kulia kwa chini kidogo kuna eneo maalum lililoandaliwa kwa ajili hiyo, itakuwa vizuri kama kila mmoja wetu atapata japo kidogo maana futari ya Mheshimiwa Rais ni futari ya Rais, siyo kila siku utapata fursa ya aina hiyo, hii ni nadra sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa dakika chache sana nijaribu kuwatambulisha wageni maana wageni leo tunao wengi sana Mheshimiwa Rais, lakini nijaribu kutambulisha kwa haraka haraka tu baadhi ili tuweze kuwahi muda wetu kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Rais Mstaafu Awamu ya Pili Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaye Rais Mstaafu Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Tunaye Rais Mstaafu Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume. *(Makofi)*

Tunaye Rais Mstaafu Zanzibar Mheshimiwa Dkt Ali Mohamed Shein. *(Makofi)*

Tunaye Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza Mstaafu Tanzania Bara Mheshimiwa John Samwel Malecela. *(Makofi)*

Tunaye Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Fredrick Tluway Sumaye. *(Makofi)*

Tunaye Waziri Kiongozi Mstaafu Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha. *(Makofi)*

Tunaye Makamu wa Pili wa Rais Mstaafu kule Zanzibar Balazi Seif Ali Iddi. *(Makofi)*

Tunaye Spika Mstaafu wa Bunge la Tanzania Mama Anne Semamba Makinda, karibu sana mama yetu tumekumiss. *(Makofi)*

Tunaye Spika Mstaafu wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Pandu Ameir Kificho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, lakini pia tunao Maspika kama nilivyowatambulisha mwanzoni wa Baraza la Mawakilishi na Spika wa Bunge la Afrika Mashariki hapa mbele. *(Makofi)*

Tunao wenza wa Marais kipekee mama yetu Mama Maria Nyerere naambiwa amekuja, ahsante sana mama. *(Makofi)*

Yuko Mama Sitti Mwinyi, yuko Mama Shadia Karume, yuko Mama Mwanamwema Shein, yuko Mama Napone Sokoine, yuko Mama Asha Nahonda na yuko Mama Esther Sumaye. Utaona mama zetu wamenyanyuka kweli kweli kuja kushuhudia Rais wetu akihutubia Bunge. *(Makofi)*

Lakini pia wako wageni maalum ambao ni wake wa viongozi nitaomba kwa sababu ya dakika chache hizi nitambue uwepo wao wote.

Mheshimiwa Rais, ni wachache niwataje yuko Mama Mbonimpaye Mpango - Mwenza wa Makamu wa Rais, yuko Mama Mariam Mwinyi - Mwenza wa Rais wa Zanzibar, yuko Mama Mary Majaliwa - Mwenza wa Waziri Mkuu, yuko Dkt. Stergomona Tax - Katibu Mtendaji wa SADC, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, lakini tunao Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama Mkuu wa Majeshi - Jenerali Venance Mabeyo, ahsante sana. *(Makofi)*

Yuko Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) - Simon Sirro, yuko Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa - Ndugu Diwani Athumani Msuya, yuko Kamishna Jenerali wa Magereza - Meja Jenerali Suleiman Mzee,. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, yupo Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Dkt. Anna Makakala. *(Makofi/Vigelegele)*

Yuko Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji - Ndugu John Masunga, yuko Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU - Brigedia Jenerali John Mbung'o, yuko Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya - Ndugu Jerad Kusaya Msabila. *(Makofi)*

Yuko Mnadhimu Mkuu wa JWTZ - Luteni Jenerali Yacoub Mohamed, yuko Mnadhimu Mkuu wa Baraza la Usalama wa Taifa - Brigedia Jenerali Andrew Chakila, ahsante. *(Makofi)*

Tunao Makatibu Wakuu wakiongozwa na Balozi Hussein Kattanga - Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu wote tunao, karibuni sana na Naibu Makatibu Wakuu tunao pia mnawaona pale wote kwa ujumla wao. *(Makofi)*

Tunao Watendaji Wakuu wa Chama cha Mapinduzi ambapo tunaye Mheshimiwa Philip Mangula - Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara. *(Makofi)*

Tunaye Naibu Katibu Mkuu - Rodrick Mpogolo, tunaye Naibu Katibu Mkuu Zanzibar - Abdullah Saadala, na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma - Ndugu Godwin Mkanwa, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia tunao Watendaji Waandamizi wa Taasisi za Serikali wakiwemo CAG, Gavana wa Benki Kuu, TRA, Msajili wa Vyama vya Siasa, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi,



Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, wote hawa tunao nawakaribisha sana. (Makofi)

Lakini pia tunao uongozi wa Mkoa wa Dodoma, karibuni sana wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, tunao Wakuu wa Wilaya zote za Mkoa wa Dodoma pale walipo karibuni sana. Tunao Wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Dodoma, wote karibuni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Rais, tunao Mabalazi na Wakuu wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa kwa kweli ni *record* tangu miaka mingi hatujawahi kupata Mabalazi wengi kiasi hiki. Naomba Waheshimiwa Mabalazi wote msimame, ahsanteni sana. Ni heshima kubwa sana kwetu Bunge, lakini pia kwa Rais wetu kwa jinsi mlivyokuja kwa wingi namna hii tumefarijika sana Waheshimiwa Mabalazi, mtupelekee salamu katika nchi zenu. Kwa hiyo hawa ni mabalazi na wawakilishi wa Kazi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa ni wengi. Kwa hiyo muda kidogo hauko upande wetu. (Makofi)

Kwa kweli nina hakika wageni wetu kama mnavyoona karatasi yangu imejaa lakini kwa hali halisi ya muda ulivyo ninaomba mtukubalie wageni wetu wote tunatambua uwepo wenu na ujio wenu, ahsanteni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli zilizopangwa sasa zimekamilika naomba tuahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Hapa Msafara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiongozana na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Job Y. Ndugai ulitoka Ukumbini)*

*(Saa 11.56 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 23 Aprili, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*